# UFUMBUAJI WA MASHAIRI YA KISWAHILI: MFANO WA *MALENGA WA MVITA* NA *MALENGA WA VUMBA*

NA

MUNG'ATHIA ROBERT

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA.

2011

3808/3
Mung'athia, Robert
*Ufumbuaji wa mashairi ya kiswahili: mfano*
2012/382590
KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

## Ungamo

Tasnifu hii ni kazi yangu na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine.

______________________ 21/10/2011

MUNG'ATHIA ROBERT TAREHE

Tasnifu hii imetolewa kwa chuo kikuu kwa idhini yetu kama wasimamizi.

______________________ 24.10.2011

PROF. GEOFREY K. KING'EI TAREHE

NA

______________________ 24.10.2011.

DKT. EDWIN MASINDE TAREHE

**Tabaruku**

Kazi hii naitabaruku kwa wazazi wangu, Margaret Kathiu na Leonard Mulika. Mlijinyima mengi ili kuniwekea msingi imara katika mkondo wa masomo yangu.

Kwa mchumba wangu, Bi. Janice K. Ibuuri. Ulivumilia na kunihimiza niimalize kazi hii licha ya kutoielewa. Nakutakia kila la heri katika masomo yako ya chuo kikuu.

## Shukrani

Namshukuru Mungu kwa kunipa nafasi hii ili kuendelea na elimu yangu hadi nikafikia kiwango hiki. Ninatoa shukrani zangu kwa wasimamizi wangu Prof. King'ei na Dkt. Masinde kwa kuniongoza vizuri pamoja na mashauri mema waliyonipa nilipokuwa nikitayarisha kazi hii.

Sitamwacha nyuma mwenyekiti wa idara ya Kiswahili Dkt. Chacha kwa usaidizi wake. Shukrani zingine ziende kwa Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa kukubaliwa kuendeleza masomo yangu hapa pamoja na kupata mazingira mazuri ya kielimu chuoni.

Vile vile, natoa shukrani nyingi kwa mchumba wangu Bi. Janice K. Ibuuri na dada yangu Vierine Kaniru Mwenda walionisaidia kwa kila hali kukamilisha masomo yangu. Shukrani pia zitamwendea Mwalimu mkuu wa Shule ya Upili ya Wavulana ya Bute iliyoko Kaunti ya Wajir, Bw. Adan Abbas aliyenipa mazingira mema ya kufanya kazi na kuniruhusu mara kadha kutoka shuleni nilipohitaji kwenda kukutana na wasimamizi wangu chuoni.

Shukrani za mwisho ziwaendee walimu wenzangu: Bw. Kimathi mwambia, Bw. Geofrey, Bw. Paul Muchiri, Bw. Abdikadir, Bw. Bare na Bw. Hassan kwa kunisaidia kwa kila hali kufanikisha kazi yangu.

Mwisho, nasema ahsanteni nyote na hata wote wale ambao sikuweza kuwataja majina yao na Mungu awabariki.

## Ikisiri

Tasnifu hii imejadili suala la ufumbuaji wa mashairi ya Kiswahili ikizingatia diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*. Mashairi kumi kutoka diwani zote mbili yaliteuliwa kwa kuzingatia mada za unyumba, lugha na maliwazo,majonzi na maliwazo.

Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni nadharia changamano iliyotokana na nadharia mbili: nadharia ya uhistoria mpya na nadharia ya udenguzi. Mihimili ya nadharia hii changamano ilitumika kama dira ya kuongoza utafiti huu katika kuyafikia malengo yake.

Malengo ya utafiti huu yalikuwa ni pamoja na kubainisha kuwa mashairi kadha ni mafumbo, kubainisha vipengele vya lugha vilivyochangia kufumba maana au ujumbe wa mwandishi na kudhihirisha jinsi ya kupata fasiri tofauti za maana ya shairi ili kufanikisha uwasilishaji wa maudhui.

Data iliyotumika katika utafiti huu ilikusanywa maktabani. Tulipitia diwani mbalimbali za mashairi pamoja na vitabu vingine vya fasihi na nadharia, tasnifu na majarida yaliyochangia kuupa msingi utafiti huu kinadharia na kimpangilio wa data.Matokeo ya uchanganuzi wa data yalidhihirisha kwamba mashairi kadha ya Kiswahili ni mafumbo. Aidha, udadisi wa kina wa mada, vipengele vya lugha vilivyotumika katika shairi, mtiririko wa ujumbe wa mwandishi kutoka ubeti wa kwanza hadi ubeti mwisho na kibwagizo hufanikisha ufumbuaji wa ujumbe wa mwandishi.

Mwisho, mapendekezo ya utafiti zaidi yalitolewa kuhusiana na matokeo ya utafiti huu.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

## Maelezo ya istilahi

Arudhi - Hizi ni kanuni au sheria za utunzi wa mashairi ya Kiswahili ya kimapokeo.

Fumbo - Hutumiwa kueleza hali fulani ambayo ina ufiche na inahitaji kufikiri na kudadisi kwa undani ili kutambua kilichofichwa.

Muundo - Mjengo wa shairi au Jinsi shairi zima linavyoonekana.

Maana - Fikira, wazo au ujumbe mkuu uliomo katika shairi.

Nasiha - Ni dhana inayotumiwa na baadhi ya wahakiki kuelezea mtindo wa msemo wa fumbo ambao unaonyesha ukinzani au upotoshaji wa maana ingawa kwa ndani kuna ujumbe mzito.

Shairi - Ni utungo wenye muundo maalum, mpangilio mahususi wa maneno, unaotumia lugha ya mkato na unaogusia swala fulani.

Uchanganuzi - Ni hali ya kuvunja na kuigawanya kazi ya kifasihi katika visehemu vyake mbalimbali kwa nia ya kuvieleza. Pia, huitwa uchambuzi.

Udenguzi - Ni mkabala wa kiuhakiki unahusishwa na Jacques Derrida kueleza falsafa ya lugha inayochunguza kutotegemewa kwa lugha kukifikia kitu kinachokuweko kando na lugha hiyo.Hupinga mtazamo kuwa kazi ya kifasihi ina kitovu cha kimaana.

Ujumbe - Ni dhana inayotumika kueleza taarifa ambazo msanii au mtunzi hutoa kwa wasomaji au kwa hadhira yake kama njia mojawapo ya kuhakikisha kuwa dhamira yake imetimia.

Uhistoria mpya - Ni mkabala wa kiuhakiki ambao hutoa maelezo madhubuti ya miktadha ya kifasihi kihistoria. Ni nadharia inayohusishwa na Michel Foucault na Raymond Williams.

Waswahili - Ni jamii inayojumuisha watu mbalimbali wenye asili ya Pwani na Bara ya Afrika Mashariki na watumiao Kiswahili katika mawasiliano na utunzi wao.

## Yaliyomo

Mada ........................................................................................i

Ungamo ......................................................................................ii

Tabaruku ....................................................................................iii

Shukrani.....................................................................................iv

Ikisiri ........................................................................................v

Maelezo Ya Istilahi ......................................................................vi

Yaliyomo ....................................................................................viii

**SURA YA KWANZA ...........................................................................1**

1.0 Utangulizi..................................................................................1

1.1 Swala la utafiti..........................................................................8

1.2 Maswali ya utafiti.......................................................................9

1.3 Malengo ya utafiti.......................................................................9

1.4 Sababu za kuchagua mada.........................................................10

1.5 Upeo wa utafiti...........................................................................12

1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada.......................................................12

1.7 Misingi ya nadharia....................................................................16

1.8 Mbinu za utafiti..........................................................................20

1.9 Muundo wa utafiti.......................................................................20

1.10 Mahali pa utafiti.......................................................................21

1.11 Sampuli na njia za kuteua sampuli.............................................22

1.12 Njia za kukusanya data na vifaa vya utafiti.................................23

1.13 Uchanganuzi wa data.....23

1.14 Uwasilishaji wa matokeo.....24

**SURA YA PILI .....26**

Historia ya waandishi wa *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*.....26

2.0 Utangulizi.....26

2.1 Historia ya mwandishi wa *Malenga wa Mvita*.....26

2.2 Taathira katika utunzi wa Ahmadi Nassir.....28

2.3 Falsafa ya Ahmadi Nassir.....31

2.4 Historia ya mwandishi wa *Malenga wa Vumba*.....33

2.5 Maisha ya awali ya Boukheit Amana.....35

2.6 Falsafa ya Boukheit Amana.....38

2.7 Eneo la Kijiografia na utunzi wa *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*.....42

2.8 Jamii ya Waswahili na utunzi wa *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*.....44

2.9 Imani, dini, lugha ya Kiswahili na utunzi wa Ahmadi Nassir na Boukheit Amana.....48

2.10 Shughuli za kiuchumi na umbuji wa *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*.....53

2.11 Kiishilio.....56

**SURA YA TATU.....59**

Matumizi ya lugha katika *Malenga na Mvita* na *Malenga wa Vumba*......59

3.0 Utangulizi......59

3.1 Arudhi ya ushairi na migogoro ya utunzi......63

3.2 Arudhi......63

3.3 Migogoro ya utunzi......65

3.4 Ufumbaji wa mashairi......68

3.5 Mashairi yasiyo mafumbo......71

3.6 Mashairi ya kimafumbo/ mashairi mazito......72

3.7 Sababu za kutumia mashairi ya kimafumbo......77

3.8 Ufumbaji wa kufumba watawala dhalimu na mifumo dhalimu ya kisiasa......78

3.9 Ufumbaji wa kitasfida......84

3.10 Ufumbaji wa kucheza na lugha......89

3.11 Kiishilio......91

**SURA YA NNE ......93**

Ufumbuaji wa mashairi katika diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*......93

4.0 Utangulizi......93

4.1 Njia za kufumbua mashairi......96

4.2 Maudhui yanayohusu unyumba......97

4.3 Owa......97

4.4 Nenda na bahati yangu......100

4.5 Wajao na kwenda....102

4.6 Leo homa....104

4.7 Maudhui yanayohusu matumizi ya lugha....105

4.8 Mkufuu na mwanafuu....106

4.9 Kisichoumbwa na M'ngu....108

4.10 Dunia jukwaa....109

4.11 Alfaqru fakhri....111

4.12 Maudhui yanayohusu maliwazo, majonzi na makiwa....113

4.13 Kullu nafsin dhaaiqatul mawt....113

4.14 Inna lillahi....115

4.15 Kiishilio....117

**SURA YA TANO....119**

Hitimisho....119

5.0 Utangulizi....119

5.1 Eneo la kazi kwa jumla....119

5.2 Matokeo, matatizo na mafanikio....121

5.3 Mapendekezo....124

Marejeleo....126

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Madhumuni ya utafiti huu ni kujadili ufumbuaji wa ujumbe au maana ya mashairi ya Kiswahili. Ingawa kazi hii haijishughulishi na historia ya fasihi na maendeleo yake maana hiyo yahitaji nafasi yake maalumu, litakuwa ni jambo zuri kueleza kwa mukhtasari dhana ya fasihi kwa jumla.

Fasihi, ukiwemo ushairi, ni taaluma inayojengwa na maneno katika fani maalumu ili kutolea makusudi au maudhui ambayo humzingatia binadamu maishani (Masinde, 2003:36). Mwanafasihi hutumia ubunifu kuteua, kupanga, na kunakili tajriba mbalimbali za maisha. Hivyo, fasihi iwe ni simulizi au andishi, ni sanaa ya lugha. Fasihi hutumia maneno kisanaa kumtazama binadamu na uhusiano wake na wenziwe, mazingira yake, viumbe vingine na itikadi kwa jumla kibunifu ili kusheheni imani na matukio katika jamii yake.

Jambo la kihistoria litokeapo, fasihi hujaribu kulisawiri na kulihifadhi kisanaa. Hili linaafiki mhimili wa nadharia ya Uhistoria mpya unaodai kwamba fasihi hurejelea, nayo hurejelewa na vitu kando yake kwenye mazingira. Kwa hivyo, jambo la kihistoria litokeapo, fasihi hujaribu kuliteka kwa kulihifadhi kisanaa. Hivi ndivyo ilivyo na ushairi wa Kiswahili katika nyakati tofauti Kihistoria na pia maeneo tofauti Kijiografia.

Lugha ni chombo cha fasihi. Kwa hivyo, ni muhimu msomaji wa kazi ya kifasihi adadisi kwa makini namna lugha hiyo ilivyofinyangwa. Lugha iliyotumiwa na mwandishi ilichimbuka katika mazingira ya wasanii kwa mujibu wa wakati. Kwa hivyo, lugha hiyo hung'amuliwa au kufasiriwa tu katika muktadha huo wa utunzi.

Fasihi ina misingi yake katika ubunifu. Hivyo, uchambuzi wa fasihi haukamiliki bila ya kuutalii ujumbe wa msanii pamoja na mbinu za kisanaa anazotumia kuuwasilisha ujumbe huo (Syambo na Mazrui, 1992).

Kwa jumla, tunaweza kusema kwamba fasihi, ukiwemo ushairi ni sanaa inayotumia lugha ili kuelezea maisha ya binadamu na mazingira yake kwa mapana na marefu. Fasihi hufungamana moja kwa moja na jamii, na hujishughulisha na maisha ya binadamu na jinsi anavyoingiliana na mazingira yake.

Hayati Mathias Mnyampala katika dibaji ya diwani yake mwenyewe alikuwa na haya yafuatayo ya kusema:

"Ushairi ni msingi wa maneno ya hekima tangu kale. Ndicho kitu kilicho bora sana katika maongozi ya dunia kwa kutumia maneno ya mkato na lugha nzito yenye kunata iliyopangwa kwa urari wa mizani na vina maalumu kwa shairi…"(1979:vii)

Hapa tunaona dhahiri kwamba Mnyampala anauona ushairi ukiwa umejengwa na vitu viwili mahususi – maneno ya hekima na sanaa yenyewe (lugha ya mkato, nzito, yenye kunata na iliyopangwa kwa urari wa mizani na vina).

Abdilatif Abdalla (1972) anapojaribu kueleza maana ya ushairi pia anatia mkazo mkubwa katika fani na sanaa yenyewe. Hata hivyo, naye kama walivyo watangulizi wake, anakubali kwamba maudhui ni sehemu madhubuti na muhimu kabisa katika ushairi.

Anasema utungo ufaao kupewa jina la ushairi si utungo wowote bali tu ni utungo ambao katika kila ubeti wake kuna ulinganifu wa vina vitukufu vilivyopangwa kimoja baada ya chenziye; wenye vipande vilivyo na ulinganifu wa mizani zisizopungufu na zisizozidi.

Abdalla anasema kwamba vipande hivyo lazima viwe vimetandwa na maneno ya mkato maalumu na yenye lugha nyofu, tamu na laini, lugha ambayo ni tetelezi kwa ulimi wa kuitamka, lugha ambayo ina uzito wa fikra, tamu kwa mdomo wa kuisema, iwe tumbuizi kwa masikio ya kuisikia na ambayo inaweza kuathiri moyo uliokusudiwa na kama ulivyokusudiwa kuadhirika.

Mawazo ya washairi hawa takriban yamo katika mshabaha mmoja. Wote wanaafiki kwamba mawazo mazito ni kitu muhimu sana katika ushairi lakini mawazo mazito, maono na hisi za ndani peke yake haziwezi kuitwa ushairi ila kwa kujengwa na sanaa maalumu; na kwamba sanaa hiyo sharti iwe na vina, mizani, maneno ya mkato na lugha ya kunata. Baadhi ya wataalamu wa Kiswahili wamewahi kutoa hoja kwamba vina, mizani na kadhalika si vitu ambavyo ni lazima viwemo katika ushairi na kwamba hayo ni mawazo ya kimapokeo ambayo hayana budi kupigwa vita na 'wanamapinduzi'.

Mashairi mengi hutungwa kwa lugha nzito, isiyo wazi na isiyoeleweka moja kwa moja kwa wasomaji. Lugha ya aina hii husitiri au hufumba ujumbe wa mwandishi. Hivyo, lugha hiyo inakuwa ya kimafumbo na kwamba inahitaji uchanganuzi wa kina ili kumwezesha msomaji au msikilizaji kuielewa ujumbe au maana ya shairi.

Ujumbe wa shairi lililofumbwa hupatikana au hufumbuliwa na msikilizaji kwa kufumbua au kuwaza [Wamitila 2003:105].

Mafumbo huundwa kwa matumizi ya tamathali mbalimbali. Kupitia tamathali hizo maana na amali tofauti za Mswahili zinadhihirika. Isitoshe, kupitia tamathali hizo,

mtunzi anaweza kusawiri na kuwasilisha maudhui yake kwa njia inayoeleweka. Lugha ya aina hii hufumba ujumbe wa mwandishi. Hivyo, lugha hiyo inahitaji uchanganuzi wa kina ili kumwezesha msomaji au mlengwa kuelewa maana ya kifasihi ya utungo unaohusika.

Hivyo, utafiti huu umechunguza matumizi ya mashairi ya kimafumbo katika kuwasilisha ujumbe wa *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba.*

Massamba (2003:69) anadai kwamba kimaudhui mashairi yanaweza

Kugawika katika matapo makubwa mawili:

a) Mashairi bayana

b) Mashairi ya kuzama

Maoni ya Massamba ni kwamba mashairi bayana ni mashairi yasiyomhitaji mtu kusukasuka mawazo au kufikiri sana ili kuweza kung'amua maana iliyokusudiwa. Haya ni mashairi ambayo yanaeleweka kwa urahisi yanaposomwa. Msomaji au msikilizaji huipata maana iliyomo katika shairi moja kwa moja.

Mashairi ya kuzama kwa upande mwingine ni mashairi ambayo humhitaji msikilizaji au msomaji kufikiri sana ili aweze kung'amua maana iliyokusudiwa. Mashairi haya ya kuzama yanaweza kugawanywa katika sehemu mbili:

Kuna mashairi ambayo hutumia lugha nzito lakini ya moja kwa moja. Picha na ishara nyingi hutumika si kwa kutaka kumkanganya msomaji bali kwa kutaka kumvuta hisia zaidi.

Pili, kuna yale ambayo ni tambo. Mshairi anaweza kutoa tambo yake akimtaka mtu au mshairi mwingine aitambue au aifumbue. Katika mashairi ya tambo mshairi huwa ana madhumuni makubwa matatu:

Ama, anataka 'kufunga nyama', kusema mtu fulani kistaarabu, au huwa anachelea kukisema waziwazi anachotaka kusema yasije yakampata makubwa baada ya kujulikana yale yasemwayo.

Kutokana na maelezo, haya mashairi yanaweza kugawika makundi mawili: mashairi ya kawaida ambayo hutungwa kwa lugha rahisi na huwa rahisi kueleweka; na mashairi ya kimafumbo au mashairi mazito ambayo hufumba ujumbe wa mshairi kwa lugha nzito na ya kitamathali. Utafiti huu umejishughulisha na uchanganuzi wa mashairi ya kuzama au ya kimafumbo.

Mashairi yana mshindo na mdundo yanaposemwa, yanapoimbwa au yanaposomwa. Basi, yamkini sana kuwa asili ya mashairi ya Kiswahili ni nyimbo. Shairi hutumiwa kimafumbo, kuichezea lugha kwa ujuzi na uhodari, kuhifadhia maneno mazito na magumu na vile vile, katika mashindano na mapambano ya washairi.

Aidha, shairi ambalo utalisoma na halafu usipate chochote ndani yake litakuwa halina manufaa (Kibao, 2003). Kuna umuhimu mkubwa wa kutoa mwongozo wa uchanganuzi wa maana ya shairi zima.

Aidha, mshairi hatumii kipawa chake kwa madhumuni ya kuwakenga au kuwatinga wasikilizaji au wasomaji wake. Bali haja yake ni kuyafichua mawazo



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

yaliyomsonga katika nafsi kwa lugha ambayo inamtoka kwa tabia, ili kuyapa sura iliyo kamili yale mambo ambayo yamemlemea (Chiraghdin, 1971).

Tangu zamani, mashairi yalikuwa yakitungwa kimafumbo. Mashairi hayo yalihitaji ujuzi na tajriba pana ili kuyafumbua (Chiraghdin, 1971). Mashairi ya Kipemba, Kimvita na maeneo yaliyo Kaskazini mwa Uswahilini kama vile Lamu, Siu na Pate yalikuwa mafumbo.

Mashairi ya Kimvita yalikuwa yakiitwa 'kufunga nyama'. Iwapo msomaji au msikilizaji angeshindwa kufumbua fumbo alitoa 'mji' ili apate kufumbuliwa fumbo hilo. Washairi wa Kaskazini walivikwa 'Uguni' na Shehe wa Malenga iwapo wangeshindwa kufumbua ujumbe wa shairi (Chiraghdin, 1971:7).

Kulingana na Mwangi (2005) shairi zima linaweza kuwa 'sitiari kuu'. Mchanganuzi huyu wa mashairi anadai kwamba kufasiri sitiari kuu kunaweza kumtatiza msomaji iwapo hana uwezo wa kufasiri sitiari iliyotokea katika mshororo mmoja. Utafiti huu umechanganua shairi zima kama fumbo na kuibua maana ya kijumla ya shairi hilo.

Ushairi umekuwa ukikaririwa tu au kuimbwa kama nyimbo na hivyo, kufurahiwa jinsi hiyo hiyo bila kuzingatia sana taswira zilizotumika katika kukamilisha ubunifu na ujumbe uliolengwa kuwasilishwa (Njogu na Chimera 1999:215). Usomaji wa aina hii ndio unawafanya wasomaji kutofahamu ujumbe wa mtunzi na kupelekea heshima ya fani hii kushuka hadhi na kuambiwa kuwa si fani yenye maana (Kibao 2003). Utafiti huu unanuia kubadilisha mkondo huu wa usomaji na kufungua ukurasa mpya wa usomaji na uhakiki wa mashairi.

Ama shairi huwa gumu ikiwa kulifahamu shairi hilo ni lazima tulijue hali na wakati lilipotungwa. Vile vile, ushairi una siri ya kukunja visa na kuficha siri (Chiraghdin, 1971). Msamiati wa washairi au watunzi huwa umekiuka kanuni nyingi za utunzi. Msamiati unaotumika kwa kiasi kikubwa ni wa kikale au wa kilahaja.

Mambo mengine ambayo yanaweza kulifanya shairi kuwa gumu kulifumbua kando na msamiati ni kufananisha mambo au vitu (Kibao, 2003). Iwapo mtunzi atatumia maneno kama 'tunda', 'ndege' au 'ua' na awe ni mwanamme anaweza kuwa anamaanisha au anazungumzia mwanamke.

Aidha, kuna misemo mingi ya kujigamba kama vile 'mti mle', 'maji male' na 'kina' yanayotumika na watunzi kuwatisha watunzi wengine. Utafiti huu umebainisha kuwa cha muhimu ni kujua makusudio ya mtunzi.

Mashairi ni ufundi wa lugha ya mkato, na uwasilishaji wa ujumbe kwa maneno haba kuliko hadithi. Kwa hivyo, mwalimu wa ushairi anatakikana awe ameutalii sana msamiati wa lugha ya Kiswahili na vile vile awe mjuzi wa kutambua kilichofumbwa katika taswira kemkemu (Njogu na Chimera, 1999). Utafiti huu umejishughulisha na jinsi mashairi ya kimafumbo yanavyoweza kufumbuliwa na kuweka ujumbe wazi kwa wasomaji na wasikilizaji.

Aidha, utafiti huu umehakiki mashairi kadha kutoka diwani za *Malenga wa Vumba na Malenga wa Mvita* kama mifano tu ya mashairi ya kimapokeo yenye ujumbe ulifumbwa.'

## 1.1 Swala la utafiti

Sanaa ya ushairi hutumia lugha ya kimafumbo na hivyo, hugubika maana iliyomo. Ili kupata kuielewa maana hiyo, mfasiri hulazimika kuchanganua maana ya jumla ya shairi lote. Hata hivyo, hakuna mbinu, hatua au njia maalumu zilizokubalika ambazo mweye kufasiri maana ya shairi anaweza kufuata katika ufumbuaji.

Kwa upande wake, Amri Abedi (1954) alipendekeza kuwa maana ya shairi hutegemea kueleweka kwa maana ya kila ubeti katika shairi. Abedi alidai kuwa kila ubeti unajitosheleza kimaana na hautegemei beti zingine ili kueleweka.

Hata hivyo, utafiti huu unaonelea kuwa maana hasa ya utungo wa shairi hutegemea kufumbuliwa na kueleweka kwa shairi lote kijumla wala si kila ubeti peke yake. Ama, shairi linaweza kuwa na beti kama nane hivi, lakini moyo wake au kiini chake kikawa katika ubeti mmoja (Kibao 2003:110).

Mbinu iliyotumika na utafiti huu ni kuchanganua maana za mada ya shairi, mtiririko wa ujumbe kutoka ubeti hadi mwingine, kibwagizo iwapo kipo, msamiati na hatimaye maana ya jumla ya shairi zima.

Nadharia ya Uhistoria mpya imeuwezesha utafiti huu kupata maana kwa mujibu wa muktadha wa historia ya jamii wakati wa utunzi wa mashairi.

Isitoshe, kwa kuzingatia Nadharia ya Udenguzi, utafiti huu umedhihirisha hatua muhimu katika ufasiri wa maana katika shairi la kimafumbo. Pia, utafiti umebainisha kwamba shairi linaweza kuwa na maana nyingi zisizolingana.

Utafiti huu umejishughulisha na ufumbuaji wa mashairi ya *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba* kama kielelezo cha ufumbuaji wa mashairi ya Kiswahili. Kazi hii imewafaidisha wasomaji na wasikilizaji wa mashairi kwa sababu wakiyafumbua mashairi wanapata maadili na mafunzo mengi yanayotokana na washairi ambao wengi wao ni wenye ujuzi na tajriba mbalimbali za kimaisha.

## 1.2 Maswali ya utafiti

Utafiti huu ulilenga kuyajibu maswali yafuatayo:

i. Je, ni sifa zipi zinazodhihirisha kwamba shairi ni fumbo?

ii. Je,ni mbinu gani za lugha hutumiwa na mtunzi au mshairi kufumba ujumbe wake?

iii. Je, kuna fasiri tofauti tofauti za maana za mashairi?

## 1.3 Malengo ya utafiti

Utafiti huu umeongozwa na malengo yafuatayo:

1) Kubainisha kwamba mashairi kadha ni mafumbo.

2) Kubainisha vipengele vya lugha vinavyochangia kufumba ujumbe wa mshairi.

3) Kubainisha kwamba ujumbe katika shairi unaweza kufasiriwa kwa njia tofauti tofauti kutegemea hali tofauti za kuelezea maana.

## 1.4 Sababu za kuchagua mada

Baada ya kupitia mashairi kadha imebainika kuwa baadhi ya mashairi yana ujumbe uliofumbwa na kwamba yanahitaji uchanganuzi wa kina ili yaweze kueleweka kwa wasomaji na wasikilizaji. Baadhi ya mashairi tuliyoyapitia ni kutoka diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba.*

Sababu za kufanya utafiti huu ni kama zifuatazo:

1) Watafiti kadha wamezungumzia maudhui ya mashairi. Hata hivyo, hakuna aliyechunguza maudhui ya mashairi ya kimafumbo. Washairi hufumba ujumbe wao na kuyafanya mashairi yao vitendawili ambavyo vinamhitaji msomaji kuvitegua ili kupata ujumbe uliolengwa na mtunzi. Utafiti huu umebainisha kuwa shairi linaweza kuwa fumbo moja ambalo limebana ujumbe wa mtunzi.

2) Washairi hutungia mada kadha ambazo zinatokana na mazingira na maisha ya kila siku ya binadamu. Miongoni mwa mada hizo ni nasiha, elimu, siasa masaibu na maliwazo, unyumba na kadhalika. Huku tukijua kuwa washairi wengi huwa na ujuzi na tajriba pana kuhusiana na stadi za maisha ni muhimu sana kuwabainishia wasomaji kuwa shairi mashairi mengine ni mafumbo na pia, kutoa mwelekeo wa jinsi ya kuyafumbua na kufaidika na ujumbe wa mshairi.

3) Utafiti huu utayafumbua mashairi na hivyo, kuwafaidisha wasomaji wa lugha, wanafunzi wa shule za msingi, sekondari pamoja na vyuo, wataalamu wa mashairi na taaluma ya ushairi kwa jumla. Hii ni kwa sababu mashairi yataeleweka kama mafumbo na kuwatolea wasomaji na wasikilizaji njia na mbinu za kuyafumbua. Pili, wanalugha wataelewa mbinu za washairi za kufumba mashairi pamoja na msamiati unaotumika. Wanafunzi na walimu watakuwa na

mwelekeo chanya kuhusiana na somo la ushairi kwa sababu watakuwa sasa wanaliangalia shairi lote kama fumbo tofauti na masomo yale mengine ya kifasihi kama riwaya na hadithi fupi. Taaluma ya ushairi itaimarika zaidi kwani wasomaji na waandishi wa mashairi watakuwa na mwamko mpya. Maudhui na malengo ya washairi yatawekwa wazi zaidi na kuwafaidisha wanajamii wengi.

4) Uchanganuzi huu ni muhimu kwa sababu utakuwa kielelezo cha uchanganuzi wa kazi nyingine za washairi tofauti tofauti. Mashairi yakifumbuliwa yatawafaidisha wasomaji na jamii kwa jumla kwa sababu watapata mafunzo kemkem na maadili kutokana na ujuzi na tajriba za watunzi wa mashairi.

5) Uchanganuzi wetu umehusisha na kulinganisha diwani mbili ambazo ni *Malenga wa Mvita* ambayo imetungwa katika lahaja ya Kimvita pamoja na *Malenga wa Vumba* iliyotungwa katika lahaja ya Kivumba. Waandishi wa diwani hizi wameonyesha uwezo wa kuyasawiri maudhui mazito kama yale yawezayo kusawiriwa na lugha nyinginezo za kigeni kwa njia sawa au kwa njia iliyo bora zaidi.

6) Katika utunzi wao, Ahmadi Nassir na Boukheit Amana wameonyesha uwezo wao wa kuchota maudhui kutoka jamii zao. Kama wasemavyo Njogu na Chimera (1999) fasihi haiwezi kuzuka kwenye ombwe tupu. Kutokana na wazo hili, utafiti huu umechunguza jinsi mazingira, jamii na historia, yalivyochangia matumizi ya mashairi ya kimafumbo.

### 1.5 Upeo wa utafiti

Utafiti huu umechanganua ujumbe wa mashairi ya kimafumbo katika diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba.* Tumebainisha ujumbe kamili wa mtunzi na lengo lake kwa wasomaji wake. Utafiti huu umekitwa katika diwani hizi mbili tu. Mashairi mbalimbali yaliyotungwa kwa lugha ya kimafumbo yaliteuliwa kwa kuzingatia mada zifuatazo:

*Malenga wa Mvita*

(a) Unyumba- 'Owa' (uk.158), 'Nenda na bahati yangu' (uk.160),

(b) Lugha- 'Mkufuu na mwanafuu' (uk.65), 'Kisichoumbwa na Mungu' (uk.59),

(c) Masaibu/ majonzi na makiwa- 'Kullu nafsin dhaaiqatul mawt' (uk.167),

*Malenga wa Vumba*

(a) Unyumba- 'Mpende akupendae' (uk.91), 'Leo homa'(uk.93)

(b) Lugha- 'Dunia jukwaa' (uk.35), 'Alfaqru fakhri' (uk20)

(c) Masaibu na maliwazo- 'Inna Lillahi' (uk.109)

Aidha, utafiti umezingatia historia fupi ya watunzi wa diwani zilizoteuliwa, mazingira ya utunzi yakiwa ni pamoja na yale ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ili kuonyesha yalivyochangia katika utunzi wa mashairi ya kimafumbo.

Utafiti huu haukushughulikia kazi zingine za washairi hawa pamoja na za watunzi wengine kwa sababu muda haukuruhusu.

### 1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Tafiti chache zimeshughulikia utanzu wa ushairi katika kuhakiki matumizi ya lugha, hususan mashairi ya lugha ya kimafumbo. Hata hivyo, baadhi ya walioshughulikia mada zinazohusiana na utafiti huu ni kama vile Chacha (1987).

Mtaalamu huyu alishughulikia maana na ufasiri wa ushairi wa Kiswahili. Chacha alichunguza jinsi mabadiliko ya kijamii na kiuchumi ya Waswahili wa Mvita yalivyoathiri matumizi ya jazanda katika mashairi. Utafiti wa Chacha ulitusaidia kufahamu jinsi aina mbalimbali za jazanda zilivyotumika na Wamvita katika utunzi wa mashairi.

Swali letu ni je, matumizi yao yalikuwa ni jazanda ndogo kama sitiari na tashbihi au ni shairi lote lililofumbwa kama jazanda moja au sitiari kuu?

*Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba* ni diwani zilizo na mashairi mengi yanayotungwa kwa lahaja ya Kimvita. Aidha, watunzi wa diwani hizi waliwahi kulelewa Mvita na bila shaka waliathiriwa na jamii hiyo. Hata hivyo, utafiti wetu utakuwa tofauti kwani utakuwa unachanganua baadhi ya mashairi ambayo tayari ni ya kimafumbo na kuyachanganua kwa kutumia mseto wa nadharia ya Udenguzi pamoja na ile ya Uhistoria Mpya.

Ndungo (1985) alichunguza usawiri wa mwanamke katika Utenzi wa Mwanakupona. Kazi yake ilitusaidia kuuelewa zaidi mtazamo wa kitamaduni na kijamii wa Waswahili kuhusu mwanamke. Ujuzi huu ulisaidia uchanganuzi wa mashairi yanayohusu unyumba katika diwani ya *Malenga wa Vumba* na *Malenga wa Mvita*.

Momanyi (1991) alichunguza matumizi ya taswira katika Utenzi wa Al- Inkishafi. Mashairi kadha ya *Malenga wa Vumba* na *Malenga wa Mvita* yametumia taswira ndogo ndogo na pia mengine ni taswira kuu, yaani shairi zima linazua taswira. Kwa mfano, shairi la 'Dunia jukwaa' katika *Malenga wa Vumba* (Uk. 35).

Utafiti wa Momanyi (1998) ulihusu namna mwanamke wa Kiislamu alivyosawiriwa katika ushairi wa Kiswahili. Wakaazi wengi wa pwani, walikotungia mashairi yao Boukheit Amana na Ahmad Nassir ni Waislamu. Mashairi mengi pia yaliathiriwa na dini ya kiislamu na hasa mtazamo na nafasi ya mwanamke. Kupitia kazi ya Momanyi, mtafiti aliweza kuchanganua mashairi ya unyumba na yale yanayohusu shughuli za wanawake katika diwani za *Malenga wa Vumba* na *Malenga wa Mvita.*

Masinde (1992) alichunguza dhamira na mtindo katika Mashairi huru na baadaye mwaka wa (2003), akachunguza maendeleo na mabadiliko ya maudhui katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti huu umefaidika kutokana na kazi za Masinde kwa sababu maudhui ndiyo huchangia au kutoa ujumbe wa jumla wa mwandishi.

Nyanchama (2004) alishughulikia matumizi ya Taswira na Ishara katika *Sauti ya Dhiki.* Tumefaidika na uchunguzi wake kwa kuzingatia aina mbalimbali za taswira na ishara. Hata hivyo, utafiti huu ulitofautiana na wake kwa sababu tumeangazia jinsi mtunzi ametumia nadharia ya udenguzi kuyachanganua baadhi ya mashairi ya kimafumbo katika diwani ya *Malenga wa Vumba* na *Malenga wa Mvita.*

Mwangi (2005) alichunguza ufunzaji wa mashairi katika shule za Sekondari. Alishughulikia 'ugumu wa ushairi' kwa wanafunzi na walimu wao. Utafiti wetu ulifaidika kutokana na matokeo ya utafiti huu kwa sababu ulituelewesha kwa nini wanafunzi na waalimu hudai kwamba mashairi ni magumu. Aidha, tulichunguza zaidi yale aliyotaja kama matumizi ya lugha ya tamathali pamoja na 'sitiari kuu' kwa muktadha wetu tukiita fumbo. Tulitofautiana na uchunguzi wake kwa sababu tulichukua shairi lote kama fumbo na kulidengua kwa kutumia baadhi ya

mihimili ya nadharia ya udenguzi pamoja na Uhistoria mpya. Tuliteua mashairi kadha katika diwani ya *Malenga wa Vumba* na *Malenga wa Mvita* na kuyachanganua kwa lengo la kufumbua ujumbe wa watunzi kwa wasomaji wake.

Njogu na Chimera (1999) wanaonyesha jinsi ya kuyachambua mashairi ya Kiswahili kwa kuzingatia vipengele vya maudhui, wahusika, fani, muundo, mtindo na muktadha. Kupitia vipengele hivi utafiti wetu ulifaidika kwa sababu utazingatia hatua za uchambuzi walizozitoa. Utafiti huu ulizingatia hatua hizo baada tu ya kubainisha kwamba shairi lote ni fumbo na kwamba liliweza kukatiza mawasiliano kati ya mtunzi na hadhira yake. Tulividengua vipengele vyote vya mashairi teule na kuunda upya ujumbe kulingana na muktadha wa wakati lilipotungwa na baadaye wakati uliopo.Nadharia ya Uhistoria Mpya utatusaidia katika uchanganuzi huu.

King`ei na Kemoli (2001) wanasema kwamba, ushairi ni chombo mwafaka kinachomwezesha mwandishi kuufumbata upana na urefu wa maisha katika maneno teule machache yaliyofinywa kisanaa. Kazi ya washairi hawa wawili ilitufaidisha kwa sababu wametuonyesha hatua za kuzingatia ili kudondoa maudhui ya mshairi (uk. 66). Utafiti huu ulichanganua baadhi ya mashairi ambayo ni mafumbo katika diwani ya *Malenga wa Vumba* na *Malenga wa Mvita* na kuyadengua kwa mujibu wa nadharia ya udenguzi pamoja na kuchambua maana ya mashairi hayo kupitia nadharia ile ya Uhistoria Mpya.

## 1.7 Misingi ya nadharia

Utafiti huu umetumia Nadharia Changamano: yaani nadharia ya Udenguzi pamoja na nadharia ya Uhistoria Mpya kama dira ya kuyafumbua mashairi ya watunzi wa *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*.

Nadharia ya udenguzi ni mwafaka na imetoa msingi maridhawa wa uchambuzi wa maana za mashairi. Hii ni kwa sababu imeuwezesha utafiti kupata fasiri mbalimbali za mashairi. Aidha, Udenguzi unadai kwamba hakuna maana moja maalumu na inayoweza kuitwa ya mwisho ya matini (utungo).

Kimsingi, nadharia ya Udenguzi ni mkabala wa kiuhakiki unaochunguza kutotegemewa kwa lugha kukifikia kitu kinachokuweko kando na lugha hiyo. Ni mkabala unaopinga mtazamo kwamba kazi ya kifasihi ina kitovu cha kimaana. Kwa mujibu wa Goring Paul na wengine (2001), nadharia ya Udenguzi iliasisiwa na mtaalam aliyeitwa Jacques Derrida aliyeishi miaka ya 1930. Baadaye ilishikiliwa na wachunguzi wa kifasihi wa Yale, Marekani.

Derrida alitumia dhana ya uhamisho ambayo inahusiana na maoni ya De- Saussure kuhusu kiashiria na kiashiriwa. Yaani hakuna uhusiano kati ya neno na kitajwa. Derrida anasema kwamba mfumo mzima wa lugha unatawaliwa na kanuni inayoitwa uhamisho.

Derrida alizua dhana za:

a) Kujengua - maana yake ni kubomoa muundo wa matini au kazi ya kifasihi.

b) Kujenga tena - kuchunguza vipengele vyote vya matini fulani na kuweka maana hiyo pamoja ili kuunda maana kamili ya matini au kazi ya fasihi.

Dhana hizi mbili zinamaanisha kuchanganua muundo wa kifasihi na wa matini ili kuunda maana upya na kuleta uelewekaji wa ndani wa matini hiyo.

Nadharia ya Udenguzi ina mihimili kadha ambayo ni pamoja na:

1) Udenguzi huzama katika kufafanua matini na kuitazama kwa jicho la ndani.

2) Nadharia hii inadai kwamba uelewaji wa marefu na mafupi ya matini unaweza kutupa mwanga kamili kuhusu jamii na kwamba si muhimu tuangalie muktadha wake.

3) Udenguzi ni unakidi wa lugha kama chombo cha mawasiliano, chenye utata na uwezo wa kujifafanua hasa katika maandishi.

4) Daima kuna mvutano wa kuwepo na kutokuwepo.

5) Kuna uwezekano wa maingiliano ya fasiri mbili za kazi moja ya kifasihi zisizolingana kamwe. Tafsiri zote mbili huenda zikakubalika.

6) Udenguzi huzingatia lugha na matini kwa kuipasua matini katika vipengele vyake vyote ili kuweka wazi maana fiche.

7) Udenguzi hudai kwamba ufasiri wa matini hauwezi kufika mwisho na kuwatosheleza wanajamii wote. Kila wakati matini isomwapo maana hupatikana. Maana hiyo haiwezi kuitwa ya mwisho.

Utafiti huu umehusisha baadhi tu ya mihimili ya udenguzi kuyadengua mashairi na kupata maana ya mtunzi. Kulingana na mhimili wa kwanza, udenguzi huzama katika ufafanuzi wa matini na kuitazama kwa jicho la ndani kwa kuyadengua na

kuyabomoa. Mashairi ni mafumbo na iwapo yatachanganuliwa kupitia vipengele vilivyoyajenga, maana itafafanuliwa na kuwekwa wazi kwa wasomaji.

Ufumbuaji wa mashairi unaungwa na mhimili wa tano unaosema kwamba kuna uwezekano wa maingiliano ya fasiri mbili za kazi moja ya kifasihi zisizolingana kamwe. Aidha, tafsiri zote mbili huenda zikakubalika na wasomaji au wafasiri. Lugha ya washairi ni changamano na inazua utata mwingi katika ufasiri wa maana. Huenda maana tofauti zikatolewa na wasomaji tofauti tofauti wa shairi moja.

Mhimili wa sita unaunga kupasuliwa kwa matini kwa vipande au vipengele tofauti tofauti na kuweka wazi kilichofichwa (maana). Mhimili huu ulizingatiwa katika kupasua mashairi kwa vipande vyake tofauti ambavyo ni pamoja na mada, beti, mishororo, kibwagizo pamoja na msamiati uliotumika.

Mhimili wa saba unaodai kwamba ufasiri wa matini hauwezi kufika mwisho na kuwatosheleza wanajamii wote umetusaidia katika utafiti huu. Kulingana na uchangamano na utata wa lugha ya kishairi maana tofauti zilipatikana.

Nadharia ya udenguzi ilikuwa na upungufu katika utafiti huu kwa sababu haikubali kurejelewa kwa muktadha au utamaduni ili kupata maana ya matini ya kifasihi. Iwapo itatumika peke yake huenda maana ya mashairi yanayorejelea utamaduni na mila isidhihirishwe. Ili kushadidia upungufu wa Nadharia ya Udenguzi tuliitumia pamoja na mihimili kadhaa ya Nadharia ya Uhistoria Mpya (Nadharia ya Utamaduni).

Nadharia ya Uhistoria mpya ni mwafaka zaidi kushadidia upungufu huo kwani itatoa msingi maridhawa wa uchambuzi wa matini kwa miktadha ya kihistoria. Hii

ni nadharia ya kisasa na kimaendeleo inayohusishwa na tapo la wasomi wenye mwelekeo wa kilimbwende na ufufuo wa elimu na maarifa katika kazi za sanaa (Murfin 1991, Rice 1993). Ni nadharia iliyoasisiwa na Michel Foulcout na Raymond Williams.

Waitifaki wa nadharia ya Uhistoria Mpya ni pamoja na Bakhtin, Althuser, Hayden White, Gadamer, Greenblatt na Marilyn Butler. Hii ni nadharia iliyoibuka kufuatia nadharia za kiufafanuzi na za kiuhakiki mpya katika miaka ya 1980. Imechangiwa na nadharia za hivi karibuni kama vile Uchanganuzi- Nafsia, Msomaji- Mwitiko, Uana na Upambanyaji (McGann, 1985).

Nadharia ya Uhistoria inadai kwamba ni muhimu uchunguzi ufanywe juu ya jamii halisi zinazozalisha fasihi katika mahala na wakati maalum (Butler, 1987).Inasema kwamba matakwa ya kijamii na kisiasa huathiri utoaji na upokezi wa kazi za fasihi (Greenblatt, 1980). Kila mtunzi huwa ameathiriwa na mazingira na athari hizi hazina budi kujitokeza katika utunzi wake.

Kila utungo wa kifasihi ni zao la jumuia fulani ambapo kiwango cha utamaduni wake, maendeleo ya fasihi yake kwa jumla miongoni mwa mambo mengine, yote huchangamana na kuupa utungo fulani maana yake maalum. Fasihi haiwezi kutengwa na historia inayohusika nayo kwani inarejelea,nayo inarejelewa na vitu kwenye mazingira.

Dhana ya utamaduni haina budi kuchunguzwa upya kwani ujumi, mielekeo, maongozi, usanii, urazini na thamani za jamii hubadilika na wakati kulingana na mabadiliko ya jamii.

Nadharia ya uhistoria mpya ilishadidia ile ya udenguzi katika kufumbua mashairi yaliyoteuliwa. Mhimili wa kuzingatia muktadha wa kihistoria wa chimbuko la kazi ya fasihi itatusaidia kuelewa historia ya jamii ya *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba* pamoja na historia ya waandishi.

Tulitumia mhimili wa kuchunguza dhamira ya mtunzi. Kwa kuzingatia mhimili huu tuliweza kujadili mabadiliko ya kihistoria tangu kuandikwa kwa diwani teule pamoja na ujumbe wa kisasa kwa wasomaji wa leo.

Katika utafiti wetu mhimili wa kuzingatia historia ya wakati wa upokeaji wa kazi ya fasihi ni muhimu. Mashairi ya diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba* zinapokelewa leo katika mazingira gani kiwakati na kimaendeleo.

Nadharia hii ya Uhistoria Mpya pamoja na ile ya Udenguzi zilichangiana na kutusaidia kufumbua mafumbo ya kishairi na kutupa ujumbe kamili wa waandishi.

Tunapofumbua mafumbo ya mashairi tunafaidika kwa kupata ujumbe uliolengwa na vile vile, tunaweza kutumia mawaidha ya watunzi hao hivi leo.

**1.8 Mbinu za utafiti**

**1.9 Muundo wa Utafiti**

Utafiti huu ni wa kimaelezo au wa kimasimulizi. Data ilitokana na uchanganuzi wa maana za mashairi teule. Lugha ya mashairi pamoja na ujumbe wa mashairi zilichanganuliwa na fasiri mbalimbali za maana za mashairi teule kuelezwa. Hii ni kwa sababu data iliyolengwa ilikuwa ni ile ya kuchanganua

maana ya shairi kwa jumla ili kubainisha kwamba shairi la kimafumbo linaweza kufumbuliwa na kutoa maana moja ya jumla. Aina ya data yetu ilihusu uchunguzi wa shairi zima kama fumbo kwa kuchunguza jinsi lugha ya kimafumbo inavyolijenga na hivyo, shairi hilo kufumba ujumbe au maana ya mwandishi. Mashairi yaliteuliwa kulingana na mada mbalimbali za mwandishi na kwa kuzingatia muda utafiti uliochukua. Mada hizo kuu ni pamoja na mbinu za lugha, unyumba na masaibu/majonzi na makiwa.

Utafiti huu pia ulidurusu habari zinazowahusu waandishi ili kuonyesha jinsi mazingira ya watunzi yalivyochangia matumizi ya lugha ya kimafumbo. Ujumbe unaowahusu wasanii ulishughulikiwa maktabani ili kuimarisha hoja za utafiti huu. Kwa hivyo, data iliyokusanywa ilihusu mwandishi, mazingira na utamaduni wa Waswahili wa Pwani, hali ya kisiasa na kijamii nchini wakati wa uandishi wa diwani zao, maudhui na tamathali za usemi kupitia kwa usomaji wa vitabu na majarida, pamoja na kufanya uchanganuzi.

## 1.10 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa kupitia usomaji wa kina maktabani ambao ni njia moja kuu ya utafiti. Utatifi ulifanyiwa katika maktaba mbalimbali katika taifa la Kenya. Katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Kenyatta tulipata vitabu na diwani za mashairi kama vile *Malenga wa Mvita, Malenga wa Vumba, Malenga wa Ziwa Kuu, Malenga wa Karne Moja* na *Malenga wa Mrima.* Vile vile, tulipata vitabu kadha vya nadharia pamoja na majarida.

Aidha, utafiti huu ulifanyiwa katika maktaba za kitaifa (Kenya National Library

Services). Katika maktaba hii tulipata data kutoka vitabu kama vile *Kamusi ya Fasihi na Nadharia, Kanzi ya Fasihi, Historical Critique in Contemporary Literary Criticism* na *Studying Literature: the Essential Companion,* miongoni mwa vingine.

**1.11 Sampuli na njia za kuteua sampuli**

Katika utafiti huu sampuli lengwa ilikuwa ni diwani mbili teule za watunzi wawili wa mashairi ya kimapokeo. Kwa hivyo, sampuli iliwahusisha watunzi na vitabu vyenyewe. Tuliwazingatia watunzi wa pwani mwa Kenya ambao ni Ahmadi Nassir Juma Bhalo na Boukheit Amana. Ahmadi Nassir, mtunzi wa *Malenga wa Mvita,* ametungia kazi zake katika mazingira ya Mvita au Mombasa ya sasa na kutumia lahaja ya Kimvita.

Boukheit kwa upande wake ametumia lahaja ya Kivumba kutunga diwani yake ya *Malenga wa Vumba.* Aidha, ameathirika na Viswahili kadha kama vile Kimvita, Kiamu na Kimrima. Hatua hii imetusaidia kuchunguza namna mazingira tofauti tofauti Uswahilini yalivyoathiri utunzi pamoja na kazi zao.

Mada za lugha, unyumba, na masaibu, majonzi na maliwazo, ambazo kulingana na utafiti huu zilifumba ujumbe zilizingatiwa.

Data nyingine tulizotumia zilitokana na kusoma vitabu vyovyote vinavyohusiana na nadharia ya Udenguzi, uhakiki wa kitamaduni (Uhistoria mpya), mazingira ya Waswahili wa pwani na hali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii wakati diwani za *Malenga wa Vumba* na *Malenga wa Mvita* zilipoandikwa.

## 1.12 Njia za kukusanya Data na vifaa vya utafiti

Kusoma na kuchanganua mashairi teule ndiyo njia kuu iliyotumiwa katika ukusanyaji wa data. Aidha, diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba* ziliteuliwa kupitia mbinu kusudio. Majarida, machapisho, vitabu vya nadharia na vitabu vingine vilivyohusu uchanganuzi wa mashairi pia vilitumika.

Lugha iliyotumiwa katika utunzi wa mashairi ndiyo iliyokuwa nyenzo kuu ya kutofautisha mashairi yaliyofumba ujumbe na yale yaliyo na ujumbe unaodhihirika moja kwa moja.

Utafiti wetu ulizingatia ubainishaji wa malengo ya utafiti huu kwamba mashairi kadha ni mafumbo.

Vile vile, tulibainisha vipengele vya lugha vilivyochangia katika ufumbaji wa ujumbe wa mshairi. Aidha, data iliyokusanywa ililenga kubainisha kwamba shairi linaweza kupewa fasiri mbalimbali za maana kutegemea hali tofauti tofauti za kuzieleza maana hizo.

## 1.13 Uchanganuzi wa Data

Hatua zifuatazo za uchanganuzi zilizingatiwa:

Katika hatua ya kwanza, historia ya waandishi wa *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba* ilichanganuliwa.

Katika hatua ya pili, mashairi mbalimbali yaliteuliwa kutoka diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba* miongoni mwa mengine yaliyohusiana na mada yetu. Katika kiwango hiki tulichunguza matumizi ya msamiati wa kikale, wa

kilahaja, wa kigeni pamoja na tamathali mbalimbali za usemi katika mashairi hayo na jinsi yalivyofumba ujumbe wa mshairi.

Hatua ya tatu ilihusisha kuainisha mashairi kulingana na mada za utafiti ambazo ni pamoja na Unyumba, Ufasaha wa lugha, Masaibu, Majonzi na maliwazo. Katika hatua hii, mashairi teule yalichanganuliwa au kufumbuliwa kwa kubainisha maana ya kila shairi.

Mwisho, tulionyesha mafanikio ya utafiti, matatizo tuliyokumbana nayo katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data, na baadaye tukatoa mapendekezo ya nyanja za kufanyia utafiti zaidi.

### 1.14 Uwasilishaji wa matokeo ya Utafiti

Matokeo ya uchanganuzi wa *Malenga wa Vumba* na *Malenga wa Mvita* yaliwasilishwa kwa kuzingatia kipengele cha maana kwa kupitia mbinu ya maelezo. Maana hiyo ni kama matumizi ya lugha kwa ufasaha, unyumba, masaibu yanayomkumba binadamu miongoni mwa mada nyingine.

Sura mbalimbali zimefuatana kama ifuatavyo:

Sura ya kwanza ndiyo utangulizi wa kazi hii; sura ya pili imejadili historia ya waandishi pamoja na mazingira yaliyoathiri utunzi wao; sura ya tatu ni maelezo kuhusu ushairi na ufumbaji; sura ya nne imejadili mada mbalimbali za mashairi ya kimafumbo; nayo sura ya tano imejadili muhtasari wa kazi na mapendekezo ya utafiti.

Hivyo, sura inayofuata imejadili historia ya waandishi: Ahmadi Nassir, mwandishi wa diwani ya *Malenga wa Mvita* na Boukheit Amana, mwandishi wa diwani ya *Malenga wa Vumba*.

Aidha, mazingira yaliyoathiri utunzi wa kazi hizi za kifasihi yamejadiliwa kwa kina kwa lengo la kubainisha sababu zilizopelekea ufumbaji wa mashairi yao.

# SURA YA PILI

## Historia ya waandishi wa *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*

### 2.0 Utangulizi

Sura ya kwanza imejadili utangulizi wa utafiti huu. Katika utangulizi, tumeonyesha maana ya ushairi kwa jumla tukizingatia maoni ya washairi mbalimbali. Swala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, upeo wa utafiti, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti yamedhihirishwa. Sura hii imejadili historia ya waandishi wa *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba* na jinsi mazingira yalivyoathiri utunzi wao.

Ni muhimu kuchunguza historia ya mtunzi wa kazi ya kifasihi. Hii ni kwa sababu fasihi huzaliwa katika mazingira maalumu ya kihistoria (Msokile, 1993:v). Uchunguzi wa historia ya mtunzi hudhihirisha kuwa fasihi huwa ni kielelezo cha hali halisi za kijamii na haiwezi kujitenga kamwe na maswala ya kijamii. Mtunzi anaishi katika jamii na anaathiriwa na maswala mbalimbali ya jamii anamoishi. Hivyo, kuna uhusiano mkubwa baina ya sanaa na matukio ya kijamii. Msanii aghalabu hutunga kutegemea hali halisi ipatikanayo katika jamii yake na hali hii huwa chimbuko la kazi yake (Masinde, 2003:49). Athari mbalimbali za kifani na maudhui zinatokana na mazingira ya mtunzi. Mazingira hayo yanaweza kujumuisha watu na mawazo yao, vitu na hali ya maisha kwa jumla.

### 2.1 Historia ya mwandishi wa *Malenga wa Mvita*

Sehemu hii inatoa maelezo kuhusu mshairi Ahmadi Nassir Juma Bhalo (au Ahmadi wa Nassir) pamoja na mazingira yaliyomzunguka ili kuonyesha kwamba mhakiki hana budi kuzingatia muktadha wa kihistoria wa kazi anayoishughulikia.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Maelezo haya yataafiki mhimili wa Uhistoria mpya kwamba fasihi haiwezi kutengwa na historia inayohusika nayo kwani inarejelea, nayo inarejerewa na vitu kwenye mazingira. Ni dhahiri kwamba maisha ya mtunzi na imani yake vina uhusiano mkubwa na kazi yake (Wellek na Warren, 1949:75).

Ubainishaji wa matukio hutegemea jinsi mwandishi anavyouchora uhalisi wa maisha kwa kuathiriwa na falsafa yake. Mashairi ya Ahmadi Nassir yanaonyesha kwamba ni zao la amali za mazingira ya wakati maalum kihistoria. Kazi yake ni kielelezo cha ushahidi wa matukio na mwenendo wa jamii yake kiuchumi, kidini, kiutamaduni, kisiasa na kiitikadi. Ni kielelezo cha jinsi fasihi na sekta hizo zinavyowiana na muktadha wa historia nzima ya jamii ya wakati wake.

Mtunzi wa *Malenga wa Mvita* ni Ahmadi Nassir Juma Bhalo au Ahmadi wa Nassir kama ajulikanavyo na Wamvita. Alizaliwa mwaka wa 1936 katika mtaa wa Kuze huko Mvita (Mombasa). Alizaliwa katika kitovu cha Uswahili huko kuze na mitaa jirani kama vile Mji wa Kale, Birikau, Mkanyageni miongoni mwa mitaa mingine. Kulingana na Chiraghdin (1971), Ahmadi alizaliwa katika mitaa ya ulumbi na ufasaha wa Kiswahili. Katika mitaa hii kumewahi kutokea washairi wengi, waimbaji, wasomaji, waalimu, wapiga ala za muziki wa kienyeji na kigeni.

Ahmadi Nassir ni kaka yake Abdillatif Abdalla, mwandishi mashuhuri wa mashairi aliyewahi kutunga diwani maarufu iitwayo *Sauti ya Dhiki*. Ahmadi Nassir ameelea zaidi kwenye kuwapa wasomaji mafunzo ya maisha yao ya kijamii huku akiepuka siasa. Hata hivyo, ametaja siasa kwa mbali katika baadhi ya mashairi yake. Kwa mfano, katika shairi la 'Moyo' katika ukurasa wa 109 anadhihirika kuwa mwoga kisiasa. Anachelea kusema neno la kisiasa kinyume na hali pamoja na utunzi wa ndugu yake Abdillatif ambaye ana msimamo dhabiti wa kisiasa. Kwa upande



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

wake Ahmadi Nassir anadai kwamba ni subira tu itakayompa mja faraja maishani.

Ahmadi amekulia katika mazingira ya usanii wa lugha na fani zake. Haya yote pamoja na kipawa chake mwenyewe alichotunukiwa, yamempa ubingwa mkubwa wa kuweza kuisanifu lugha jinsi atakavyo.

## 2.2 Taathira katika utunzi wa Ahmadi Nassir

Sehemu hii imebainisha kwamba historia na mazingira yanayomhusu Ahmadi Nassir yamesaidia kuelewa muktadha na kuchangia pakubwa ufahamu kuhusu utunzi wake. Washairi wengi tangu zamani, hawakuweza kujiepusha na athari za utunzi wa watangulizi wao. Desturi hii yapatikana karibu kwa kila mshairi (Abdalla, 1972: 11).

Kimvita, lahaja aliyoitungia Ahmadi Nassir ina tarehe ndefu ya utungaji na watungaji wa mashairi na nyimbo. Tokea mashairi ya asili ya vugo, gungu na diriji mpaka tungo za malenga mashuhuri waliotangulia kama vile Muyaka, Mwalimu Sikujua, Sheikh Sudi, Bwana Ayubu, Mtwana wa Sumba na wengineo.

Mshairi wa Mvita wa sasa akitunga atakuwa akifuata njia ambazo zimepitwa na mlolongo wa washairi waliotangulia. Ni juu yake mwenyewe, mshairi wa kisasa akitaka kunufaika na mdororo huu wa malenga halisi. Tungo za Ahmadi Nassir zimechukua faida nyingi kwa malenga wenziwe waliomtangulia na ndipo mashairi yake mengi yakawa yamefanana na tungo nyingi za kishairi za waliomtangulia (Chiraghdin, 1971).

Hivyo, mashairi ya Ahmadi Nassir yamefanana na ya malenga wengine wa Mvita waliomtangulia.

Mifano ifuatayo imebainisha ukweli huo:

Gongwa ni mwina wa kina, azamaye yuzamile
Si mwenye kuzuka tena, yuzamapo yupotele
Huwa akikosekana, hutwawa ni maji male
Mjenga nyumba halele, yulele ukumbizani.
(Muyaka)
(Chiraghdin,1971:4)

Nilikuwa ng'ombe tangu, halitangulia zizi
Hawaturuku wanangu, nili hamu na simanzi
Punde haona wenzangu,wajile na paa wazi
Wametiwa mandakozi, na kutupiwa chumbani
(Sheikh Sudi)
(Chiraghdin, 1971:4)

Kumbuka, utayaona, mangapi yapisiyeo
Ya watu wenye maana, ni kipi kikomo chao
Haile ngoma ya wana, sijaona ikeshao
Kuno kuzima kweleo, haiwi kwisha uhunz
(al-Mambasi)
Chiraghdin, 1971:4)

Siwahi kupumzika, bwana hataakhari
Mwana amekasiriwa, pokeya ndiyo khabari
Wakati nilipofika, kunandiya nadhari
Mara alitaghayari, kibibi zabarajadi
(Ayubu)
(Chiraghdin, 1971:5)

Usijitie huzuni, nakwambiya shika langu
Kwa vishindo duniyani, ni ada ya walimwengu
Ni mbio za sakafuni, zisikutiye tewengu
Kitukuzwacho na Mngu, hapana wa kukitweza
(Ahmadi wa Nasiri)
(Chiraghdin, 1971:5)

Ukitazama mashairi ya Bwana Muyaka (1776 – 1840 B.K) utaona pasi na shaka iwayo kuwa yeye alikuwa amefika kiwango cha juu katika mlolongo wa Wangoi, naye pia kama Nassir, amenufaika na watangulizi wake.

Muyaka bin Haji, mtunzi wa mashairi ya Kiswahili ambaye huchukuliwa kuwa baba wa ushairi wa tarbia ulio mwingi sasa, alizaliwa mnamo mwaka wa 1776 na

kuishi hadi mwaka wa 1840. Mifumo ya historia ya Mombasa ambako Muyaka aliandikia mashairi yake ilikuwa imejaa misukosuko mingi ya vita kati ya watawala wa Mvita (Mombasa) na wale wa Pate. Aliandika mashairi ya masomo mbalimbali yalihohusu utamaduni wa nchi ya Waswahili pamoja na mapokezi yao ya kiuchumi. Hali hii iliyafanya mashairi yake kuwa stashahada ya historia ya Mombasa ya kati ya miaka ya 1810 na 1840. Wakati huu ndio mashairi yake mengi huangukia.

Aidha, mashairi ya Muyaka yana historia ndefu katika fasihi ya Kiswahili na Waswahili. Aliweza kutufunulia mengi juu ya watu wa Mombasa, pamoja na vile walivyoshirikiana na majirani zao.

Muyaka ndiye aliyetoa mchango mkubwa wakati wa tawala za Kiarabu na Mazrui huku akibadili ushairi wake kwa kukwepa maudhui ya kidini na kuanza kujishughulisha sana na maswala ya kijamii, na kuukashifu ukoloni (Ombuge na Adaka, 1999). Mfano wa shairi la nyakati za kikoloni ni 'Ngome' lililosema:

> Ngome ni ngome ya mawe, na fusi la kufusiza
> Ngome ni matumbawe, na boriti kuikiza
> Ngome wetwapo sikawe, enda hima nakufuza
> Ngome imetuumiza, nasi tu mumo ngomeni
>
> (Uk. 6)

Hapa Muyaka anadhihirisha uzalendo wake kwa kuchochea mapinduzi ya utawala wa Kireno uliokuwa unawanyanyasa. Aidha, alilaani kuwepo kwa matabaka na vibaraka wa wakoloni katika jamii ya Waswahili akisema, "Viwi mwaviramba vyema mngevilaje".

Muyaka aliandika mashairi yenye mawazo bora, ukumbusho wa ushahidi wa yaliyopita, yanayozunguka kwa nyakati zote na kuwapa watu faida kwa nyakati zao.

'Kati ya walioangukiwa na kura ya kipawa cha utunzi, Muyaka ndiye aliyezidi. Na kumweleza ni ngumu sana, kwa yaliyoandikwa humo', (Chiraghdin, 1971).

Mashairi ya Muyaka yalikuwa na ujumbe mzito wa kisiasa lakini habari yenyewe ilikuwa imefichwa ya kuwazindua wenyeji na kuwafumba wakoloni. Kuna kueleana kukubwa kati ya Ahmadi wa Nassir na Muyaka bin Haji, sio kwa sababu tu ya lahaja wanayotumia katika mashairi yao, bali pia kwa mtindo na maudhui makuu yanayojitokeza katika mashairi yao.

Tunadhani mifano tuliyotoa hapo juu ya kuonyesha kufanana kwa Ahmadi na watangulizi wake kama vile Muyaka, Sheikh Sudi, al-Mambassi na Ayubu utatosheleza kwa sababu hatuwezi kulinganisha kazi zao zote katika uchanganuzi huu.

Mwandishi huongozwa na itikadi katika uelezaji wa matukio ya jamii anayoishughulikia, na itikadi hiyo hujibainisha kwa namna anavyotoa maelezo yake au kuwasawiri wahusika wake. Itikadi yenyewe hujitokeza katika maudhui na dhamira ya mwandishi (Njogu na Chimera, 1999: 28). Sehemu ifuatayo imejadili falsafa ya Ahmadi Nassir.

## 2.3 Falsafa ya Ahmadi Nassir.

Falsafa ya mwandishi ni namna msanii anavyoliangazia jambo kisanaa kuhusiana na maisha. Ni mtazamo madhubuti kuhusu suala au kipengele chochote. Pia, ni busara iliyofikiwa baada ya mtu kutafakari kwa kina kuhusu jambo la kilimwengu. Kwa hivyo, falsafa ni fikira kuu za mtunzi au mwandishi wa kisanaa. Fikira hizo hutokana na imani na misimamo ya mwandishi anayehusika na huathiriwa kwa kiasi kikubwa na jinsi anavyoyatazama mazingira yake.

Mashairi ya Ahmadi yamesheheni fikira nzito, mafunzo, maonyo, matatizo ya kilimwengu na mambo mengine yanayomhusu mja au binadamu katika maisha yake. Katika mashairi ya maliwazo, Ahmadi Nassir anailiwaza roho na kuonyesha maonevu na madhila yamfikayo mtu na mavumilivu ambayo mja afaa kuwa nayo kwa kuwa hiyo ndiyo hali ya dunia.

Nassir ametumia misemo ya busara ya Kiswahili kama vile 'mnyonge kupata haki ni mwenye nguvu kupenda'; 'subira huvuta kheri' na 'mbio za sakafuni huishia ukingoni' na kadhalika kuwapa wasomaji wake maarifa ya maisha ya ulimwengu. Aidha, mashairi ya Nassir yamefungamana na uhusiano wa mwanamume na mwanamke katika maisha ya kimapenzi ndoa. Kwa mfano, shairi la 'Owa' (uk. 158) limefanana na shairi la jina lilo hilo la Muyaka. Muyaka alimhimiza rafiki yake, ambaye alitaka kuoa, aoe na ajaliwe mke wa imani, baraka, utulivu, uzima na kadhalika.

Beti za malenga hawa wawili zinaweza kulinganishwa ifuatavyo:

Owa ndiwe muolezi, uzoeleo kuowa
Owa sifumbe maozi, maninga uchiyavuwa
Owa uzaze uzazi, kama ulivyo zaliwa
Owa sizi ndizi ndowa, aso kuowa ni yupi

(Abdulaziz, M.H.*Muyaka*,1979:182)

Owa sandame hadaa, moyo ukahadaiwa
Owa anaye kufaa, mke mwenye kusifiwa
Owa upate kuzaa, kama ulivyozaliwa
Owa ukijaaliwa, mupendane na mkeyo
(*Malenga wa Mvita*, 1971:158)

Ahmadi Nassir anasawiri mwisho wa maisha ya mwanadamu kwa lugha inayostahiki kina cha majonzi na msiba, na kwa namna itiavyo ukiwa. Lugha yenyewe aliyoitumia ina utukufu ulinganao na lugha nyingine yoyote. Shairi lake

la 'Kullu Nafsiri Dhaaiqatul mawt' (Uk. 167) ni aya ya *Kurani Tukufu* (Sura 21:34), inayoeleza kuwa kila roho itaonja mauti. Alikuwa anajiliwaza wakati wa kufikwa na msiba wa kuondokewa na babake, marehemu Nassir wa Jumaa.

## 2.4 Historia ya Mwandishi wa *Malenga Wa Vumba*

Uchanganuzi huu umezingatia historia ya maisha ya mwandishi wa *Malenga wa Vumba* ili kuelewa zaidi msukumo na ilhamu ya uandishi wake. Hii ni kwa sababu sanaa ni mojawapo ya mbinu zinazotumiwa na mwanadamu ili kudhibitisha uhalisi (Sanchez, 1973: 37). Aidha, uhusiano kati ya sanaa na jamii ni wa kihistoria ambapo msanii huwa ni wa wakati wake.

Nadharia ya Uhistoria mpya inadai kwamba mwandishi huwa na historia yenye matukio muhimu yanayomwathiri kwa njia na namna fulani (Davis na Schleifer, 1986: 43; Butler, 1987).

Aidha, Uhistoria mpya unadai kwamba fasihi inarejelea, nayo inarejelewa na vitu au watu kando yake kwenye mazingira. Hivyo, madhumuni ya sehemu hii ni kubainisha kwamba maelezo kuhusu historia ya Boukheit Amana na mazingira yake husaidia kuelelewa muktadha, jambo ambalo linachangia ufahamu wetu kuhusu utunzi wake.

Kazi hii imebainisha kuwa mtunzi huishi katika jamii na huathiriwa na mambo mengi kulingana na wakati. Waandishi wa mashairi kama wanajamii, huwa wanaguswa na matukio ya kijamii (Nyembembe 1997: 18). Hivyo, wanalazimika kutunga mashairi yao kadiri wanavyoiona na kuifahamu jamii. Hususa, wanazitoa hisia zao nje katika sura ya ushairi (Masinde, 2003: 74). Mwandishi husimulia tajriba mbalimbali ambazo zimemkumba au zimeikusa jamii yake (Njogu na

Chimera, 1999: 48). Masimulizi ya mwandishi aghalabu hutokana na upekuzi na uteuzi wa hali mbalimbali zinazoigusa hisia zake. Kisha, upekuzi na uteuzi wa hali zinazosimuliwa mara nyingi utakuwa umefungamana na falsafa yake kuhusu yale anayoyaona.

Sura hii imedhibitishwa kwamba kuna uhusiano mkubwa kati ya maudhui na hali halisi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii katika kipindi maalum cha historia ya jamii. Pia, inatoa maelezo kuhusu mshairi Boukheit Amana na mazingira yaliyomzunguka wakati akitunga kazi yake ya *Malenga wa Vumba*. Lengo ni kudhihirisha kuwa maisha, mazingira pamoja na imani ya mtunzi vina uhusiano mkubwa na utunzi wake.

Aidha, utafiti umegusia historia ya mfumo wa kisiasa na kijamii wakati wa utunzi wa *Malenga wa Vumba*. Madhumuni ya sehemu hii ni kuonyesha kwamba mkondo wa fasihi ya Kiswahili,hususa, ushairi wakati wa utunzi wa Boukheit uliadhiriwa na uhalisi wa kimazingira na unaweza kueleweka katika muktadha huo.

Falsafa ya mwandishi huyu imejadiliwa ili kuona iwapo utunzi wa mshairi huyu umebainisha uhalisi uliokuwapo. Msingi huu ni muhimu katika kuelewa msukumo uliompa Boukheit ilhamu ya kuandika. Falsafa hutokana na maamuzi ya mtu fulani kuhusu hali ya dunia, mazingira yanayomzunguka na miungu ama nguvu zinazoutawala ulimwengu na juu ya maisha kwa jumla.

## 2.5 Maisha ya awali ya Boukheit Amana

Kutokana na matukio mbalimbali katika maisha ya msanii, huweza akaelekezwa kutunga kwa njia fulani (Davis na Schleifer, 1986: 433). Hivyo, utafiti huu umegusia kwa kiasi maisha ya Boukheit Amana.

Boukheit Amana alizaliwa Kusini mwa Pwani ya Kenya huko Uswahilini eneo lijulikanalo kama Vumba. Lugha au Lahaja itumikayo huko ni Kivumba. Kulingana na Msami (1982), Boukheit alibahatika kupata taaluma ya Viswahili mbalimbali. Hii ni kwa sababu wavyele wake wa upande wa kuumeni asili yao ni Waswahili wa kutoka Kaskazini mwa pwani ya Kenya, yaani wenyeji wa asili ya Kisiwa cha Siu. Kisiwa cha Siu ni maarufu sana kwa lugha ya Kisiu na ushairi wa Kiswahili. Kutokana na ulimi wa wazazi wake wa kuumeni aliweza kujipatia maarifa ya kutosha katika lugha ya Kisiu na ushairi wake.

Aidha, wazazi wa kukeni wa Boukheit ni Waswahili wenye asili ya wenyeji wa Kusini mwa Pwani ya Kenya, yaani Vumba. Tena, Boukheit aliweza kuupata uzuri na utamu wa ulimi wa Kivumba, lugha ambayo kwake ni ulimi wa mama, na kama marehemu Shaaban Robert katika takhmisa yake alivyosema:

Titi la mama litamu, hata likiwa la mbwa.
Kiswahili naazimu, sifazo inavyofumbwa
Kwa wasiokifahamu, niimbe ilivyo kubwa
Toka kama chemchemu, furika palipozibwa
Titi la mama litamu, jingine halishi hamu
(Robert, S.,*Pambo la Lugha,*1974:27)

Wavumba ni washairi wa kale na asili ya lugha yao ya kivumba hupendeza mno ikitumika katika mashairi ya Kiswahili. Ni lugha ambayo humsaidia sana mshairi kwa kufupiza mizani au kurefusha. Kuna mashairi machache ya mtunzi mmoja wa kale wa Kivumba yanayodhihirisha ubingwa huo wa Wavumba:

Rara lirarile rara, rara lirarile gunge
Uje wembe wakuvara, na noo lamviringe
Rarizo rukalivara, hata marara yatenge
Nyumba inangia tenge, mwanenaje mawaria?

Nyumba k'aiezekeki, nyumba madongedonge
Nyumba k'aigandikiki, nyumba misongesonge
Nyumba hii ivunjiki, simameni ruijenge
Nyunba inangia tenge, mwanenaje mawaria?

Nyumba hino na pandaze, zosi hizi ruzifunge
Chana sana ruzikaze, hata nyumba migange
Mbugu ruzi'utanize, yosi ruizongezonge
Nyumba inangia tenge, mwanenaje mawaria?
(Msami, 1982:3)

Maelezo yetu yameonyesha jinsi Boukheit Amana alivyoweza kujipatia taaluma ya Viswahili vya Kisiu na Kivumba kutokana na uhusiano wake wa kuzaliwa. Isitoshe hayo, vile vile yeye mwenyewe ana ujuzi mwingi sana wa lugha ya Kimvita kwani katika baadhi ya umri wake mwingi aliwahi kulelewa katika mji wa Mvita (Mombasa).

Bahati yake ya kupata wasaa wa kuendelea kujifunza vilugha vya Kiswahili haukukomea Mvita. Wavyele wake wote walipohama na kwenda kuishi Mrima (Dar es Salaam), Tanzania, Boukheit alipata nafasi ya kujifunza taaluma ya lugha ya Kiswahili cha Mrima.

Boukheit alichagua kutungia mashairi yake bila kuonekana hadharani, hadi akafikia hatua ya kuiandika diwani ya *Malenga wa Vumba*. Kwa kawaida lakabu za kishairi huchaguliwa na washairi wenyewe; au washairi hupewa lakabu na watu wengine baada ya kujulikana kuwa mshairi huyo hana shaka, amejikinai na atosha kabisa kuwa mshairi chipukizi, hodari na wa kuzingatiwa. Boukheit

aliamua kujichagulia lakabu katika uwanda wa ushairi na kujitambulisha kama Mti Mle. Katika shairi lake la 'Mti-mle' anasema:

Zitavuma
1. Zitakoma
Nitakwima
Mti-mle.
(*Malenga wa Vumba*, 1982:19)

Maana hasa ya 'mti-mle' aliyoichagua Boukheit Amana ni mti-mrefu. Maneno mti-mrefu yametumiwa kama isitiara ya kuwabainishia washairi wenziwe kuwa hakuna mshairi awezaye kukifikia kilele cha uhodari wa ushairi wake.

Mnamo mwaka wa 1981, jumuiya ya kukuza Kiswahili nchini Kenya, yaani 'Kenya Kiswahili Association' pamoja na wizara ya Utamaduni na Ustawi wa Jamii walitoa shindano la utunzi wa mashairi bora juu ya utamaduni wetu. Boukheit ndiye aliyenyakua zawadi ya kwanza. Hivyo, alilisambaza jina lake miongoni mwa waandishi maarufu chipukizi na kuupasua ukimya uliokuwa umemzingira. Hii ni dalili tosha isiyoweza kupingika inayoonyesha kuwa mti-mle ni bingwa na anayeelewa fani na mbinu mbali mbali za utunzi wa mashairi bora na fasaha. Diwani yake ya *Malenga wa Vumba* ilimchukua miaka isiyopungua minne kuitunga.

Umuhimu wa historia hii fupi kumhusu Boukheit Amana ni kuonyesha kwamba, maisha ya maeneo mbali mbali ya Pwani ya Kenya na Tanzania pamoja na mazingira mbali mbali aliyokumbana nayo yalimpa tajriba iliyomwathiri namna alivyouona ulimwengu na kufasiri maswala yake. Hivyo ndivyo alivyousawiri ushairi na kutoa falsafa yake.

## 2.6 Falsafa ya Boukheit Amana

Baadhi ya dhamira katika utunzi wa mwandishi huyu ni za kuadilisha mioyo ya wasomaji. Amewapa wasomaji wake falsafa kuhusu umaskini na kwamba mtu aridhike na kile akipatacho. Vile vile amegusia maswala ya unyumba, wasifu, nasiha, masaibu pamoja na maliwazo.

Katika shairi la 'Alfaqru fakhri' amewapa wasomaji wake mafunzo ya jinsi vile inavyostahili mtu mwema mwenye murua kuishi kwa njia bora katika ulimwengu huu wenye matatizo.

Katika ubeti mmoja wa shairi hilo anasema:

8. Watu wameghafilika, kwa kuabudu dinari
Imani zimewatoka, wendapo huwaza shari
Hawajui kuridhika, tamthili ya kafiri
Alfaqru fakhri, nipatacho hutosheka.
(*Malenga wa Vumba*, uk. 20).

Boukheit ni mwalimu hodari wa kuwafunza watu utu, busara na tabia njema. Katika shairi la 'Ufunguo wa maisha' tunaweza kuuona uwazi na ubingwa na umbuji alio nao mshairi huyo aliyevishwa taji la heshima ya *Malenga wa Vumba*. Ubeti wa kwanza wa shairi hili unatudhihirishia ukweli huo:

Mwanangu njoo karibu, nikupe ya manufaa
Uyajue ya wajibu, uepukwe na balaa
Usije kapata tabu, dunia ina hadaa
Katika ya manufaa, mojawapo ni elimu.
(*Malenga wa Vumba*, uk. 41)

Katika shairi hili, malenga Boukheit Amana amejaribu kutumia mbinu za kutoa funzo la kuwakumbusha wazee jinsi ilivyo wajibu wao kutoa mafunzo na nasaha bora kwa watoto wao. Aidha, katika shairi lilo hilo, anawapatia vijana funzo lao pindi nao wajaliwapo kupata watoto wasisahau kuwapatia wana wao mambo

mawili yaliyo muhimu katika maisha yao, yaani elimu na mafunzo ya adabu njema.

Mtu asiyewapa wanawe elimu atakuwa amewaua kifo cha uhai. Anatahadharisha pia kuhusiana na mema na mabaya ya tamaduni za kigeni.

Kupitia shairi la 'Tamadunizo siase', anasema:

Twalonena si kidogo, mengi tumezungumza
17. Tuipunguze miigo, kuiga yasopendeza
Asili kuipa sogo, utumwa twajifungiza
Twige ya kutuongoza, kwenye tamaduni zenu
(*Malenga wa Vumba*,Uk. 51)

Kwa kawaida, kila taifa na kila kabila huwa lina aina ya makosa yake na ila yake katika utamaduni wake. Hivyo, Mti-Mle katika shairi lake hili, anataka wasomaji wa diwani yake wawe mahiri muda wanapotaka kuiga utamaduni wa kabila fulani au taifa fulani, kwanza wanayachunguza kwa makini, hayo watakayoyaiga yanaweza kukuza utamaduni wao au la. Ikiwa mambo yatakayoigwa ni yale ya kuharibu mila na desturi zetu, Ustadh Bhalo anasema katika kibwagizo cha ubeti huo kwamba tuachane nayo na tufuate tu yale yatakayosaidia katika kutuongoza ili tuwe na utamaduni bora.

Boukheit vile vile, amegusia swala la haki za wanawake. Tafsiri za mwanamke zimeathiriwa na mila, utamaduni na mazingira. Hivyo, ubinadamu wake umekuzwa na kuzushwa (Masinde, 2003:139). Miongoni mwa majukumu ya fasihi, ukiwemo ushairi, ni kuikosoa jamii kutokana na mawazo batili ambayo yanaweza kuipofusha na kuikwamisha. Hii ndiyo sababu Boukheit Amana anajitokeza na kupigania hadhi ya mwanamke katika jamii.

Kwa kweli mshairi ni kama kinyonga, mara anageuka rangi hii mara nageuka rangi ile (Msami, 1982:7). Hivyo, Boukheit katika shairi lake 'Uhaba wa kazi' (uk. 42) amejifanya msemaji wa wanawake. Amelitunga shairi lake hilo katika umbo la kuonyesha kama kwamba shairi hilo limetungwa na mwanamke. Madhumuni ya shairi hili haswa ni kuwapa kina mama pamoja na wasomaji wake wengine changamoto waone picha ya jinsi ulimwengu huu wa sasa ulivyokuwa na kuendelea hata imekuwa mwanamke na mwanamume wamekuwa hali moja kazini. Katika shairi lake anasema:

Mbona watuingilia, kaka ubaguzi
2. Likukeralo twambia, tulijue wazi wazi
Au unalochukia, ni wake kufanya kazi
Maisha ya kisiku hizi, watu ni bega kwa bega.
(*Malenga wa Vumba*,Uk.42)

Mwandishi anapinga kinaganaga mawazo batili ya kumdunisha mwanamke. Anapiga vita taasubi ya kiume na ubaguzi na uonevu wa wanawake. Ujumbe mahususi wa shairi hili ni kwamba kuna haja ya kuwa na fikira mpya na mkabala tofauti kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii.

Mwandishi huyu anapinga dhuluma na unyanyasaji dhidi ya wafanyikazi. Amefumbua fumbo la wengi wanaowatesa wafanyikazi wao kwa kusema:

Muda kirudi sokoni, mama hana wasiwasi
6. Ni mijiguo ndooni, nii fuwe kwa nafasi
Pasi na kutakamani, jioni nipige pasi
Heka ni kazi kisasi, nisorudi nitokako
( *Malenga wa Vumba*,'Narudi nitokako', uk. 44)

Amegusia maswala ya kisiasa kwa kutetea misimamo ya serikali pamoja na viongozi wakuu serikalini. Itakumbukwa kwamba kazi yake ilichapishwa mwaka wa 1982. Hizi zilikuwa nyakati za giza la kisiasa nchini Kenya. Nyakati hizo, hata kuonekana kupinga serikali ya Moi au hata mtangulizi wake Hayati Mzee Jomo

Kenyatta ilikuwa ni hatia na usaliti. Akihimiza uungwaji mkono wa serikali, Boukheit anasema:

Kalili huwa imara, iwapo na kiongozi
2. Kiongozi wa busara, asiye na ubaguzi
Ubaguzi ni hasara, isofaa siku hizi
Siku hizi za fikira, za watu wanomaizi
Kumaizi yalo bora, yasiyo na pingamizi
(*Malenga wa Vumba*,'Heshima kwa serikali', uk. 85)

Ametunga shairi la kumsifu Mzee Jomo Kenyatta, Rais mwanzilishi wa taifa la Kenya katika shairi la 'W-A-S-I-F-U W-A B-A-B-A K-E-Y-A-T-T-A' akisema:

Ameivunja miamba, nyayoze twakanyagia
17. Na nchi akaipamba, baraka kututilia
Akaifunga kamba, Harambee kuivutia
Ndipo twaomba muumba, Kenyatta mshufaia
( *Malenga wa Vumba*, Uk.66)

Mashairi ya Boukheit yamedhihirisha kwamba kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya matukio ya kihistoria na kijamii na maswala aliyoshughulikia. Katika uchanganuzi huu mashairi ya Boukheit yamedhihirisha maendeleo ya kijamii kulingana na wakati.

Maswala yaliyoshughulikiwa yamepanuka na kufungamana na jamii ya kisasa. Kazi yake imeafiki kipengee cha nadharia mojawapo iliyoongoza utafiti huu ya Uhistoria mpya kwamba, kila mtunzi huwa ameathiriwa na mazingira, na athari hizi hazina budi kujitokeza katika utunzi.

## 2.7 Eneo la Kijiografia na utunzi wa *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*

Kushughulikiwa kwa eneo la kijiografia na utafiti huu ni muhimu katika kuchanganua mambo yaliyochangia ufumbaji wa mashairi katika diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba.*

Waswahili wanaishi katika eneo la pwani ambalo ni takribani kilomita 1000 tokea Somalia hadi Msumbiji katika sehemu ya kusini (Chiraghdin na Mnyampala 1977).

Eneo la kijiografia wanamoishi Waswahili limepelekea kundi hili lifanyiwe utafiti mwingi na Wanaathropolojia, Wanahistroria pamoja na Wanaisimu (Chacha 1994: 92; Nyanchama 2004:53). Waswahili wanaishi karibu na Bahari Hindi jambo ambalo limewawezesha kuingiliana mno na wageni waliotembelea Afrika Mashariki kuanzia karne ya pili kupitia kwa usafiri wa majini huku wakitumia pepo za misimu na mikondo ya bahari (Chiragdin na Mnyampala 1977; Nyanchama 2004: 53)

Mtunzi wa fasihi, sawa na fasihi yenyewe, ni zao la mazingira maalumu ya historia ya jamii. Fasihi haikui katika ombwe tupu, bali hupewa msukumo, umbo, mwelekeo na hata eneo la kushughulikiwa na nguvu za kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa mujibu wa jamii husika (Odaga, 1985).

Ahmadi Nassir ameyasawiri mazingira ya pwani katika diwani ya *Malenga wa Mvita.* Kwa mfano ametunga shairi liitwalo 'Maji' (uk. 140) huku akilimithilisha na mawazo ya waja. Katika shairi hili Nassir aliwashauri waja wawaze yaliyo ya thamani kwao na yaliyo makuu kama maji makuu (bahari).

Kwa sababu ya kuwepo karibu na pwani ambapo kilimo cha minazi ni muhimu sana, Nassir ametunga shairi la kusifu minazi. Katika shairi lake la 'mnazi' anaanza na kutamatisha akisema:

Pani kiti nileketi, niwasifiye mnazi
1. Faida ni makuti, huvimbiya paa wazi
Kigogoche hukiketi, na wenzawa habarizi
Sitouwata mnazi, mti wa faida nami

Kaditamati shairi, la zaidi siongozi
21. Jina langu mashuhuri, pulikani wasikizi
Ni Ahmadi Nasiri, niloutunga mnazi
Sitouwata mnazi, mti wa faida nyingi.
(*Malenga wa Mvita*, Uk.95)

Mshairi huyu anausifu na kutangaza kwamba mnazi una faida nyingi kwake na kwa Waswahili kwa jumla. Ingawa ametaja maeneo na mazingira tofauti tofauti katika shairi lake la 'Kisichoumbwa na M'ngu' kwa kiasi kikubwa amerejelea maeneo na miji mbalimbali ya pwani. Ametaja maeneo ya kijiografia ya pwani pamoja na utunzi wao anaposema:

Na malenga mulo Amu, Pate na kizingitini
20. Ndinyi malenga alimu, tangu kale na zamani
Nijibuni nifahamu, kisichoumbwa ni nini?
Kitu gani duniyani, kisichoumbwa na M'ngu?
(*Malenga wa Mvita*, Uk.59)

Kwa sababu ya kuwepo karibu na bahari, uvuvi wa samaki baharini ni mojawapo ya shughuli zinazofanyika pwani. Katika *Malenga wa Mvita,* mshairi anabainisha kuwepo kwa uvuvi anapotunga shairi liitwalo 'Mvuvi':

Sivuwi bahari ndogo, hatia nanga fuoni
2. Havisimbika vigogo, vilivyozama majini
Na wala sivuwi ngogo, vidagaa na mbirini
Siwavui asilani
(*Malenga wa Mvita*,Uk.34)

Katika ubeti huu na shairi lote kwa jumla, Boukheit ameonyesha kufahamu aina mbalimbali za samaki na maeneo ya uvuvi mambo ambayo ni mzawa wa pwani pekee anaweza kuelewa na hivyo kupata maana.

Boukheit kwa upande wake ametunga mashairi yaliyoathiriwa na lahaja nyingi kwani yeye ni Mswahili wa Uswahilini (Msami, 1982:2). Lahaja alizotumia ni pamoja na Kisiu, Kimvita, Kivumba na Kimrima. Kadhalika, Boukheit ametunga shairi la kusifu minazi. Katika shairi lake 'Mazaoye ya shinani' anasema:

Mnazi toka dahari, fakhari yao warembo
2. Kumeakwe si papari, uonapo lake umbo
Wamea kisirisiri, na tilatila majambo
Mnazi mezuwa, mazaoye ya shinani
(*Malenga wa Vumba*,Uk.29)

Katika diwani yake Boukheit, sura nyingi zimechorewa minazi kuonyesha anavyoithamini. Ametunga shairi la kusifu maji (uk 73) pamoja na kusifu ukulima kwani Waswahili wengi pia ni wakulima hodari.

Kwa muhtasari, mazingira ya kijiografia yaliwaathiri watunzi katika utunzi na uwasilishi wa maudhui, hususan katika matumizi ya mashairi ya kimafumbo katika *Malenga wa Mvita na Malenga wa Vumba.*

## 2.8 Jamii ya Waswahili na utunzi wa *Malenga wa Mvita* wa *Malenga Wa Vumba*

Jamii ya waswahili imeathiri utuunzi wa diwani hizi mbili kwa njia kadha. Kwanza, diwani zote mbili zimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili ambayo inazungumzwa na Waswahili.

Pili, utamaduni wa waswahili umeathiri kwa kiasi kikubwa utunzi wa diwani hizi. Kwa mujibu wa uhakiki wa uhistoria mpya (utamaduni), hali zote zinazohusu utamaduni ambamo fasihi huibuka hutiliwa maanani.

Waswahili wamegawanyika katika makabila au koo mbalimbali. Kwa mujibu wa Abdulaziz (1979) koo hizi ni kama vile Wabarawa wazungumzao Chibarawa, Wapate, Wasiu, Wabajuni, Waamu (Wakiwandeo), Wamvita, Wajomvu, Wafunzi wanaozungumza Chichifundi na Wavumba kutoka Vanga.

Ahmadi Nassir anatambua ukoo wake katika shairi la 'Nawauza Kimvita' :

Ndimi fundi mshairi, na jina likumbukeni
2. Ni Ahmadi nasiri, juma Bhalo elewani
Kimvita chakhubiri, waswahili nijibuni
Iwapo mutabaini, munijibu kwa makini
(*Malenga wa Vumba*,Uk.54)

Nasiri anaisifu lugha yake wa kutumia msamiati mpana na kutangaza kwamba kusudio lake ni kusema Kiswahili.

Vile vile, Boukheit anatumia lahaja yake ya Kivumba kutunga mashairi ya *Malenga* wa *Vumba*. Amejaribu kubainisha misemo mingi ya Kivumba na jinsi ilivyo tofauti na lahaja nyingine katika shairi la 'Kiwiliwili sikia' :

K'akuna asomuoga, kuogova siku hiyo
1. Rosini rwalegalega, ruhu zatwenenda mbiyo
Dunia ruchaiaga, pasi na matamaniyo
Pasi na matamaniyo, wenzeru washaiga
(*Malenga wa Vumba*,Uk.24)

Kutoka Tanzania, koo za Waswahili ni Wamrima (Wamtangata), Waunguja na Wapemba.

Koo zingine za Waswahili ni Wangazija na Wanzuani wapatikanao kwenye visiwa vya Ngazija. Katika visiwa vya Unguja na Pemba, kuna koo tatu ambazo

huzumgumza lahaja tatu tofauti hususan Waunguja, Watumbatu na Wahadimu (Mbaabu 1978:22).

Kwa muhtasari, Waswahili huishi katika pwani na visiwa vya Afrika Mashariki kuanzia Somalia hadi visiwa vya Komoro.

Waswahili wa Mombasa (Mvita) wamegawanyika miji kumi na miwili. Miji hii imegawanywa makundi mawili yaani Miji Mitatu na Miji Tisa. Kundi la kwanza linajumuiasha Wachangamwe, Wakilindini na Watangana. Kundi la pili ambalo limeundwa na Miji Tisa (Tisa- Taifa) ni Wamvita, Wakilifi, Wajomvu, Wamtwapa, Washaka, Wapate, Wafaza, Wakatwa Na Wabajuni (Wangunya).

Waswahili huzungumza Kiswahili kama lugha yao ya kwanza ambayo imekuwa ikitumiwa tangu enzi za mababu zao (Abdulaziz 1979: 21-22). Waswahili wamewahi kutembelewa na wageni mbalimbali kama vile Waarabu, Wahindi, Waajemi, Wachina pamoja na Wareno. Hawa wote walitua nchini mwa Waswahili wakiwa safarini kuelekea India na maeneo mengine ulimwenguni.

Hata hivyo, yasemekana wageni wa kwanza kuja baadhi ya janibu za Uswahili walikuwa wa kabila la Banu Ghassami, wenye asili ya nchi ya Shamu (Syria). Baada ya kufika sehemu hizi walioana na wanawake wa Kiswahili. Wageni hawa waliwakuta Waswahili wakiwa katika mazingira ya utamaduni wao wakiongea lugha yao ya Kiswahili. Wageni hawa waliwakuta waswahili wakiwa katika mazingira ya utamaduni wao wakiongea lugha yao ya Kiswahili. Moja ya hizo tamaduni zao ni nyimbo- nyimbo za Kiswahili. Nyimbo hizo zilikuwa zikiimbwa kwa mitindo ya mashairi (Saadan A. Kandoro 2003: 118).

Athari ya Wareno inadhihirika katika *Malenga wa Mvita* (Utangulizi). Mfano wa mashairi ambayo yasemekana ni ya wakati wa Mreno na ambayo watungaji wake hawajulikani ni pamoja na:

Portugesi afala, faliki afala velo
Baziyada spanyola, wa tafarai busolo
Si nyama za kuanila, dafedhali dafedhalo
Vinyu inakusumbula, vinyu na butizialo

Limefasiriwa hivi:

Mreno yumo hunena, hunena mambo ya kale
Baziada msipana, dira yuilekezele
Si nyama za muamana, heri zitoe kimbele
Chupani imeshupana, mvinyo ikudhikile

Kutokana na uhusiano wa Waswaili na wageni, Kiswahili kimetohoa maneno mengi ya kigeni kutoka katika lugha za kigeni kama vile Kiarabu, Kihindi, Kiajemi, Kijerumani, Kituruki, Kireno na Kiingereza. Mila na tamaduni za Waswahili vile vile zimeathiriwa na tamaduni za kigeni hasa dini ya kiislamu (Nurse na Spear 1985).

Jambo lingine lililokuwa dhahiri Mombasa (Mvita) na kwingineko Uswahilini ni kuwepo kwa matabaka ya wangwana na watwana. Wangwana walitoka tabaka la juu ilhali watwana walikuwa wa tabaka la chini. Watwana walikuwa wafanyakazi wa waungwana. Utabaka unadhihirika katika utunzi wa Ahmadi Nassir katika shairi lake la 'Zindukani' (uk 120):

2. Siliwale mlimwengu, malimwengu siliwale
Yazingatile ya M'ngu, na M'ngu mzingatile
Hupa nyale mato kungu, matu kungu hupa nyale
Wali wale leo wale, wale wale ndio wale

Mtunzi huyu anaonekana kushutumu tabia ya kuwadharau walio chini au maskini. Boukheit kwa upande wake anakashifu ukabaila au tabia ya kujiona

bora kuliko wengine. Tabia hii mbovu, ustadi Boukheit anaipa jina 'Mnyama Mui' yaani mnyama muovu anayedhuru watu. Katika shairi la 'Nyama huyu kabaila anasema:

Kabaila nyama mui, nyama aso na huruma
7. Muovu aula chui, si mwema katu si mwema
Huyu kwetu ni adui, shamba letu talichoma
Kiunga atakichoma, nyama huyu kabaila

Ahmadi na Boukheit wanakataa jamii ya kitabaka na kupendelea iliyo na haki na usawa. Mashairi yao yanawahimiza watu wote waheshimiane na kusaidiana. Mfumo huu wa jamii ya Waswahili uliathiri ufumbaji wa mashairi ya *Malenga wa Mvita na Malenga wa Vumba.*

## 2.9 Imani, dini na lugha ya Kiswahili na utunzi wa Ahmadi Nassir na Boukheit Amana

Sehemu hii ni muhimu katika kubainisha jinsi imani, dini na athari zake katika lugha ya Kiswahili viliwaathiri watunzi wa mashairi ya *Malenga wa Vumba* na *Malenga wa Mvita.*

Kuja kwa Waarabu na dini ya Kiislamu katika pwani ya Afrika Mashariki vilikuwa na athari kubwa katika lugha ya Kiswahili pamoja na itikadi nzima ya Waswahili (Chacha 1987; Nyanchama 2004: 6). Kabla ya majilio ya dini ya Kiislamu, Waswahili walikuwa na dini yao kama Waafrika wengine. Walitoa sadaka na maombi kwa Miungu yao (Nyanchama 2004).

Hivi leo, takribani idadi kubwa ya waswahili ni wafuasi wa dini ya Kiislamu (Nurse na spear 1985). Imani ya Waswahili kwa Mungu inadhihirika kupitia shairi la Ahmadi Nassir liitwalo 'Imapo siku ya M'ngu'.

Sichoke stahamili, utizame ulimwengu
2. Mazito kikukabili, ni maandishi ya M'ngu
Ubora tuza akili, usijitiye tewengu
Imapo siku ya M'ngu, hapatakuwa la kuwa.
(*Malenga wa Mvita*, Uk.107).

Mwandishi anawahimiza waja wamwamini Mungu wao kwa yale yanayowakabili au kuwakumba. Anahimiza waja wasiwe na wasiwasi bora wamtegemee Muumba wao. Katika shairi la 'Bora mno ni subira',Nassir anasema:

Nanena nawe nafusi, sikithirishe fikira
1. Kujitiya wasiwasi, ni bure mara kwa mara
Mtashakari Quddusi, sichoke yangakukera
Bora mno ni subira, hakuna lisilokoma
(*Malenga wa Vumba*, Uk.111).

Mshairi anazungumza na nafsi yake akiihimiza ipate kumwamini Mungu zaidi na kuacha wasiwasi au kukereka na yanayofanyika ulimwenguni.

Boukheit pia ameathiriwa na dini katika utunzi wake. Katika utunzi wake wa 'Ujumbe wa mauti'. Kwa mfano anasema:

Naapa kwake manani
28. Kuanzia leo hivi
Taifata Qur'ani
Na masjidi tangia

Saumu taimaliza
29. Na Hijja nitatimiza
Niyatende ya muweza
Binniyati si kwa ria
(*Malenga wa Vumba*, Uk 104).

Washairi ni Waislamu na kama tujuavyo Waislamu husoma na kufuata mafunzo kutoka kitabu chao cha *Qurani*. Waislamu pia huenda kuhijj huko Meka aghalabu mara moja maishani kando na mambo mengine yanayofungana na dini ya Kiislamu

Ingawa hivyo, dini ya Kiislamu imeathiri ndoa, makazi, mavazi na fasihi ya Kiswahili miongoni mwa Waswahili. Takribani wanawake wote huvaa buibui (hijab), vazi lililoaminiwa sana katika dini ya kiislamu. Vazi hili huvaliwa na wanawake wanapotoka nje ili kuweka heshima yao ya kusetiri wasije wakatamaniwa na wanaume. Vazi hili linafunika miili yao gubigubi. Aidha, maswala ya ndoa na talaka yameathiriwa mno na dini ya kiislamu. Dhana ya kufu iliwafisha moyo wanawake kuolewa na watu waliochukuliwa kutoka kwenye kufu duni (Momanyi, 1998).

Ahmadi Nassir ameathiriwa na dini ya kiislamu kuhusiana na maswala ya ndoa anapotunga shairi lake 'Owa' linalosemekana kuwa limefanana na la Muyaka:

Owa aliye na kheri, muandamane kwa dini
2. Owa yai la johari, litiye nuru nyumbani
Owa mdomo mzuri, ukupambie lisani
Owa ungiye nyumbani, mpendane na mkeyo

Owa Moyo wa imani, usosumbua mafuja
3. Owa usiowe duni, anayeitwa kioja
Owa mtenda ya dini, ndiye mke mwenye haja
Owa utungiwe koja, mupendane na mkeyo.
(*Malenga wa Mvita*, Uk.158)

Mwandishi anamhimiza msomaji wake aoe mke mwenye imani, mtiifu na atakayemtumikia.

Boukheit kwa upande wake anapinga mfumo pamoja na mitindo ya zamani ya ndoa ambapo wanawake waliwatumikia waume zao. Anapiga vita ubabe-dume pamoja na kasumba ya kuwainua wanaume huku wanawake wakitweza. Mwandishi huyu amejifanya mtetezi wa haki za wanawake katika shairi la 'uhaba wa kazi (uk.42). Hata hivyo, anahimiza ushirikiano wa mke na mumewe anaposema:

Baba mbele mama nyuma, yamekuwa simulizi
Muradi zote twasoma, soteni tuwe walezi
Wake haturudi nyuma, tunataka mapinduzi
Maisha ya siku hizi, watu ni bega kwa bega.
(*Malenga wa Vumba,* Uk. 42).

Katika jamii ya Waswahili, ndoa huithinishwa na kadhi, mwalimu wa dini au Khalibu. Mbali na ndoa iliyokubalika, Waswahili pia walikubali ndoa ya usuria iliyokuwa ndoa isiyoambatana na sherehe yoyote (Momanyi 1998:45).

Ili ndoa ifanyike, mvulana anastahili kutoa mahari kwa msichana. Mahari hiyo huweza kutumiwa kununulia vitu vya kupambia nyumba ya mke. Mke ana ruhusa ya kubeba vitu hivyo iwapo ndoa hiyo itavunjika. Mshenga ndiye hutumwa kupeleka posa kwa wazazi wa msichana. Wazazi huwachagulia wana wao wachumba. Waswahili pia huthamini kudumisha ubikira kwa mabinti zao. Binti huruhusiwa kutoka tu anapokwenda safarini (Mbaabu 1985: Nyanchama 2004).

King'ei akishadidia swala la ndoa kwa Waswahili anasema:

"Waswahili huthamini sana ubikira na hujaribu juu chini kuwatunza binti zao ili wawe bikira pale wanapoozwa kwani ubikira huchukuliwa kuwa kielelezo cha uadilifu au tabia njema" (King'ei, 2003:6-7).

Dini ya Kiislamu pia inaruhusu kutoa talaka. Talaka huruhusiwa iwapo mke hatosheki na malezi ya mumewe kwani mume ndiye hushughulika na kuwalisha familia yake (Nyanchama 2004:63). Pamoja na kuathiri mavazi na ndoa, dini ya Kiislamu pia iliathiri aina ya elimu iliyotolewa katika jamii ya Waswahili.

Kabla ya kuanzishwa kwa mfumo wa elimu ya kimagharibi watoto walipewa elimu ya madarasa ambayo ilihusu mafundisho ya dini ya Kiislamu wakitumia hati za Kiarabu (Mbaabu 1996). Mfumo wa awali wa elimu ulibadilisha baada ya



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

kuanzishwa kwa mfumo wa Kimagharibi uliofuata mitaala na fasihi na Wakoloni (Waingereza).

Kujifunza lugha na fasihi kulifanya kupitia kusikiliza. Hata hivyo, baada ya kuanzishwa kwa mfumo wa Kimagharibi, wahusika walianzisha lugha na fasihi mpya zilizotoka katika tamaduni tofauti (Nyanchama 2004: 64). Hati zilizotumika zilikuwa za Kirumi tofauti na hati za awali za Kiarabu.

Elimu ya kimagharibi imechangia na kuathiri kwa kiasi kikubwa kuandikwa kwa diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*. Ahmadi na Boukheit walipitia chini ya mfumo huo wa elimu ambao uliwawezesha kuandika mashairi ya diwani hizo. Awali, fasihi ya waswahili ilihusu hadithi kama vile za Abunuwasi. Mafunzo yalitolewa mapema kupitia vitendawili na ufumbaji. Jambo hili lilichangia pakubwa baadaye katika utamaduni wa kutunga mashairi kutoka upande wa watunzi na wasiklizaji. Watunzi walikuwa na njia ya kuficha tashtiti kwa kutumia jazanda au sitiari, tashbihi na vitendawili. Katika *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba,* watunzi wametumia mafumbo kadhaa, tashbihi, sitiari pamoja na mashairi ya kimafumbo kuwasilisha maudhui ya diwani zao.

Aidha, Waswahili wanatumia hadithi kuelimisha wadogo kwa wakubwa. Isitoshe fasihi yao inatawaliwa na hadithi za manabii wa Kiislamu kama vile Mohamed, Adam, Ibrahim na Ismail.

Kutokana na maelezo haya, ifahamike kuwa mafunzo ya dini ya Kiislamu waliyopewa Nasiri na Boukheit yamechangia usawiri wa baadhi ya maudhui ya diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba.*



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

### 2.10 Shughuli za kiuchumi na umbuji wa *Malenga wa Mvita* na *Malenga Wa Vumba*

Sehemu hii ni muhimu kwa sababu inachangia kuonyesha jinsi shughuli za kiuchumi zilivyochangia katika utunzi na ufumbaji wa mashairi ya *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*. Waswahili wana shughuli nyingi ziliozohusiana na bahari kwa sababu ya kuishi karibu nayo. Shughuli za kiuchumi huko ni pamoja na kuunda vyombo vya baharini, kuvua samaki, kushiriki kilimo na ufugaji.

Waswahili hufanya au hujihusisha na biashara za aina mbalimbali. Kwa mfano, mabaharia husafirisha bidhaa kati ya miji mbalimbali ya pwani (Nurse na Spear, 1985). Wakati mwingine bidhaa hizo zinasafirishwa kati ya pwani na sehemu nyingine za ng'ambo hususan Uarabuni na Bara Hindi. Bidhaa hizo zinasafirishwa kwa majahazi makubwa kwenda miji mbalimbali (Abdulaziz, 1979:50; Chiraghdin, 1987:6).

Waswahili matajiri hushiriki kilimo na hulima mazao ya kila aina. Mazao hayo ni kama vile nazi, korosho, mpunga, mihogo, mahindi, mtama, mboga na matunda kama vile maembe, machungwa na ndizi.

Umuhimu wa mnazi kwa wakazi wa pwani si jambo geni. Katika shairi la 'mnazi' (uk. 95) Ahmadi Nassir amefafanua baadhi ya matumizi ya mnazi huku yakiranda katika maeneo ya kijamii, kiuchumi na hata kitamaduni. Kwenye mmea huo kunapatikana pato la kifedha, dawa, vyakula na hata vifaa vya michezo vitumiwavyo na watoto. Mtunzi anasema:

Tunda lakwe hupikiya, kwa kutowa tui nazi
2. Penye wali hutujiya, hapikiya na mituzi
Na samaki hapakiya, khaswa tafi na mkizi
Sitouwata mnazi, mti wa faida nami

Enywi miti mitukufu, wana wa shina na mizi

20. Musiudhike hiswifu, utukufu wa mnazi
Meutukuza latwifu, kwa kuupa swifa hizi
Sitouwata mnazi, mti wa faida nami.
(*Malenga wa Mvita,* 1971:95)

Ujumbe ulio katika beti hizi ni kwamba mnazi una faida nyingi na ndio kwamba mtunzi anasema hawezi kuacha mti wa manufaa. Boukheit alipotunga shairi linalohusu mnazi liitwalo 'Mazaoye ya shinani' alisema:

Mnazi toka dahari, fakhari yao warembo
2. Kumeakwo si papari, uonapo lake umbo
Wamea kisirisiri, na tilatila majambo
Mnazi mezuwa mambo, mazaoye ya shinani.
(*Malenga wa Vumba,* 1982:29)

Kutokana na ubeti huu ni dhahiri kwamba upanzi wa minazi ni mojawapo wa shughuli muhimu sana katika jamii ya Waswahili.

Pamoja na upanzi wa mimea, Waswahili pia hufuga ng'ombe, kondoo, mbuzi, kuku na hata punda. Kwa mfano, Waswahili hufuga punda kwa minajili ya kuwatumia kubebea mizigo sokoni.

Biashara ndogo ndogo pia ni kazi inayofanywa na Waswahili. Wanashiriki biashara kama vile ya masoko ya samaki, nyama na mikahawa. Kina mama na mabinti hupika mahamri na vyakula vinginevyo na kuviuza madukani na hata sokoni.

Katika shairi la 'Bidhaa zakosa soko' Boukheit anawatetea wanajamii wenzake kwa kuharibika soko la mazao yao.

Mazao tuliyozaa, mema yenye nang'aniko
Yavutia matufaa, maembe na matomoko
Maghalani yamejaa, tamaa tembe haiko
Zatupa misukosuko, bidhaa kukosa soko
(*Malenga wa Vumba,* Uk. 30)

Mwandishi anazungumzia bidhaa kadha ambazo huzalishwa na jamii yake na kwamba zimekosa soko ama hazipati kununuliwa. Boukheit vile vile anadokeza kwamba Waswahili wanafanya au hujihusisha na kazi za ajira kama vile kuajiriwa maofisini. Mwandishi huyu alifanya hivyo kupitia shairi la ngojera liitwalo 'Uhaba wa kazi':

Kaka: Kusoma nilikosoma, kambiwa sipati kazi
Yapata mwaka mzima, nategemea shangazi
Wasiojuwa husema, sababu sina ujuzi
Huno uhaba wa kazi, mesababishwa ni wake.
(*Malenga wa Vumba*, Uk.42).

Mwandishi huyu anatumia shairi hili kuonyesha ubaguzi ulioko dhidi ya wanawake katika nyanja za ushindani mkali kati ya wanawake na wanaume baada ya kupata elimu ya kimagharibi.

Kuwepo kwa wasomi katika jamii ya Waswahili kunadhihirika katika diwani ya *Malenga wa Mvita* kupitia shairi la Ahmadi Nassir liitwalo 'Nawau'za Kimvita':

Tama natiya khatima, jina langu tabashiri
32. Ahmadi N. Juma, mtungaji mashuhuri.
Nilopata diploma, kwa kutunga mashairi
Na zaidi ya khabari, nikosapo samahani.
(*Malenga wa Mvita*, Uk.54).

Mshairi anatuonyesha jinsi anavyothamini elimu ya uandishi wa mashairi pamoja na diploma aliyopata kutokana na elimu hiyo.

Kazi nyingi zinazofanywa Uswahilini ni kama vile biashara, kilimo, uvuvi, useremala na uashi na kazi hizo hupitishwa kutoka kizazi hadi kingine. Kutokana na desturi hii watunzi wa *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba* wamerithi ufundi wa kutunga mashairi yao kutoka kwa watangulizi wao, hususan wazazi

wao. Kwa muhtasari, hizi ndizo baadhi ya kazi ambazo zimekuwa zikifanywa na Waswahili tangu jadi.

## 2.11 Kiishilio

Sura hii imeshughulikia historia ya mwandishi, utamaduni wa Waswahili na uhusiano kati ya shughuli za kiuchumi na kijamii na utunzi wa *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*. Imebainika kwamba mazingira ya utunzi (yaani historia na utamaduni wa mtunzi) yameathiri utunzi wa mashairi ya malenga hawa wawili kifani na kimaudhui. Kwa mfano, imedhilika kwamba Waswahili walitumia ushairi kama walivyofanya Ahmadi na Boukheit kuzungumzia maswala kama vile ya kisiasa na kitabaka. Walifanya hivyo kwa kutumia lugha ya kimafumbo hususan tashibihi, sitiari na jazanda ili kuficha makali ya ujumbe huo na kuufanya ueleweke kwa njia halisi

Hali ya kisiasa nchini ilirutubisha maudhui ya mtunzi wa *Malenga wa Vumba*. Kwanza, amesema ni lazima wananchi wawe na kiongozi wanayemwamini na kumpenda. Pili kiongozi huyo ni lazima awe mwenye busara, tena asiyekuwa na ubaguzi. Tatu, ni lazima wananchi wajuwe kwamba ubaguzi ni tendo baya kwani huleta hasara nchini na kudhuru uchumi. Katika shairi la 'Heshima ya Serikali' (uk. 85):

Kalili huwa imara, iwapo na kiongozi
2. Kiongozi wa busara, asiye na ubaguzi
Ubaguzi ni hasara, isofaa siku hizi
Siku hizi za fikara, za watu wanomaizi
Kumaizi yalo bora, yasiyo na pingamizi.
(*Malenga wa Vumba*, Uk.85).

Katika kuzidi kuendelea kuangazia zaidi juu ya mambo muhimu ya kisiasa, Boukheit amejaribu katika shairi lake la W-A-S-I-F-U W-A B-A-B-A K-E-N-Y-A-T-T-A (uk 66) kuweka kumbukumbu kwa vizazi vijavyo vijue ile kazi ngumu iliyofanyiwa taifa hili la Kenya na mzee Jomo Kenyatta aliyekuwa rais wa kwanza wa taifa hili. Katika shairi hili anasema:

17. Ameivunja miamba, nyayoze twakanyagia
Na nchi akaipamba, baraka kututilia
Akaifunga na kamba, harambee kuivutia
Ndipo twaomba muumba, Kenyatta mshufaia.
(*Malenga wa Vumba*, Uk.66).

Boukheit vile vile alikisifu chama tawala cha wakati wa utunzi wake yaani chama cha KANU.

Katika shairi lake la 'Chama cha Haki' anasema hivi:

4. Kaka: Kamwe dadangu sichoki, kukupa yangu maoni
Wala sifanyi hamaki, kanena yaso maoni
KANU ni chama cha haki, maarufu duniani
Maanaye twaamini, KANU ni chama cha haki.
(*Malenga wa Vumba*, Uk.77).

Katika ubeti huu mshairi anadhihirisha uaminifu wake kwa chama tawala cha KANU. Kwa muhtasari, malezi waliyopewa Ahmadi na Boukheit na wazazi pamoja na jamaa zao yalikuwa na athari kubwa katika maandishi na maisha yao kwa jumla. Kutokana na maelezo haya, imedhihirika jinsi fasihi inavyozuka kutokana na mtunzi kuingiliana na mazingira yake. Ndiposa nadharia ya uhistoria mpya inasema kwamba fasihi haiwezi kutengwa na historia, siasa na jamii ambamo inazaliwa. Isitoshe, hali zote zinazohusu utamaduni ambamo fasihi imeibuka hutiliwa maanani.

Kulingana na utafiti huu, kuna sababu kadha zilizochangia matumizi ya mashairi ya kimafumbo katika diwani za *Malenga Wa Mvita* na *Malenga Wa Vumba*. Sababu hizo ni pamoja na historia ya jamii ya Waswahili, malezi waliyopewa watunzi pamoja na mazingira walimolelewa pamoja na mazingira ya kisiasa na kiuchumi katika kipindi cha historia cha utunzi wa mashairi yao.

Sura inayofuata imejadili kwa kina lugha ya kimafumbo katika mashairi ya Kiswahili pamoja na sababu au malengo ya ufumbaji.

# SURA YA TATU

## Matumizi ya lugha katika diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*

### 3.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia uchanganuzi wa lugha ya kimafumbo katika utunzi wa mashairi ya *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*. Lengo kuu ni kubainisha kwamba mashairi kadha ni mafumbo na kwamba lazima yachanganuliwe ili maana kamili ieleweke. Aidha, sehemu hii imebainisha namna mazingira yalivyochangia katika ufumbaji wa mashairi ya Ahmadi na Boukheit.

Kwa mujibu wa uhistoria mpya mtunzi wa fasihi, sawa na fasihi yenyewe, ni zao la mazingira maalumu katika kipindi maalumu cha historia ya jamii. Aidha, mfumo wa jamii huathiri namna msanii anavyouona ulimwengu wake na jinsi anavyousawiri.

Kazi ya kifasihi hupewa msukumo, umbo, mwelekeo, maudhui na nguvu za kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa mujibu wa jamii husika (Odaga, 1985: xxi; Masinde 2003:32). Hivyo, imebainika kwamba mashairi ya Ahmadi Nassir na Boukheit Amana ni kazi za utunzi zenye uyakini uliofungamana na wakati, mazingira na mfumo wa jamii. Aidha, chimbuko la ujumbe wa kazi za Ahmadi Nassir na Boukheit Amana ni mazingira halisi ya jamii kwa mujibu wa wakati maalumu kihistoria.

Kila mtunzi huwa ameathiriwa na mazingira na mambo mengi maishani mwake na athari hizi hazina budi kujitokeza katika tungo zake (Syambo na Mazrui, 1992: xii). Haya ni maelezo yanayoafiki kipengele cha nadharia ya Uhistoria mpya kinachodai kwamba fasihi haiwezi kutengwa na historia inayohusika nayo. Watu

hukulia katika jamii fulani na aghalabu mtazamo wao wa jambo hufinyangwa kwa kiasi fulani na mazingira na utamaduni wao (Masinde 2003:33). Hivyo, tungo zote za kifasihi ni zao la jumuiya fulani katika kipindi maalumu kihistoria. Uchambuzi wa kazi yoyote ya kifasihi lazima uhusishe miktadha ya kihistoria kwa makini na utaratibu mkubwa ili kudengua maana zote zinazoweza kumsaidia msomaji na msikilizaji kuielewa.

Mashairi ya kisasa yamesarifu ujumla wa maisha yetu yote. Kwa mujibu wa Uhistoria mpya, matakwa ya kijamii na kisiasa huathiri utoaji na upokeaji wa kazi za kifasihi. Athari hizi hazina budi kujitokeza katika kazi za watunzi kwa mujibu wa mapito ya wakati.

Fasihi ni sanaa inayowasilisha hali, maingiliano, mivutano na mikinzano miongoni mwa binadamu na mazingira yake. Msomaji au msikilizaji wa kazi yoyote ya kifasihi huingiliana na tajriba za hali iliyowasilishwa na wahusika wa kazi hiyo kama walivyosawiriwa, na huku akikata kauli kuhusu ukweli, uhalisi na ubora wa yale anayokumbana nayo (Njogu na Chimera, 1999:26).

Msanii aghalabu, hutunga kutegemea hali halisi ipatikanayo katika jamii husika. Huongozwa na itikadi katika uelezaji wa matukio ya jamii husika, na itikadi hiyo hujibainisha katika umbuji wake. Kwa mujibu wa Uhistoria mpya, mhakiki hana budi kueleza dhamira za mtunzi kwani jambo hili huathiri na kubadili maendeleo ya historia ya kazi ya kifasihi.

Fasihi ni ile huboreshwa na kuimarishwa kwa ujenzi wa jamii imara yenye uadilifu wa usawa na haki (Masinde, 2003:35). Haya yamebainika katika utunzi wa *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba* katika harakati zao za kuadili jamii

kupitia mashairi yao ya unyumba pamoja na yale yanayohusu uhusiano kati ya mke na mume (ndoa).

Aidha, diwani hizi mbili zimefafanua nafasi ya dini katika maisha ya binadamu.

Kwa mujibu wa nadharia ya uhistoria mpya, mhakiki hana budi kuangalia hadhira ya sasa na ya siku zijazo kwa urazini kwa kufafanua madhumuni na eneo la uhakiki wake. Kazi ya mwandishi wa fasihi ni kiungo cha jamii anayoilenga. Hivyo, kazi yake haiwezi kutengwa na jamii yake. Aidha, fasihi ni mafunzo na maadili yanayojenga mshikamano wa kijamii. Fasihi imetumika katika maombi na makafara ili binadamu apendeze machoni mwa Mungu au miungu yake. Ushairi kama vile *Utenzi wa Al-Inkishafi* wa Abdalla bin Nassir (1718-1815), *Utenzi wa Mwanakupona* wa Mwanakupona Binti Mshamu (1790-1860) pamoja na diwani ya *Malenga wa Mvita* ya Ahmadi Nassir (1971), yamegusia masuala ya kidini.

Kwa mfano 'Al-Inkishafi' ni shairi lililotungwa na Sayyid Abdalla bin Nassir (1718–1815). Mwandishi huyu aliyeishi pate alikuwa mwalimu mwenye ujuzi wa dini na sharia za Kiislamu. Vile vile, alikuwa ni mmoja katika ukoo wa washairi kwa baba na mababu (Chiraghdin, 1987:1).

'Al–Inkishafi' ni utungo wa kidini uliokusanya mambo mengi mazuri. Mshairi anauonya moyo wake usifuate hawaa ya nafusi, uache raha za kilimwengu na uandame mambo yanayomwajibikia Mwenyezi Mungu. Aidha, aonyesha kuwa dunia sio makao ya binadamu ila ni mapito tu ya kwenda ahera. Kwa mfano kuhusu matajiri wa Pate alisema:

Nyumba zao mbake zikinawiri
1. Kwa taa za kowa na za sufuri
Masiku yakele kama nahari
Haiba na jaha iwazingile.

(*Malenga wa Karne Moja*, 1987:2)

Hawa ni matajiri walioishi maisha ya raha mustarehe duniani.

Hata hivyo, baada ya kifo chao tunanyeshwa taswira tofauti:

Nyumba zao mbake ziwele tame
10. Makinda ya popo iyu wengeme
Hasikii hisi wala ukeme
Zitanda matandu walitandiye.
(*Malenga wa Karne Moja*, 1987:3).

Mwanakupona Binti Mshamu (1790 -1860) aliyekuwa mke wa Bwana Mataka alizaliwa huko Pate na baadaye akahamia Lamu. Alikuwa akitunga kwa lengo la kumuasa binti yake Mwana Hashima binti Mataka mafunzo ya namna ya kuishi na mumewe kwa kumtii na kusikiliza amri yake kulingana na sharia za Kiislamu. Vile vile, utungo huu una mawaidha juu ya kutangamana na kwenenda na marafiki, ndugu na watu wa aina mbalimbali. Kwa mfano:

Mwanangu uwe sandiki, na awe radhi mumeo
3. Ushikalo ulithiki, siku zote mukaao
Mtu asoshika haki, siku akhitariwao
Saandamane nae ndia, awe radhi mekuwia.
(*Malenga wa Karne Moja*, 1987:38).

Kuhusu watu wengine Mwanakupona anasema:

Mwanangu siwe mkoo, akupendae mpende
9. Tenda kama nonao, akuizao mwenende
Kupea na kosha choo, kwa zema mvundevunde
Si dharau mara moya, la'ala akaridhiya.
(*Malenga wa Karne Moja*, 1987:38)

Kwa hivyo, kazi ya fasihi huonyesha uhalisi na hujaribu kuwashawishi watu kuwa na mwelekeo fulani kuhusu huo uhalisi (Masinde,2003). Maelezo haya yanatoa taswira kwamba fasihi huwa na madhumuni ya kufunza, kuadilisha, kuonya, kuzindua, kuburudisha, kustarehesha na kurudi miongoni mwa mengine.

### 3.1 Arudhi ya kishairi na migogoro ya utunzi

Sehemu hii imechanganua kwa kifupi arudhi zilizofuatwa na watunzi au jamii ya wanamapokeo au wanajadi walioshikilia kwamba kuna sheria zinazopaswa kufuatwa pamoja na migogoro iliyozuka katika utunzi wa mashairi ya Kiswahili. Kwa mujibu wa nadharia ya uhistoria mpya, ni muhimu kuelewa historia ya kipindi ambamo kazi fulani imeandikwa na kutolewa, na historia ya muktadha ambamo kazi hiyo inasomwa na kufasiriwa (Murfin, 1991: 331). Aidha, hata mashairi yasiyoweza kufanana yanapatikana katika mkumbo au mkururo wa hali za historia, mahusiano ya jamii na maathiriano.

### 3.2 Arudhi

Zamani, ushairi wa Kiswahili ulikuwa ni nyimbo. Nyimbo hizo hazikuwa zikiufuata utaratibu maalumu. Zilikuwa hazina vina na mizani kama kawaida ya ushairi wa leo unavyohitaji (Massamba, 1973:61). Ni baadaye tu ambapo manju na malenga walipoanza utaratibu wa kutumia urari wa vina na mizani. Maelezo haya yana maana kwamba ushairi haukuanza na vina na mizani, na si lazima kwamba utaisha na vina na mizani.

Sheria za utunzi wa mashairi zilifafanuliwa na Sheikh Kaluta Amri Abedi katika *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri Abedi*. Miongoni mwa sheria hizo ni pamoja na vina, mizani, utoshelezi na kituo. Wanamapokeo wanasema kwamba sharti shairi liwe na muundo maalumu ndipo liweze kutambulika kama shairi la Kiswahili. Wanaeleza kuwa ni kawaida na kaida ya maumbile kuwa jambo lolote linalofanywa na jamii ya watu hutambulika kwa linavyofanywa (Ruo, 1989:16; Masinde, 2003).

Arudhi ni istilahi inayotumiwa kuelezea nadharia ya utunzi wa mashairi (Wamitila 2003: 24). Kimsingi arudhi huhusisha uchuguzi wa jinsi ya mashairi, vina, mizani, utoshelezi, urari na beti.

Mizani ni dhana hii inayotumiwa katika taaluma ya ushairi kurejelea silabi zinazoweza kutamkika. Kwa kawaida shairi la kimapokeo huwa na idadi maalumu ya mizani (Wamitila 2003:128). Kila silabi moja ni mizani moja. Kwa hivyo, mizani ni matamshi au tamshi kamili au mapigo ya sauti katika neno.

Kwa mfano:

Pe-ndo-ni pa-nde the-ni-ne, la ku-mo-ja si-o pe-ndo
(1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16)

La kumoja lina mavune, mwingi mno uvundo
Hilo msiandamane, lahasiri kama kondo
Siri kubwa ya mapendo, kupenda akupendaye
(K.W, Wamitila, *Pendo*, kaza macho)

Vina ni dhana inayotumiwa katika taaluma ya ushairi kuelezea silabi zinazofanana katika sehemu sawa katika mpangilio wa ubeti wa shairi. (Wamitila, 2003:345). Kwa hivyo, vina vya shairi ni silabi za mwisho wa maneno zinazotokana, yaani silabi zenye sauti moja. Kwa mfano, ikiwa neno la mwisho katika mshororo mmoja ni furahika, kinache ni ka na neno la mwisho la mshororo wa pili liwe linaisha kwa 'ka'.

Ubeti ni kifungu cha maneno kilichoandikwa kwa ufundi wa kishairi. Wingi wake ni beti. Ni kifungu cha mshororo mmoja au mishororo kadha katika shairi na ambacho kinajitosheleza. Mishororo hiyo inaweza ikawa na mpangilio fulani wa vina na mizani au isiwe nao. Ubeti ni dhana ya kimaana ambayo inafanana na aya katika uandishi wa kinathari kwa kuwa inabeba maana nzima

inayozungumziwa katika kifungu fulani. Shairi linaweza kuwa na ubeti mmoja au zaidi.

Kujitosheleza ni kueleweka kwa habari iliyoandikwa, yaani ubeti ukisomwa wazo liwe limekamilika, limefunuliwa vizuri mshororo hadi mshororo.

Baada ya kusoma ubeti wote, msomaji aone jambo muhimu lililoelezwa bila kutegemea ubeti unaofuata. Vile vile sheria zote za utunzi ziwe zimetumika, kama vile vina na mizani.

Kibwagizo ni neno linaloleta dhana ya kubwaga. Na kubwaga ni hali ya kutupa 'hapo na hapo'. Ni ile hali ya mstari au mshororo wa mwisho kutobadilika katika kila ubeti.

Mchango wetu ni kwamba mpangilio wa maneno katika ushairi, idhini ya kishairi kama vile tabdila, mazda na inkisari, msamiati wa kikale pamoja na kibwagizo tata huchangia katika ufumbaji wa ujumbe au maana ya mshairi.

### 3.3 Migogoro ya utunzi

Wanamapokeo wanashikilia kwamba vina na mizani ndivyo vitambulisho vya ushairi wa Kiswahili. Dai hili lina maana kwamba vina na mizani ndivyo vinatofautisha ushairi wa Kiswahili na kazi nyingine za kifasihi. Dai hili limepingwa na wanamapinduzi wanaotunga mashairi huru.

Zamani, mashairi yaliwakilisha watu wachache na lugha yake ilikuwa ngumu kuielewa isipokuwa kwa wale wenye kipawa cha uchambuzi (Ombuge na Adaka, 1996:11). Kulingana na Njogu na Chimera (1999) mshairi ana uhuru wa kutunga

atakavyo, muradi tu adhihirishe usanifu na apandishe maudhui yake kwa taswira na uteuzi wa lugha.

Wanamapokeo wameshtumiwa kwa kuzingatia muundo sana na kupuuza umuhimu wa maudhui, hivi kwamba wamekuja kuonekana kama Wanamaumbo. Kendoro ambaye ni mwanamapokeo anadai kwamba vitu huelezwa kwa umbo lake maalumu:

Wasojua hubishana, na mjuaji wa vitu
Wakawa waelezana, ingawa mbele za watu
Shabaha huonyeshana, zisadi ubishi wetu
Umbile umbo la kitu, kitu hutambulikana.

Sokwe akapewa jina, huyu sokwe mtu
Watu kukubaliana, sokwe ni mwenzetu
Ni wazi twajitukana, kudharau wetu utu
Umbile umbo la kitu, kitu hutambulikana
(*Mashairi ya Saadan*, 1972)

Mshairi huyu, kwa kumfananisha binadamu na sokwe mtu, anaonyesha tofauti zilizopo baina ya mashairi yanayofuata arudhi na mashairi huru. Anadai kuwa kwa vile mashairi huru hayana muundo wa kimapokezi, hayawezi kuitwa mashairi ya Kiswahili. Hoja hapa ni kuwa umbo la shairi ni kitu cha msingi.

Wanausasa, washairi ambao wamepuuzilia mbali arudhi, wanasema kuwa hakuna sheria za kutunga mashairi (Kezilahabi, 1974:60). Wanausasa wanadai kwamba kila mshairi ana njia yake ya kutunga mashairi, na njia yake ya kutoa mawazo ya kishairi. Wanasisitiza kuwa zile mbinu ambazo washairi huziita 'sheria' ni ufanano wa mashairi wakati fulani kihistoria; lakini si sheria. Kundi hili la wanasiasa wanadai kwamba dhamira na maudhui, mawazo, maadili, na falsafa zitawale fani ya ushairi. Watunzi hawa wangetaka mshairi wa Kiswahili asifungike kwenye sheria za mishororo, beti, vina na mizani.

E. Kezilahabi ameandika shairi linalofafanua mawazo ya msimamo huu katika utangulizi wa *Kichomi:*

Mtu yoyote akiniuliza,
Kwa nini vina mizani,
Situmii na mistari na,
Beti sitoshelezi,
Nitamwambia: Rafiki
Kuna njia nyingi za kwenda
Bustanini.
Lakini kama mtu yule yule
Kunizoza akiendelea na kuniambia

Nitamwambia;
Rafiki, twende nyumbani kwangu
Kwa miguu, na nyumbani kwangu
Tukifika jaribu kunifunza
Kutembea.
(Uk. Xiii).

Maoni yake ni kwamba mshairi ana uhuru wa kutunga atakavyo, muradi tu adhihirishe usanifu na apandishe maudhui yake kwa taswira na uteuzi wa lugha. Kwa hakika, si lazima vina na mizani viwepo katika shairi. Shairi linaweza kuvutia bila matumizi ya kaida hizo ilmradi mtunzi ateue maneno yake vizuri ili aeleze hisia zake kwa njia inayonata akilini mwa msomaji, na shairi liwe la kupendeza. Wanamapokeo wanashikilia kuwa lazima waige vile waandishi maarufu wa zamani walivyoandika. Mtazamo huu umeendelezwa na Harold Bloom (1988) pamoja na washairi wengine. Mtazamo huu huwasawiri washairi kama waigaji wa watunzi wa zamani, na kwa hivyo inawabidi waige vyema. Mkabala huu wa kitaathira unachukulia kuwa ushairi wa kale ndio ulikuwa na nguvu zaidi. Kulingana na Njogu na Chimera (1999), ushairi wa kale ulikuwa tofauti kwa kiasi fulani na ushairi wa sasa. Waandishi wanaweza kuathiriwa lakini hii haina maana kwamba wanaiga. Kile cha muhimu ni kwamba wazingatie ubunifu.

Madai ya wanausasa ni kuwa miundo mipya haifuatwi ili ichukue nafasi ya ile ya zamani; inafuatwa ili iwe nyongeza ya ile iliyopo, na iwe mchango katika ukwasi wa sanaa ulioachwa na vizazi vilivyotangulia. Pia, wanausasa wanaonekana kudai kwamba, ili kuuelewa ushairi wa leo, itabidi tuuelewe ushairi wa kale. Ni kama kwamba ushairi wa leo unamulika ushairi wa kale, na wa kale unamulika wa leo. Wanausasa wanasisitiza pia kuwa vina na mizani ni kunga za utungaji zilizozuia ushairi wa Kiswahili kukua na kusambaa kwa mapana na marefu yake.

Kezilahabi (1974: xiii) anadai kuwa jambo alilotaka kuhusisha katika ushairi wa Kiswahili ni utumiaji wa lugha ya kawaida; lugha itumiwayo na watu katika mzaungumzo ya kawaida ya kila siku. Kwa maoni yake mashairi ya zamani yalikuwa yakiweka mkazo zaidi kwenye mafumbo, hivi kwamba uelewaji wa ushairi ulikuwa uwezo wa kufumbua fumbo.

Maoni ya kijumla ni kuwa wanamapokeo wanasisitiza vina na mizani wanapoeleza dhana ya ushairi ilhali wanausasa wanazinagatia maudhui. Utafiti huu umezingatia mashairi ya wanamapokeo kwani *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba* wote wamezingatia maoni na mtindo wa wanamapokeo.

### 3.4 Ufumbaji wa mashairi

Sehemu hii imeonyesha jinsi watunzi wa mashairi hufumba mashairi yao pamoja na mbinu wanazotumia kuuficha ujumbe wao kwa wasomaji na wasikilizaji.

Kulingana na kamusi ya Fredrick Johnson (1935), neno 'kufumba' lina maana kadha:

Kwanza, kamusi hii inadai kwamba kufumba ni kukutanisha, kwa mfano kufumba macho ni kukutanisha makope.

Pili, kufumba ni kuficha maana; kufumba maneno ni kutumia maneno magumu yasiyofahamika vizuri. Neno 'ufumbaji' kama tulivyotumia katika utafiti huu lina maana ya 'ficha maana'. Ufumbaji ni neno lenye maana ya kufanya maneno yasemwayo yawe magumu kueleweka na yasijulikane kwa urahisi. Ingawaje ufumbaji huweza kuleta ugumu katika mawasiliano, ufumbaji huo sio jambo la hatari kila wakati katika utoaji wa maarifa na taarifa.

Kulingana na Abedi, K. A. mshairi wa Kiswahili:

> ...Anapenda sana kufumba mawazo yake yasijulikane ila kwa wale wenye kuzielewa kunga hizo.(1954:xiv).

Katika mazingira ya tamaduni mbalimbali, ufumbaji ni jambo la kawaida na lina dhima na umuhimu maalumu. Utafiti huu umeambatana na mhimili wa uhistoria mpya unaodai kwamba matakwa ya kijamii na kisiasa huathiri utoaji na upokeaji wa kazi za fasihi (Greenblatt, 1980). Kila mtunzi huwa ameathiriwa na mazingira na athari hizi hazina budi kujitokeza katika utunzi wake.

Katika fasihi, mafumbo yote yanaweza kutafutiwa jawabu, lakini inahitaji utulivu na upevu wa akili ili kuweza kulitatua fumbo kwa sababu mara nyingi ufumbaji huwa haujulikani kama ni ufumbaji kwani maneno yatumikayo ni yale yale yafahamikayo. Uchunguzi wa kina wa mashairi katika utafiti huu unaafiki mhimili wa ndenguzi unaodai kwamba, udenguzi huzama katika ufafanuzi wa matini na kuitazama kwa jicho la ndani kwa yadengua na kuyabomoa.

Wamitila (2003:50) anasema kwamba neno kufumba hutumiwa kuelezea hali fulani ambao ina ufiche na inahitaji kufikiri ili kuweza kutambua kilichofumbwa.

Gibbe (1990) akinukuu kitabu kilichohaririwa na Omari na Mvungi (1980) anaeleza kuwa:

'Hali hii (=Ufumbaji) ndiyo inayogeuza-geuza maneno kutoka daraja hili kwenda daraja la pili na kadhalika na hali maana yake ya asili ipo palepale.'

Wamitila (2003:97) kufunga nyama: huu ni usemi unaotumiwa kuhusiana na ushairi. Hutumiwa kuelezea tabia au mtindo unaopatikana katika ushairi wa Kiswahili ambapo mshairi hutunga shairi lenye fumbo kasha washairi wenzake hulazimika au hubidiika kujaribu kulifumbua fumbo hilo la kishairi. Hii ni tabia iliyohusishwa na utunzi wa papo kwa papo, bila ya kuwazia utungo kwanza au kuandika.

Wallah (1988: xiv) anasema kwamba upeo wa juu wa utunzi bora wa mashairi huhitaji matumizi mema sana ya maneno. Na si maneno tu, uwepo na ubingwa mkubwa wa kuyatumia maneno haya ili kuyapatia maana uzito kiasi cha kuwa neno la kawaida tu laweza kuwa kama msamiati, msemo, nahau na mithali. Katika utangulizi wa *Malenga wa Mvita*, Chiraghdin (1971:3) anasema hivi:

'...listaajabishalo watu ni uzito na ukale wa lugha yake na kina cha fikira na mawazo yaliyomo'.

Lugha ya ushairi huwa na uzito mkubwa na mawazo yake ni mazito. Lugha inayotumiwa inaonyesha sifa ambazo si kawaida kwa kiwango kikubwa. Sifa hii inaifanya lugha kama walivyoshikilia wanaurasimu wa Kirusi, kuchimuzwa hasa kutokana na miundo yake, msamiati wake na kadhalika.

Mshairi ana uhuru mkubwa zaidi wa kuchanganyachanganya msamiati, kuubadilishabadilisha, ili uafikiane na mahitaji yake ya kishairi ya kipekee. Uhuru

huu wa kupindukia mipaka wa washairi ndio unaotatanisha wasomi katika utanzu huu wa kifasihi.

Mashairi ni ufundi wa lugha ya mkato, na uwasilishaji wa ujumbe kwa maneno haba kuliko hadithi. Kwa hivyo, mchanganuzi wa mshairi anatakikana awe ameutalii sana msamiati wa lugha ya Kiswahili na vile vile awe mjuzi wa kutambua kilichofumbwa katika taswira kemkem (Njogu na Chimera, 1999).

Aidha, mashairi mengi hufumba ujumbe na mchanganuzi hana budi kuufumbua. Mashairi yanaweza kugawika mikondo miwili. Mkondo wa kwanza ni mashairi ya kawaida na mkondo wa pili ni mashairi mazito au ya kimafumbo.

### 3.5 Mashairi yasiyo mafumbo

Mashairi haya hutungwa kwa lugha ya kawaida na huwa rahisi kueleweka. Mashiri haya hushughulikia mada za kawaida kama vile mapenzi, fedha, elimu, lugha ya Kiswahili na kadhalika. Kulingana na Amri K. A.(1954) mtungaji anayetungia mambo ya kawaida lazima atumie lugha nyepesi ya desturi. Diwani za Ahmadi Nassir na Boukheit Amana zimesheheni mashairi ya kawaida. Katika shairi la 'Ufunguo wa Maisha' (uk. 41) Boukheit anasema:

1. Mwanangu njoo karibu, nikupe ya manufaa
   Uyajue ya wajibu, uepukwe na balaa
   Usije kapata tabu, dunia ina hadaa
   Katika ya manufaa, mojawapo ni elimu.
   (*Malenga wa Vumba*)

Mzazi anamuasa mtoto wake ili apate kuelewa kwamba kuna mengi yanayoweza kumpotosha ulimwenguni lakini kilicho muhimu zaidi ni elimu. Lugha ya shairi hili ni nyepesi na inaeleweka waziwazi.

Shairi la 'Ngwenje' (uk. 103) Ahmadi Nassir ametumia lugha inayoeleweka kwa urahisi na mada ambayo hujadiliwa na watu wote yaani pesa. Kila mtu anajua, huhitaji na kutumia pesa. Hata hivyo, pesa ni kitu adimu sana, na zinapotosha. Mshairi anasema:

1. Pesa ni kitu adhwimu, kwa kiumbe duniani
   Hukufanya mahashumu, kwa nduguzo na wendani
   Ukatangaa isimu, zimapo kukuzaini
   Bali zina walakini, tahadharini na pesa.
   *(Malenga wa Mvita)*

Haya ni mashairi yanayoweza kuitwa ya kawaida kwa sababu yametungwa kwa lugha nyepesi na maudhui yake yanaeleweka moja kwa moja.

### 3.6 Mashairi ya kimafumbo/ mashairi mazito

Haya ni mashairi ambayo yanafumba na kutega fumbo. Washairi hutumia aina hii ya mashairi kuonyesha ubingwa wao wa kutumia lugha na pia kuonyesha fahari ya ushairi. Mashairi ya mkondo huu hutungwa kwa ajili ya kueleza kitu maalumu kwa ajili ya mtu au kitu fulani maalumu kinachotendeka au kilichotukia au kile kitakachotukia katika siku zijazo. Mashairi haya huwa na shabaha ya kuonyesha huzuni, furaha, adabu na kadhalika.

Uchambuzi huu umejishughulisha na uchanganuzi wa mashairi haya ya kimafumbo huku ukizingatia mseto wa nadharia ya Uhistoria mpya kupata maana maalumu na vile vile nadharia ya Udenguzi kufumbua maana mbalimbali za

mashairi ya aina hiyo. Hivyo, utafiti huu umeafikiana na mhimili wa udenguzi unaodai kwamba kuna uwezekano wa maingiliano ya fasiri mbili za kazi moja ya kifasihi zisizolingana kamwe.

Uchambuzi wa aina hii ya mashairi ulikuwa ukifanywa tokea zamani. Ni desturi ya ushairi na kama mila ya wenyewe washairi. Uchambuzi wa mashairi ya kimafumbo ulikuwa ukifanywa kwa ukali muda washairi walipokuwa wakipingana na kuchokozana, huyu akimchokoza huyu na huyu akimjibu na huku akiyachambua mashairi ya mwenziwe pamoja na lugha yake. Katika karne iliyopita, Muyaka alichokozana na Mwenyi Jitu, ndipo aliposema:

Ushairi mbwa welevu, jadi ya Mwenyi Malindi
Usambe watoka Jomvu, kwa ngao na Mwachifundi
Silino Jitu pumbavu, nguo livete mapindi
Ujaonapo mnandi, kujenga nyumba kutwani?

Karibuni tunampata Ahmadi Nassir akimchambulia S. Karama katika shairi akisema:

Haniimbi mshairi, hamjibu kwa utambo
Humjilia dhahiri, hamweleza kulla jambo
Apandapo munkari, tukaonyana vigambo
Kwaye muumba wa mambo, mtenzi saya na saya.

Mnyampala anafumba hivi katika diwani yake (1963: 55):

Tambo nakueleteeni, mliotaalamika
Mafundi wa ushindani, kwa mafumbo kufumbuka
Sinalo shaka moyoni, jungu lenu mtapika
Nchi gani ilotoweka, baada ya dunia kuwa?

Alipokuwa anafumbiana na wenzake Ahmadi Nassir alisema hivi (1996:8):

Sambi siwaambii sambi, siwaambili wambi saya
Sayano sawanyi kumbi, masombo wangatatiya
Jimbi tawikia jimbi, awikapo tawikia
Si saya yawele saya, wapo nisaya huwaje?

Ni desturi ya washairi kujigamba na kujitutumua kuonyesha upeo wa ustadi wao katika kuisanii na kuisarifu lugha. Basi katika diwani yake ya *Malenga wa Mvita*, Ahmadi wa Nassir atongoa ungoi wake (Chiraghdin 1971:15).

Saadan A. Kandoro anacheza na neno kitendawili huku akifumba kitendawili ambacho anakitega kama vita vya watu wawili:

1. Imelia tarambeta, yaashiria kitali
Kuicheza hii kwata, muwe wawili wawili
Muwe hodari wa vita, muipige vita kali
Vita nyenda kwa yaleli, kitendawili cha tata.

3. Saadani kakitata, kigumu kitendawili,
Wa kizoma kawaita, na wa Tabora wa pili
Nani majibu taleta, ajibu kitendawili
Vita vyenda kwa yaleli, kitendawili cha tata

Mtu atakayeleta, alete jibu la kweli
4. Asiwe kubwatabwata, kuziburuga kauli
Sote tunajifumbata, twangoja jibu kuwili
Vita vyenda kwa yaleli, kitendawili cha tata.
(K.A Abedi 1954: 80- 81)

Shairi la 'Mkufuu na Mwanafuu' (uk. 65) limefuata mpango wa 'kufunga nyama. Ameichanganya kazi ya malenga wawili na amewaita Mkufuu (Mkufunzi) na Mwanafuu (Mwanafunzi). *Shairi hili limetokana na fumbo la kale la Kimvita:*

Cha mkufuu, mwanafuu ha, na akila hu
Cha mwanafuu, mkufuu hu, na akila ha.

Boukheit kwa upande wake amefumba ujumbe wake kwa kutumia taswira, isitiara na jazanda miongoni mwa mbinu nyingine za lugha na tamathali. Shairi lake la 'Mti Mle' limetumia lakabu ya "mti mle" kujitambulisha. Maana hasa ya lakabu hii ni mti-mrefu, maneno ambayo anakusudia kuwabainishia washairi wenziwe kuwa hakuna mshairi awezaye kukifikilia kilele cha uhodari wake. Papo hapo inaweza kuwa kimo cha umbile lake kwani kimo chake si haba (Msami

1982). Shairi hili linaafiki mhimili wa Udenguzi kuwa matini inaweza kuwa na maana mbili tofauti na zisizoingiliana kamwe.

Katika kuangazia juu ya mambo muhimu ya kisiasa, Boukheit amejaribu katika shairi la 'W-A-S-I-F-U W-A B-A-B-A K-E-N-Y-A-T-T-A' (uk.66) kuweka kumbukumbu kwa vizazi vijavyo vijue ile kazi ngumu iliyofanyiwa taifa hili la Kenya na Mzee Jomo Kenyatta aliyekuwa Rais wa kwanza wa taifa la Kenya. Boukheit anasema:

Ameivunja miamba, nyayoze twakanyagia
17. Na nchi akaipamba, baraka kututilia
Akaifunga na kamba, Harambee kuivutia
Ndipo twaomba muumba, Kenyatta mshufaia.

Katika ukwapi wa ubeti huu, amebainisha kuwa Rais huyu ndiye aliyeivunja miamba, yaani wale waliogandamiza maendeleo ya uchumi wa nchi yetu.

Kupitia kwa washairi kama Muyaka na Shaaban Robert, ushairi wa Kiswahili ulionyesha ufundi mkubwa hasa katika kuleta hali ya utaifa na uzalendo na kuwahimiza watu weusi wajitolee kiwazi kudai nchi na uhuru wao kutokana na utawala wa kiimla ulioletwa  na Wakoloni wa Kiarabu na Kizungu.Mashairi yao yalikuwa na ujumbe mzito wa kisiasa lakini habari yenyewe ilikuwa fichifichi ya kuwazindua wenyeji na kuwafumba wakoloni, kama vile, shairi la Muyaka liitwalo 'Ngome'. (Ombuge na Adaka, 1999:7).

Washairi wa zama za kale walisisitiza ile hali ya mshairi kuibuka na jambo au hoja au fumbo geni zaidi lakini ambalo ladhihirika katika uzoefu wa tajriba za jamii ya Waswahili. Ilikuwa ni hali ya kubuni mawazo na fikira huku mshairi akielezea jambo halisi maishani kwa kulipigia msemo au mafumbo.

Ujumbe wa shairi uliweza kufumbwa katika mashairi ya jadi na ya sasa kwa kueleza mambo au mawazo kwa njia ya mkato. Mbinu hii ina sifa ya kujenga taswira katika akili ya msomaji na kupanua fikra zake katika aidha hali ya kutanabahi, kutahayari au kutafakari na mwishowe akajenga imani yake kuhusu maisha. Wazo hili linaafiki mhimili wa Udenguzi unaodai kwamba, mhakiki huzama katika ufafanuzi wa matini na kuitazama katika ufafanuzi wa matini na kuitazama kwa jicho la ndani kwa kuyadengua na kuyabomoa. Mashairi ya kimafumbo yakichanganuliwa yataweka wazi ujumbe na kuwafaidi wasomaji. Katika shairi moja la Boukheit liitwalo 'Dunia Yazongomea' anasema:

> Dunia yazongomea, ishi tushufu ghulamu
> Dunia inachakaza, ishi tashufu ghulamu
> Dunia itakwangaza, ishi tashufu ghulamu
> Dunia hutoiweza, ishi tashufu ghulamu.
> ( Msami, 1982:11)

Ubunifu mwingine wa ushairi wa Kiswahili na unaofumba ujumbe ni ule wa kutumia tamathali za usemi. Kwa mfano kulinganisha tabia za binadamu na zile za wanyama. Kwa mfano shairi la 'Simba Marara' (Boukheit, 1982: 71).

Ubunifu mwingine ulitokea katika msamiati. Kwa vile Kiswahili kina lahaja nyingi palitokea ile hali ya kutunga kwa kutumia Kipate, Kiamu, Kivumba na Kimvita. Kule kucheza na maneno ya lugha ya kawaida kuzua jambo geni kabisa kwa mfano:

> Ipotele-ipotee
> Waraka-barua
> Tabu-taabu, na kadhalika.

Ujumbe wa ushairi umefumbwa kwa sababu una lugha fichifichi. Lugha hii ya ushairi inaweza kufananishwa na ile ya madaktari. Hata hivyo, kazi ya mshairi huwa ni kupigania na kuhifadhi maslahi ya walio wengi katika jamii. Hii ndio



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

sababu kuu ya uchanganuzi huu ambao unakusudiwa kuwaelewesha wengi mashairi. Mwalimu wa ushairi anatakikana awe ameutalii sana msamiati wa lugha ya Kiswahili na vile vile awe mjuzi wa kutambua kilichofumbwa katika shairi. Tunaweza kuhitimisha sehemu hii kwa kusema kwamba, ufumbaji, ambao ni utumiaji wa tambo, ni mbinu ya kifasihi ambayo mwanafasihi huweza kuitumia, kwa hiari kutokana na mazingira yanayomkabili.

### 3.7 Sababu za kutumia mashairi ya kimafumbo

Kwa kuzingatia fikira za Abdilatif Abdalla, ni muhimu mwanafasihi aeleze mambo yale yanayomkera bila ya kukwepa au kuusema nusunusu ukweli uliopo. Mwanafasihi ana hiari ya kutoboa yote kwa waziwazi au kusema kwa mafumbo. Katika utangulizi wa kitabu cha T.S.Y. Sengo kiitwacho *Shabaan Robert: Uhakiki wa Maandishi Yake,* Abdilatif Abdalla (1975: xix) alitoa rai kuwa, ni muhimu mwanafasihi aandikapo kuhusu jambo la hatari:

> '...alifumbefumbe jambo ambalo si gumu kwa mshairi wa Kiswahili maana ni mojawapo ya kazi zake lau yu wakabiliwa na hali kama hiyo au ikiwa ni kuonyesha ufundi wake pia.'

Kutokana na dondoo hili, tunathibitishiwa kuwa, ufumbaji ni mbinu mojawapo muhimu sana katika mawasiliano ya kifasihi ukiwemo ushairi.

Zifuatazo ni baadhi ya sababu zinazowafanya watunzi wengi wa mashairi na fasihi kwa jumla kutumia lugha ya kimafumbo.

### 3.8 Ufumbaji wa kuwapinga watawala dhalimu na mfumo mbaya wa kisiasa.

Fasihi ni chombo ambacho kimekuwa kikitumiwa kuupinga udhalimu uendeshwao na watawala. Imekuwa ikitumiwa kutoa mchango katika kuutetereshа, kuutetemesha, na kuuteketeza mfumo dhalimu wa kisiasa. Fasihi yenye lengo hili, imekuwa ikiandikwa kwa tahadhari sana, yaani kwa ufumbaji. Kumekuwa na ufumbaji wa namna hii hata kabla ya karne ya ishirini, ila tutazingatia mifumo ya fasihi iliyoandikwa katika karne hii kwani mifano iliyopo ni mingi na inatosha kufafanua jambo hili. Utafiti huu utachanganua diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba.*

Nchini Tanzania nyakati za ukoloni, gazeti la mamboleo lilikuwa likichapishwa kwa idhini na udhalimu wa serikali ya kikoloni ya Waingereza. Katika gazeti hili iliwalazima wanafasihi watawaliwa yaani Waafrika, waandike mambo yasiyoikashifu serikali, au waandike kwa kufumba mkoloni.

Katika kitabu cha *Mamboleo* Nakala 1 (uk.9) mwanafasihi mmoja aliwaita wakoloni wa Kiingereza 'cha *mamboleo mapanya'.* Panya ni mnyama ambaye huuma na kupuliza. Utawala wao, Waingereza, ulikuwa wa kuuma na kupuliza. Waingereza walijaribu kuwadanganya Waafrika kuwa, utawala wao ulikuwa mzuri zaidi ya ule wa watangulizi wao, Wajerumani, ambao walitumia kiboko katika utawala. Mtawaliwa mmoja aliwajibika kuwapasha habari wenzake kwa mafumbo katika gazeti hilo kuhusu uovu wa Waingereza akisema kuwa, Waingereza ni kama

"Baa la mapanya":

Baa la mapanya
Jinsi wanavyotufanya

Ati kutukanya
Kumbe kutudanganya
Gibbe,'Ufumbaji na ufumbuaji wa mashairi',1990:2)

Katika mashairi na fasihi ya Kiswahili kwa jumla. 'panya' hutumiwa kusawiri au kuchora taswira ya unafiki au uzandiki.

S.A. Mohamed (1978:160) katika riwaya yake iitwayo *Asali Chungu*, ameyasawiri maisha hivi:

Kama panya, maisha huuma na kupuliza. Yanapouma huuuma mwanadamu; na yanapopuliza mwanadamu pia. Maumivu yake humpa mwanadamu majuto ya kuzaliwa; Mpulizo humsahaulisha kama hata wakuumbwa, sahau hujiweka kati baina ya maisha ya mwanadamu yakawa tama tupu…

Mshabihisho wa uharabu wa panya na maisha alioufanya mwanafasihi huyu unatusaidia kuelewa vizuri zaidi uharabu wa waingereza. Kutokana na Uharabu huo, mshairi S.A. Kandoro (1966) kwa mujibu wa Gibbe (1990), aliwaita wakoloni hao 'nyoka' katika shairi lake liitwalo 'Siafu wamekazana' alilomtumia ili kumweleza jinsi siafu (wananchi) walivyokuwa wanaunganika chini ya chama cha TANU, chama cha kisiasa Tanganyika miaka 1977, "dhidi ya nyoka" (mkoloni wa Kingereza). Kwa kutumia mafumbo ya kishairi aliweza kuwasiliana na mjomba wake na kumhamasisha bila ya kugunduliwa na wakoloni.

Kandoro alisema:

Nyoka amegutuka, ndani ya shimo katuna
1. Tena amekasirika, hasira zenye kununa
Nyoka anababaika, shimoni kwa kujikuna
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika

Nyoka ameshaondoka, na siafu hujazana
6. Shimoni wakipeleka, vyakula kuliliana
Ndilo walilolitaka, wale kwa kutulizana
Siafu wameungana, nyoka amekasirika
(Gibbe,1990:3)

Kwa kuwa Kaluta Amri Abedi alikuwa anajua mazingira ya kisiasa ya Waafrika, aliweza kuelewa kuwa shairi hili lilikuwa linawasema Waingereza. Kwa kuelewa kuwa Waingereza wangeizuia barua yake kwenda kwa S.A Kandoro, Abedi aliona ni heri amjibu kwa fumbo ili kuwafumba wakoloni kama wangeifungua bahasha na kuisoma. K. Amri abedi alisema:

Saadan chambilecho, cholimbecha kumenyeka
1. Kunyume ni kiambacho, chombaakini hakika
Hila tutie chekecho, chokeche kuzipinduka
Kwa wenye chongo kifika, nawe fumba lako jicho.

2. Wasione waonacho, japo mchana kutoka
Usiku wakae macho, matumbwi ya kutumbuka
Visiwafae mkocho, japo wakifilisika
Kwa wenye chongo kifika, nawe fumba lako jicho.
(Gibbe,1990:4)

Maneno chambilecho, nikiambacho na chokecho, yamegeuzwa kwa kutumia tabdili na kuwa cholembicha, chomaakini na chokeche ili kumkanganya zaidi msomaji asiyekusudiwa kuelewa ujumbe usemwao. Mawazo kama hayo ambayo yalikuwa ya kuwaasi wakoloni ilibidi yaandikwe kwa mafumbo, ili waandishi wajisalimishe.

Mapambano dhidi ya utawala dhalimu hayakukoma wakoloni (wa Kizungu) walipoondoka. Yameendelea kujitokeza hata baada ya nchi nyingi za Kiafrika kupata uhuru. Wengi waliuita uhuru huo, uhuru wa bendera. Kwa hivyo wanafasihi wanajikuta bado wana jukumu lao la kujitetea wao wenyewe na kuwasemea wasio na uwezo huo. Kwa kuwa ilibidi waseme mambo ya uchungu na makali kwa serikali tawala, ilibidi waufumbefumbe.

Mshairi aliyejifunga msombo kupambana dhidi ya madhara na madhila yaliyokuwa katika nchi ya Kenya na bara la Afrika kwa jumla ni Abdilatif Abdalla, mwandishi wa *Sauti ya Dhiki* na nduguye Ahmadi Nassir.

Ni imani ya Abdilatif Abdalla kuwa kunahitajika wimbi kali lije kuusafisha uchafu (= udhalimu) uliomo barani Afrika kama bara lenye "jipu", ambalo limejaa usaha na uchafu mwingine wa kila aina. Katika diwani yake ya *Sauti ya Dhiki* anaieleza hali hii katika shairi la 'Jipu' (uk 7):

1. Moyoni furaha sina, ningaitaka sinayo
Si usiku si mtana, ni mamoya kwangu hayo
Mateso nnayaona, yaujawa wangu moyo
Si mwako na wayowayo, uliyonifikiliya.

2. Nna jipu lituunza, linipalo tabu mno
Tangu liliponianza, kamwe sipati usono
Kwamba ni mara ya kwanza, kuugua ndwezi hino
Latoma kama sindano, utunguwe nakwambiya
(Abdala,1972)

Mshairi mwingine aliyesimama kidete dhidi ya udhalimu huo ni Euphrase Kezilahabi. Mwandishi huyu alitunga akiwa na imani kuwa, bara la Afrika bado linao ugonjwa uliokuwako wakati wa ukoloni.

Katika shairi la AFRIKA NA WATU WAKE lililomo katika diwani yake iitwayo *Kichomi* Kezilahabi anasema:

Mimi unaona mgonjwa
Bado amelala kitandani
Kama hatutamtoa kitandani
Mgonjwa hataweka miguu yake chini
Ili kutembea bila kujiegemeza.

Miiba iliyomo ndani mwetu
Pia iondolewe upesi kabla haijaingia
Kati ya mifupa na kufa pamoja nasi
Baada ya kuitoa tuvae viatu vya chuma
Halafu tucheze nao mchezo wa siasa na uchumi.

Lakini kuitoa miiba hii

Tunahitaji macho makali
Mikono isiyo tetemeka
Moyo usio na huruma
Na kuona miiba ilipoingia
(Kezilahabi,1974)

Kwa kifupi, Kezilahabi anaeleza kuwa, wadhulumiwa inawalazimu kuwa na "moyo usio na huruma" katika kushughulika na wadhalimu yaani watawala wasio na huruma kwa wananchi watesekao. Yote haya yamesemwa kwa fumbo la kishairi. Mwandishi wa *Malenga wa Vumba* hakuwa makini sana kutumia mafumbo japo aliandikia mada za kisiasa za wakati wake. Boukheit alijishughulisha zaidi na mashairi ya kawaida ya kutetea utawala na kuunganisha wananchi chini ya serikali ya KANU. Hata hivyo, katika shairi lake la 'Siwe?' anaonekana kuhamakishwa na viongozi wanaowahadaa wananchi ili wawape kura na baadaye kuwasahau:

1. Siwe ulosema jana, ya kuwa mashuhuri
Ya kuwa wajuwa sana, aidha huna kiburi
Nchini wajulikana, mwanasiasa mahiri
Bungeni tukuajiri?

Katika shairi la 'Nyama Huyu Kabaila' (UK 82-83), Boukheit analinganisha unyanyasaji kwa wananchi na mnyama mbaya anayeweza kula wanyama wengine kama vile chui bila huruma:

7: Kabaila mnyama mui, mnyama aso huruma
Muovu aula chui, si mwema katu si mwema
Huyu kwetu ni adui, shamba letu talichoma
Kiunga takichoma, nyama huyu kabaila.

Boukheit Amana analinganisha wananchi na wakulima ambao hawajaungana kumwangamiza adui ambaye ni kabila lililojiona bora zaida kuliko makabila

mengine. Kabila hilo la kibaguzi limetajwa kama mnyama mkali anayepaswa kuhamishwa kwa muungano wa makabila mengine yote.

Ahmadi Nassir hakuwahi kujishughulisha sana na mada za kisiasa. Hata hivyo, ameandika shairi liitwalo 'Kimya' ambalo linafanana sana shairi lilioandikwa na Muyaka.

Ahmadi aliandika lake katika '*Poems from Kenya*' (uk 16) anwani yake ikiwa ni 'Iwapo Kimya Si Chema':

Kimya musikidharau, tahadharini nasema
Kitayavua makuu, ya gugumo na khamasa
Kivunde wendi maguu, pasiwe wa kusimama
Iwapo kimya si chema, na maneno hayafai.
*(Poems from Kenya).*

Kimya musambe ni bure, ki mbizini kimezama
Kimya musikitotore, kwa vyembe mukakifuma
Kimya chaja zua mare, tahadharini nasema
Kimya kiwapo si chema, na maneno hayafai
*(Malenga wa Mvita)*

Miaka ya 1970, kipindi ambacho Ahmadi Nassir aliandika tungo hizi mbili kilikuwa ni kipindi cha kisa cha kisiasa nchini Kenya. Ahmadi aliamua kuwafumbia wasomaji wake wasiseme sana kwani wangejipata wakihangaishwa na serikali kama alivyofanywa ndugu yake Abdilatif Abdalla.

Aidha, aliwatahadharisha wasomaji kuwa kimya si kizuri sana kwani wataendelea kunyanyaswa. Pia, anaonekana kuwaonya watawala kupitia methali ya Kiswahili kuwa 'kimya kina mshindo mkuu'.

### 3.9 Ufumbaji wa kitasfida

Mwanafasihi hulazimika 'kuwasema' baadhi ya wanajamii, ili kuwakemea, kuwazomea na pengine kuwarekebisha. Aidha, fasihi haipaswi kupayuka, inapaswa kusoma kwa staha ili asemwaye asivunjiwe mbeleko. Mtaalamu wa mashairi, Mbega (1975), kama alivyonukuliwa na Gibbe (1990), aliwaasa watunzi wenzake kuwa inafaa kufumba, kuliko kusema kwa wazi mno:

...watu ufumba kisiri, maneno ya kusanifu
Yakazibwa kama dori, yakapambwa kinadhifu
Malenga wakatabiri, yakawazonga vipofu

...Ni aibu mshairi, kuitwa mlaanifu
Kwa ajili ya uchafu, watunzi wa mashairi

Kupayuka si jambo linalokubalika katika jamii. Gibbe (1990) akiinukuu diwani ya *Akili–Mali* ya Snow-White (1963) anasema kwamba kuna shairi moja lililoandikwa kwa fumbo ili lisiumize hisia za wanajamii waliohusika na kitendo cha kuumbua haki na kutenda mambo ya zinaa, wakiwafuga wanaume katika 'mizizi' huku wakiongea lugha yenye maneno "Mwashibota" na "Mwanabonaki":

Punguzeni uonezi, wanyonge kuwaonea
Kuwafanya kama mbuzi, mazizini kuwatia ...

Haki haifichiki, japo iwe miyaka mia
Mwenyezi Mungu wa haki, haki ataifichua
Awatenge wanafiki, haki mnyoumbua
Rabi humlipizia, mnyonge mkosa haki

Rabi atawafidhuli, haki wanayoumbua
Mwisho awakebehi, avunje wenu uluwa
Mwezi wenu nimewahi, Mungu ameniokowa
Rabi humlipizia, mnyonge mkosa haki.

Mshairi huyu alikuwa anazungumzia jambo lililohusu umalaya; haingekuwa jambo jema kulitaja wazi kabila la watu waliokuwa wakipiga umalaya, lakini mwandihi huyu alidokeza kabila hilo kwa kutaja maneno yatumikayo sana katika

kabila hilo wakati wa kusalimiana. Lugha ya kimafumbo ya namna hiyo, japo hailitaji jina la kabila hilo waziwazi, ina faida moja kubwa, inakwepa kuliumbua kabila zima kwa ajili ya malaya hao wachache.

Kulitaja waziwazi kabila hilo, kungeleta msisimko wa kikabila, na pengine mtetemeko au mtengano wa kitaifa.

K. Amri Abedi (1957: 74) katika diwani yake ya *Sheria za kutunga mashairi na Diwani ya Amri* kuna mistari isemayo:

> Simpendi mrukia, mwenda akirukaruka
> Leo anaye Asia, Kesho bibiye Rebeka …

Katika mistari hii, fikira nzito za kupigana na ukware zinajitokeza; pamoja na fikira hizo, kuna fumbo kuwa katika swala la mapenzi inafaa kuzingatia dini yako. Asia ni mwanamke wa Kiislamu, ambapo Rebeka ni mwanamke wa wa Kikristu – vijana wanaelezwa kuwa si vizuri warukeruke, leo kwa kuyu kesho kwa yule, pia si vizuri warukie wasichana wa dini tofauti.

Mambo haya yalisemwa kimafumbo, kwani kama yangesemwa moja kwa moja, tungepata fikira kuwa K. Amri Abedi alikuwa na upendeleo wa dini fulani na chuki kwa dini nyingine. Kama angetaja waziwazi na kuonyesha upande au upendeleo wa dini moja, angezua fikira za ubaguzi wa kidini.

Lugha ya kimafumbo ina mvuto wake. Kwa kawaida, mtu kumkasirikia kwa ghafla, pia hawezi kuzitonesha hisia zake mara moja. Ni rahisi kukuvumilia ukimtukana au ukimwambia habari nzito kwa umafumbo. Jambo alilokuwa akiambiwa S.A Kandoro lilikuwa nzito: alitakiwa ayaache madhehebu yake ya Suni na kuingia katika madhehebu ya Ahmadiya.

Saadan .A. Kandoro (1966:25) alisema:

...Najua umeugua, ndwele zakupa madhila
Zakutia sislisia, kicho wazicha shakala
Kula waona udhia, jitamu hutaki kula
Dawa mziwanda kula, kula upate afia...

...Dawa chungu viinajua, huitamani kuila
Maradhi sike kuna, pasipokuwa muhula
Uchungu wa kukuzaa, utanifunika shela
Dawa mziwanda kula, kula upate afia.

Fumbo jingine kuhusiana na dini ni lile lililotungwa na K. Amri Abedi (1957:60-61). Shairi hilo lilitungwa na kutumwa kwa S.A. Kandoro na liliitwa "Dawa mziwanda kula, kula upate afia'. Kandoro alijibu kwa fumbo pia katika shairi akisema:

1. Sili ingawa ni dawa, sili nisichotamani
Japo shuruti ikiwa, hakiukipi afueni
Kwa kweli haitokuwa, tiba haiwezekani
Sili nisichotamani, sili ingawa ni dawa.

2. Sili au sintolishwa, nikaacho kataani
Kataani sintolishwa, ila kwa hemima ndani
Jibu lililopitishwa, nduguyo silitamani
Sili nisichotamani, sili ingawa ni dawa.

Lugha iliyotumika na washairi hawa wawili ina utauria au utasfida ndani yake-imejaa sitara ndani yake. Lugha hii inawaacha wahusika wote katika hali ya kuheshimu dini zao, kila mmoja akiiheshimu dini ya mwenzake.

Nyimbo za Taarab huweza kutumia mafumbo ili kumtaja "mpenzi". Katika baadhi ya nyimbo hizo, "mpenzi" huyo hutajwa kwa kutumia herufi ya kwanza ya jina lake. Kwa mfano, kama anaitwa Fatuma, katika wimbo atatajwa kama F; kama jina lake ni Rehema, basi ataitwa R. kuficha jina namna hii kwa kutumia herufi ya mwanzo tu hutokea kwa sababu mapenzi ni siri ya wawili tu, si kitu cha kutangazwa kwa kila mtu.

Katika wimbo mmoja, mtunzi analia kama ifuatavyo katika moja ya beti zake. Knappert (1972) akinukuliwa na Gibbe, (1990) alisema:

Moyo naona thakili, mwili sina tena damu
Usiku kucha silali, hukuwaza maudhamu
Njoo ala kuli hali, wewe ndiwe dawa tamu

Mkarara

Nakupenda kwa haki
Ewe harufu ya mimu
(Herufi ya mimu = herufi ya M).

Katika jadi ya Kiswahili; mapenzi si kitu cha kuanika na kukikansha hadharani, bali ni tunda tamu la kula umeficha. Kwa hivyo, ni jambo la kutia aibu kumwimbia wimbo mpenzi kwa kumtaja waziwazi na kumwimba katika hadhara kwa jina lifahamikalo. Kumtaja mpenzi kwa jina kungemkata maini mhusika, kungeitia aibu aila au ukoo wa mpenzi huyo, kungeistua jamii nzima, kungetoa picha mbaya ya mtunzi na pengine kungesababisha kuvunjika kwa mapenzi ya hao wawili wapendanao.

Katika shairi la 'Nyonda' (uk. 148) Ahmadi Nassir amefumba masuala ya mapenzi kwa msamiati usio wa kawaida anaposema:

6. Yomi bui, mwenziyo nimedangana
Hunijui, moyoni ninavyoona
Sinwi shai, nisikutaje kwa jina

7. Yomi toba, mwenziyo ni taabani
Kwa mahaba, yalinovaa moyoni
Hunikaba, wala utungu sioni
(*Malenga wa Mvita*,Uk 148)

Mshairi anamweleza mpenzi wake jinsi alivyo na mapenzi (nyonda) asiyoweza kuvumilia bila kuwa naye. Mshairi amefumba ujumbe wake kwa msamiati mzito kama vile nyonda, yomi na shai.

Kwa hivyo, mshikamano wa kijamii husababisha ufumbaji katika fasihi kukiuka miiko hiyo ya kijamii kungestua jamii na kuifanya fasihi hiyo ionekane kama imetungwa kwa ajili ya wendawazimu. Njia ya kukwepa hukumu kama hiyo ni kutunga kwa mafumbo.

### 3.10 Ufumbaji kwa kucheza na lugha

Mshairi kwa kawaida ni mtu anayeifahamu fika lugha aitumiayo kwa hiyo anaweza kucheza nayo ili imtumikie kama apendavyo. Kwa kawaida, mchezo huo wa maneno huwa si mchezo tu, bali huwa ni kazi ya kisanaa yenye maana.

Mchezo huu hufanywa kwa matumizi ya neno lililo na maana nyingi au urudiaji wa neno lile lile ili kusisitiza maana fulani.

Vile vile, muundo wa neno hubadilishwa ili kufumba habari fulani. Kwa mfano K.A Abedi akizungumza na S.A Kandoro alisema:

Saadani chambilecho, cholembicha kumenyeka
Kinyume nikiambacho, chombaakini hakika
Hila tutie chekecho, chokeche kuzipunduka
Kwa wenye chongo kifika, nawe fumba lako jicho.

Maneno chambilecho limekuwa cholembicha; nikiambacho likawa chombaakini; na chokecho likwa chokeche. Mchezo huu wa maneno ambao unatokana na uhuru wa kishairi (idhini ya kishairi) ni tabdili na umeficha maana nzito na maudhui makali yapiganayo na ukoloni.

Ali Athmani ((Ali Koti), 1776-1834) aliwahi kutunga shairi liitwalo 'Mzigo'. Inasemekana kwamba alitunga shairi hili kwa kuwacheza shere jamaa zake. Shairi hili lilipelekwa pamoja na mzigo wa mtama. Watu wa Pate wakati huo walikuwa wamepata tisho la vita kutoka kwa wenzao kutoka Siu na hivyo, hawakulima mwaka huo. Watu wa Siu walipovuna waliwapelekea mzigo wa mtama kisimani walipoenda kuteka maji. Ali Koti alisema:

2. Yambo iwi yeo pako, nla chakula ukute
Wenende kwa wenye mbeko, ukawalimbushe tete
Uwaonye limo lako, wawate kumiza mate
Ela muyini sipite, wawatie kisimani.

3. Wanao mfuwatane, mzigo uutongate
Kauweke uuone, khabari zote wapate
Uwambiya awanyani, kwa kila mtu apate
Ila muyini sipite, wawatiye kisimani.
(*Malenga wa Karne Moja,* Uk 31-32)

Aina nyingine ya kucheza na lugha inahusisha maneno yenye uhomonemia; maelezo ya neno kwa maana nyingi zisizohusiana. Shairi la Ali Koti 'Kaa' lililo katika diwani ya *Malenga wa Karne moja* anasema:

1. Kaa la moto ni kaa, liwakalo likazima
Kaa lamnazi kaa, litendalo zimazima
Kaa upumue kaa, utuze wako mtima
Kaa! Umenisukuma! Nami sikutaki tena
(uk 33)

Shairi lingine la Ali Koti ni la 'Paa' ambalo alilitunga kwa bahari ya Zivindo. Shairi hili alitunga wakati alipotamkiwa neno paa na Sheikh Mohamed naye kwa uhodari wake akalitungia shairi papo kwa papo kuonyesha maana zake mbalimbali:

Paa, kipungu mpaazi, upaae usotua
Paa, ni ya wake mbazi, wapikao na kwepua
Paa, vimbate mkwezi, lisije kushuka vua
Paa! Nimeitena! Usikizeni mshindo.
(*Malenga wa Karne Moja*, Uk. 33)

Mtungaji ameeleza maana nne za neno *paa.*

Shairi la Muyaka 'OA' lililo katika *Diwani ya Muyaka* iliyohaririwa na Hichens (1940:73) ni mfano mzuri wa shairi la kihomonemia:

Oa, ndiwe muokezi, uzoeleo kuoa
Oa, sifumbe maozi, maninga uchiyavua

Oa, uzaze uzaai, kama ulivyozaliwa
Oa, sizi ndizi ndoa, aso kuoa ni yupi?

Mchezo wa maneno yenye uhomonemia una faida kubwa ya kufundisha maana mbalimbali za neno. Kutokana na shairi hili neno 'Oa' lina maana saws na 'oga' katika mstari wa kwanza; lina maana ya 'ola' au tazama katika mstari wa pili; lina maana ya 'kuoa mke' katika mstari wa tatu.

Abdullaziz (1979:98) aliweza kuonyesha mifano kadha ya mashairi ya homonemia kutokana na mashairi ya Muyaka.

Mshairi mwingine ambaye ameweza kuandiika mashairi ya Kihomonemia ni Ahmadi Nassir (1971:55). Kwa kutumia mchezo huu ameweza kuhifadhi maana mbalimbali za maneno, mathalan:

9. Isha ni jina la kwetu, kwa kiumbe mwanamke
Isha huambiwa mtu, kuwa maliza = wondoke
Isha nne rakaatu, ni ya swala ikumbuke
Mwenye yane natamke, hiyo ndiyo isha gain?

10. Kaa ni kusema kama, na muwaliko ni kaa
Kaa ni alosimama, wamuweleza kukaa
Kaa ni lililozima, na lenye moto ni kaa
Mwenye ya tano afaa, anene ni kaa gani?
(*Malenga wa Mvita*,Uk.55)

Katika shairi la 'Tunda Tunda' (uk 26) Boukheit ameonyesha uhodari wa hali ya juu kwa kuchukua neno moja katika kila ubeti na kulipa maana tatu zenye maana mbalimbali. Kwa mfano:

Kijana tuza makini, nikwambie usikile
Chakula mahotelini, si kizuri usikile
Ufikapo mlangoni, kizingiti usikile
(*Malenga wa Vumba*)

Tukichunguza kwa makini katika ubeti huu tutaona kuwa 'usikile' ya mshororo wa kwanza na 'usikile' ya mshororo wa pili zina maana mbalimbali. Kadhalika na hiyo

'usikile' iliyopo katika mshororo wa tatu, pia nayo ina maana yake mbali iliyo tofauti kabisa na hizo 'usikile' mbili, zilizo katika utao wa mwanzo na mloto.

Katika mashairi haya washairi walikusudia kuupanua ujuzi wa lugha hasa kwa wanafunzi wa somo la fasihi waweze kujuwa jinsi msamiati mmoja unavyoweza kupinduliwa kutoka maana ile hadi ile.

Tunaweza kuhitimisha sehemu hii kwa kusoma kuwa "Kucheza na lugha" ni mbinu ya kisanaa ambayo inaweza kutumika kuficha maudhui mazito kama mifano yetu inavyoonyesha.

## 3.11 Kiishilio

Sura hii imeshughulikia namna lugha ya kimafumbo ilivyotumika katika utunzi wa ushairi. Lengo kuu la sehemu hii lilikuwa kubainisha vipengele vya lugha vilivyofumba ujumbe wa Ahmadi Nassir na Boukheit Amana. Vile vile, sura hii ilijadili kwa kifupi uhusiano kati ya fasihi na jamii, hususan jinsi fasihi ilivyoathiri maisha ya kila siku ya mwanadamu.

Kila utanzu wa fasihi andishi una sifa zake zinazoubainisha na vile vile kuutofautisha na tanzu nyingine. Miongoni mwa sifa za ushairi zinazoubainisha na tanzu nyingine kama vile tamthilia, riwaya na hadithi fupi ni arudhi ya ushairi na idhini au uhuru wa mshairi. Arudhi ya ushairi ilishughulikiwa kama ilivyopendekezwa na K. Amri Abedi (1954). Abedi alidai kwamba sharti utunzi wa mashairi uzingatie idadi maalumu ya mizani, mishororo iwiane katika kila ubeti na vile vile kuwe na uwiano wa vina.

Idhini au uhuru wa mshairi ambao uhusisha mazida, inkisari na tabdili huchangia kuufumba ujumbe au maana ya mwandishi. Msomaji au msikilizaji wa mashairi

anayefahamu fika matumizi ya uhuru wa mshairi, ndiye atayeweza kuufumbua ujumbe wa mwandishi kwa urahisi. Aidha, Ahmadi na Boukheit walitumia lugha ya kitamathali na msamiati usio wa kawaida kama vile wa kikale, kiarabu na kilahaja kufumba mashairi yao.

Sehemu hii vile vile ilijadili sababu kadha zilizopelekea watunzi wa *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba* kufumba mashairi yao. Sababu hizo ni pamoja na kuwafumba watawala dhalimu na mifumo ya kisiasa inayowanyanyasa watawaliwa, ufumbaji wa kitasfida au kuficha makali ya lugha na ufumbaji wa kucheza na lugha.

Sura inayofuata imeshughulikia ufumbuaji wa mashairi ya *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba* kwa kuzingatia mada za unyumba/ baina ya mume na mke, lugha na majonzi na makiwa.

# SURA YA NNE

## Ufumbuaji wa mashairi katika diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*

### 4.0 Utangulizi

Sura hii imechanganua mashairi ya kimafumbo katika diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*. Lengo kuu katika sura hii limekuwa kubainisha kwamba mashairi yanaweza kufumbuliwa au kuchanganuliwa na kuweka wazi ujumbe wa mshairi. Lengo la pili la sura hii limekuwa kudhihirisha kwamba mfasiri wa shairi la kimafumbo anaweza kupata zaidi ya maana moja kutokana na shairi lilo hilo. Kuchunguzwa kwa mashairi ya kimafumbo katika diwani hizi kumewezesha kubainisha jinsi Ahmadi Nassir na Boukheit Amana walivyotumia mashairi ya kimafumbo kuwasilisha maudhui yao kwa wasomaji na wasikilizaji. Mada zilizozingatiwa katika utafiti huu ni pamoja na unyumba (uhusiano baina ya mume na mke), matumizi ya lugha na masaibu/maliwazo.

Mashairi ya Kiswahili ni mojawapo ya njia za mawasiliano. Hivyo, ujumbe uliomo katika shairi lazima ufasiriwa kwa kuzingatia muktadha ili umfaidi msomaji. Hata hivyo, wasanii wengi hufumba ujumbe wao katika matumizi ya lugha ya kitamathali. Tamathali wazitumiazo watunzi wengi ni pamoja na tashbihi, sitiari na taashira (Nyanchama 2004).

Aidha, watunzi hutumia msamiati usio wa kawaida. Kwa mfano watunzi hutumia msamiati wa kikale, wa kilahaja na wa lugha za kigeni kama vile Kiarabu. Msamiati wa aina hii huchangia katika ufumbaji wa mashairi.

Katika diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba* kuna mashairi ya aina mbili: yaliyo na ujumbe ulio wazi pamoja na yale yaliyofumba ujumbe wa mtunzi. Kwa hivyo, kuna mashairi ya kawaida na mashairi ya kimafumbo. Mashairi haya ya kimafumbo pia hujulikana kama mashairi mazito.

Kaluta Amri Abedi anasema:

> Unapotaka kutunga shairi zito kwa fikira, tumia lugha ya kizamani, lugha iliyotumiwa na wazee katika mazungumzo, tumia methali ziwe kituo, na huko na huko dokeza mafumbo (1954:23).

Aidha, Said A. Mohamed anasema:

> Lugha katika msingi wa matumizi yake mbalimbali, ndiyo msingi mkubwa wa kutenganisha nathari na ushairi. Ushairi una mwelekeo wa lugha ya sauti zilizotengwa kusudi kunasa sikio la nje na sikio la akili. Ushairi hunasibika na mpangilio adimu wa maneno, midundo, teuzi za tamathali, na ujumbe wa picha na ufupisho kwa matumizi ya taswira na picha; ufupisho wa wazo, dhana au jambo pana na refu katika ufinyu wa maneno yanayonata sanaa. (1984: v)

Ahmadi Nassir na Boukheit Amana ni mifano ya washairi waliozingatia mawazo haya ya S.A Mohamed katika kuwakilisha mawazo, fikira na falsafa yao kwa wasomaji.

Wakichanganua maana ya shairi, Njogu na Chimera wanasema:

> "Mwandishi aandikapo, huwa mwanzo ana mawazo fulani yaliyomkabili, au kile S.A.Mohamed alichokiita 'kariha'. Mawazo haya hujibainisha yanapoelekezwa kwenye dhamira iliyokusudiwa". (1999:110)

Njogu na Chimera wanasema, tunapozungumzia kuhusu maana katika ushairi, hatuna budi kutazama:

i) Lengo la mwandishi,

ii) Umbo la utungo na aina yake,

iii) Namna mawazo yalivyowasilishwa na

iv) Namna lugha ilivyotumiwa kusheheni mawazo hayo.

Utafiti huu umezingatia baadhi ya maoni ya Njogu na Chimera katika ufumbuaji wa ujumbe wa mashairi ya kimafumbo katika diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba.*

Mtunzi wa mashairi hujaribu awezavyo kufikia kilele cha lugha kwa kuifinyanga na kuutafakari ukwasi wake ili shairi lake linoge. Kwa hivyo, inamjuzu mhakiki aitafakari lugha, sio tu kama chombo cha fasihi, bali pia kama chombo kinachosheheni maana.

Kwa mujibu wa Kezilahabi; (1974: xiii), mashairi ya zamani yalikuwa yakiweka mkazo zaidi kwenye mafumbo, hivi kwamba ulelewekaji wa shairi ulikuwa uwezo wa kufumbua fumbo. Kwa sababu hii, ushairi wa Kiswahili ulikuwa, kwa muda mrefu, ni mazungumzo baina ya wasanii wachache tu. Ndipo akaona kuwa ipo haja ya kuteremka chini na kuwapa nafasi watu wa kawaida ili wafaidi utamu wa ushairi.

Lengo kuu la utafiti huu ni kutoa mwongozo wa uchanganuzi wa mashairi ya kimafumbo ili kuwawezesha wasomaji wote kufaidi utamu wa ushairi kwa kupata ujumbe wa waandishi.

Ili ujumbe wa shairi uweze kudhihirishwa, inabidi lugha ya kitamathali pamoja na msamiati usio wa kawaida zifafanuliwe. Ufasiri wa tamathali na msamiati lazima ufanyiwe kwa kuzingatia muktadha wa utamaduni kwa kuwa lugha inapatikana katika utamaduni; ni kipenyo cha utamaduni, na ni sehemu ya utamaduni ( Nyanchama, 2004:131).

Jambo hili limepelekea wataalamu wengi kutoa kauli kwamba lugha na utamaduni ni mambo yasiyoweza kutenganishwa.

King'ei na Amata wanasema:

"...ushairi ni sehemu mojawapo ya lugha na utamaduni wa jamii. Kwa sababu hii ni vigumu kuelewa ushairi wa jamii fulani bila kuifahamu lugha na utamaduni wao."(2001:4).

Kutokana na maelezo haya, ni dhahiri kwamba kuelewa lugha na utamaduni wa jamii fulani ndio ufunguo wa kuuelewa ujumbe wa mashairi ya kimafumbo ya jamii iliyosawiriwa na mtunzi wa mashairi.

## 4.1 Jinsi ya kufumbua mashairi

Kwa mujibu wa A.G. Gibbe (1990:12), mashairi ya kimafumbo yanaweza kufafanuliwa ikiwa mfafanuzi ataweza kuwa mvumilivu, mwenye akili pevu au mtulivu na asiye na papara. Kulingana na mchanganuzi huyu, kuna njia nyingi zinazoweza kutumika kulifumbua shairi la Kiswahili. Hata hivyo, njia muhimu ni mbili: ya kwanza ni kuongea na mtunzi mwenyewe; na ya pili ni kutafuta vidokezi muhimu katika kazi yenyewe ya fasihi.

Utafiti huu umezingatia mbinu ya kuchunguza vidokezi vilivyopo katika shairi maalumu pamoja na kuelewa siyaki ya mtunzi.

Katika baadhi ya kazi za sanaa, huwa kuna vidokezo vinavyoweza kumsaidia mtafiti kugundua ufumbaji uliopo. Mfano mzuri ni shairi liitwalo 'MAMBA' katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* iliyotungwa na Abdilatif Abdalla:

1. Nami nambe, niwe kama waambao
   Niupambe, upendeze wasomao
   Niufumbe wafumbuwe wawezao

2. Kuna mamba, mtoni metakabari
   Ajigamba, na kujiona hodari
   Yuwaamba, kwamba 'taishi dahari

(Uk.10)

Shairi hili lina vidokezi vingi vinavyoonyesha kwamba lenyewe ni fumbo. Kwa mfano, katika ubeti wa kwanza, tunapata neno "niufumbe", yaani lengo la

mwandishi ni kutunga utungo wenye fumbo. Kuelewa siyaki ya mtunzi, yaani mazingira ya mtunzi wakati wa kuandika, husaidia sana katika kupata ufafanuzi sahihi wa fumbo. Kwa mfano, kwa kuwa diwani ya *Sauti ya Dhiki* iliandikwa kutokana na siyaki ya vuguvugu la kisiasa nchini Kenya, basi inatarajiwa kuwa kila shairi katika diwani hiyo, ili kulifumbua ni wajibu wa mfasiri kulihusisha na siasa (ya Kenya).

## 4.2 Maudhui ya unyumba/ baina ya mke na mume

Sehemu hii imechanganua mashairi yanayohusu unyumba au uhusiano wa mke na mume katika diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*. Utafiti huu umechanganua mashairi yanayohusu uhusiano wa kinyumbani ambao ni msingi wa jamii. Uhistoria mpya unadai kwamba matakwa ya kijamii na kisiasa huathiri utoaji na upokezi wa kazi za kifasihi (Greenblatt, 1980).

Mashairi yaliyochanganuliwa katika sehemu hii ni pamoja na 'Oa' (uk. 158) na 'Nenda na bahati yangu' (Uk. 160), kutoka diwani ya *Malenga wa Mvita*; na 'Mpende akupendae' (Uk. 91) na 'Leo homa' (uk. 93), kutoka diwani ya *Malenga wa Vumba*.

## 4.3 Owa

Shairi hili limefanana na shairi lenye jina kama hilo katika nudhuma au tungo za Bwana Muyaka.

Hili ni shairi la beti kumi na mbili na linaweza kuitwa la aina ya tarbia. Hii ni kwa sababu kila ubeti una mishororo minne. Shairi hili lina neno 'owa' ambalo

limerudiwarudiwa mwanzoni mwa mishororo yote na hivyo ni shairi la bahari ya kikwamba.

Neno 'owa' lina maana ya oa au kuoa ikiwa na maana ya kupata mke. Umuhimu wa shairi hili ni kwamba linaangazia maswala ya ndoa au ya kifamilia. Kitamaduni familia nzuri kwa Waswahili na Afrika ndiyo msingi wa jamii dhabiti.

Kilichofumba ujumbe wa shairi hili ni msamiati wa kikale, wa kilahaja pamoja na ule wa kigeni kama vile wa Kiarabu. Kwa mfano neno "mafuja" (maovu au matata); "kuzangaliya" (kuziangalia); "uyuwe" (ujuwe); "simnakisi" (usimtie kasoro); na "mutaanasi" (mustarehe), si ya kawaida. Hivyo, yanakuwa magumu kueleza.

Kila mfasiri wa shairi hili atalazimika kupitia msamiati, kuuchunguza kwa makini pamoja na kudadisi jinsi ujumbe unavyotiririka ubeti baada ya mwingine hadi kufika mwisho wa shairi.

Shairi hili linazungumzia mke mwema na mrembo kama anavyodokeza mshairi:

11. Owa chenye asimini, kikuba cha asiliya
Owa kila na rihani, na waridi, aridhiya
Owa kilicho na shani, na manukato kutiya
Owa uyuwe duniya, mupendane na mkeyo

Katika shairi hili, Ahmadi anamhimiza rafiki yake ambaye alitaka kuoa, kwamba aoe na ajaliwe mke wa imani, baraka, utulivu, uzima na kadhalika. Tunapata kujua ujumbe wake kutokana na neno lililotumika kama mada ya shairi hili. Hata hivyo, shairi hili linaweza kupata maana na dhamira nyingine na hivyo, kuakisi mhimili wa udenguzi unaodai kwamba ufasiri wa maana ya matini hauwezi kufika mwisho na kuwatosheleza wafasiri wote.

Kila wakati matini isomwapo, maana mpya hupatikana ambayo haiwezi kuitwa maana ya mwisho. Kuhusu uchanganuzi wa maana katika beti mbalimbali tunaakisi mhimili wa udenguzi uliodai kwamba matini inapaswa kupasuliwa katika viambajengo vyake ili kudondoa maana. Kwa mfano katika ubeti wa kwanza mwandishi anasema:

> Owa sandame hadaa, moyo ukahadaiwa
> Owa, anayekufaa, mke mwenye kusifiwa
> Owa upate kuzaa, kama ulivyozaliwa
> Owa ukijaaliwa, mupendane na mkeyo.

Ubeti huu unapendekeza msomaji aoe mke mwema na kwamba wapate kuzaa na kupendana. Hii ni maana ya ubeti mmoja tu. Utafiti huu unapendekeza uchanganuzi wa matini nzima na kujenga maana kamili. Mtunzi huyu anaendelea kusema hivi:

> 4. Owa siowe tambara, linukiyalo vibaya
> Owa mwanamke jura, umfunze yenye ndiya
> Owa usiowe sura, kutaka kuzangaliya
> Owa mzuri tabiya, mupendane na mkeyo.

Katika ubeti huu Ahmadi anamkanya msomaji dhidi ya kuoa mke aliyewahi kuwa kiruka njia au aliyewahi kuwa na tabia isiyokubalika katika jamii huku akikimbilia warembo. Ujumbe huu unadokezwa na matumizi ya neno 'tambara', likiwa na maana ya nguo iliyoraruka baada ya kutumiwa sana. Hii ni sitiari iliyo na maana ya mwanamke aliyejihusisha na wanaume wengi au aliyeshiriki katika mapenzi ya kiholela. Mshairi huyu anasema:

> 12. Owa utukuze cheo, na jina lipate kuwa
> Owa upate mkeo, aambiwe meolewa
> Owa kama wauwao,moyo usiliye ngowa
> Owa ujuwe kukuwa, mupendane na mkeyo.

Ubeti huu unazua maana nyingine ya kuwa msomaji akioa atatambuliwa katika jamii na kutukuza cheo chake katika jamii. Iwapo hataoa, basi, hatapata wa kumtambua. Ujumbe huu unadokezwa katika mshororo wa kwanza wa ubeti huu.

Maana zote zikiwekwa pamoja ndipo maana au dhamira ya mtunzi itaweza kujulikana. Mtunzi ana maana ya kuwa lazima kila mwanamume katika jamii apate mke ili aheshimike katika jamii. Aidha, Ahmadi anaonekana kutilia nguvu nafasi ya dini katika ndoa. Vile vile, Ahmadi anasisitiza kuwa ndoa nzuri au mke mwema ndiye msingi wa jamii nzuri.

### 4.4 Nenda na bahati yangu

Shairi hili linazungumzia mhusika aliyefunga safari ya kwenda huku akimwacha mwenzake katika hali ya upweke na isiyo nzuri na isiyotamanika. Haya yanadokezwa na mada. Mada hii ni tata na inayoelekea kulipa shairi maana tofauti tofauti. Mada pamoja na msamiati uliotumika unafumba ujumbe au maana ya mwandishi.

Udenguzi unashikilia kuwa kinamchosaidia msomaji au mfasiri katika fasihi ni kuielewa maana na uwezo wake wa kutofautisha kati ya neno na kisichomaanishwa na neno hilo. Huu ni mhimili unaosisitiza kuwa daima kuna mvutano wa "kuwepo na kutokuwepo". Mada ya 'Kwenda na bahati yangu' kunaweza kuwa na maana nyingi. Hili ni shairi la beti nne pekee lakini ni fumbo kwa sababu ya mada pamoja na msamiati uliotumiwa na mwandishi kuuficha ujumbe wake.

Katika uchanganuzi wa mtiririko wa maana tunapata:

1. Mosi naanza awali, kwa salamu nyingi mno
Pili nakujuza hali, ni mzima sina neno
Tatu naona thakili, kupunguwa maonano
La'ne sipate usono, nenda na bahati yangu.

6. Tano hakika ya moyo, haikomi kukuwaza
Sita ni yanipatayo, sina wa kumueleza
Saba sikomi kiliyo, moyoni ningajikaza
Nane sina mliwaza, nenda na bahati yangu.

Ujumbe unaopatikana kati beti hizi ni kama wa tungo ziitwazo taabili au ambazo ni mashairi mafupi na ya kirasimi au kisherehe yanayotungwa kwa ajili ya kitu au mtu fulani. Taabili inaweza kuwa utungo ambao unatafakari maswali fulani kama mapenzi au kifo (Wamitila, 2003:206).

Kifo kinaashiriwa kwa neno 'kiliyo' katika mshororo wa tatu wa ubeti wa pili. Ni desturi katika utamaduni wa Kiafrika kuachwa na kilio cha siku nyingi kumkosa au kumwomboleza mume au mke katika familia kwa aliyefiwa.

Hata hivyo, tunapata maana tofauti katika ubeti wa tatu:

3. Yote niliyoyanena, kwa hisabu hakwambiya
Ndiyo yanilayo sana, na mawazo kunitiya
Tisa naliliya jina, kwa bahati kuwa mbaya
Kumi sina pa kungiya, nenda na bahati yangu.

Mshairi anaweza kuwa na maana ya kutengana na mke wake na wote kuishi kando kando.Kile anachoonekana kulilia ni kwamba hadhi ya jina au labda cheo chake kimetiwa doa kwa sababu ya kutengana na mkewe au mumewe. Inaonekana pia kwamba mshairi alipoachwa hakuachiwa wa kuishi au hata wa kueleza masaibu yake.

Neno 'bahati' linaweza kuwa na maana ya riziki ambayo mshairi aliweza kunyang'anywa na mwenzake. Huenda bahati yenyewe ikawa ni cheo, pesa, watoto au kitu kingine cha thamani kwa mshairi na mwenzake.

### 4.5 Wajao na kwenda

Fumbo la kinjama ni uhusiano anaouhisi msomaji kati yake na kazi. Kazi hii huwa ngumu na inamlazimisha muda na wakati ili kuweza kuielewa (Wamitila 2003: 51).

Shairi la wajao na kwenda haliwezi kueleweka moja kwa moja na hivyo, linaweza kuwekwa katika kundi hili la mashairi ya kimafumbo. Hili ni shairi ambalo linaangazia maisha ya duniani ambayo huonekana kama safari ya kuwasili duniani, kuondoka na kwenda kwingineko. Hili linadokezwa na mada ya shairi. Boukheit ametumia msamiati unaohitaji uchanganuzi ili kupata maana kamili ya shairi lenyewe. Kwa mfano:

4. Hupanda juu angani, kimawazo na hisia
Munganiona ni chini, ni mwili ulosalia
Mwenyewe ni qamarini, naitumbuza dunia
Viumbe kiwaangalia, huwa wakija na kwenda.

Mwandishi ametumia maneno 'qamarini' lilikuwa na maana ya mwezini na 'naitumbuza' lilikuwa na maana ya kuitazama dunia. 'Kupanda juu angani kimawazo na kihisia' ni lugha ya kipicha inayoonyesha mtu aliye na uwezo wa kuona mengi yanayofanyika duniani. Msamiati huu na kipicha inayoonyeshwa na ubeti wa kwanza unamlazimu msomaji kwenda kwa beti nyingine za shairi ili kupata ujumbe kamili pamoja na dhamira mtunzi.

3. Kila mwaka huchanuwa, na la kunivutia
Mauwa yalomwaiwa, marashi ya kunukia
Harufu kipiga pua, wazimu huniingia
Hatamani kuyagwia, haya yajayo na kwenda

Ubeti huu unaleta dhana au maana tofauti na ya ubeti wa kwanza uliowaangazia watu wote na kuangazia wanawake ambao hurejelewa kwa matumizi ya maneno kama 'maua'. Neno 'au' katika mshororo wa kwanza huonyesha kwamba wanawake wazuri na warembo huja na kutoweka kama afanyavyo au yanyaukavyo maua. Ubeti huu unadokeza maisha mafupi na mazuri ya mwanadamu.

Ubeti huu unaweza pia kupata maana nyingine ya raha na anasa za ulimwengu ambazo huwapumbaza walimwengu. Shairi hili linaweza kuonyesha ugumu wa kupata mke mwema. Kwa mfano mshairi anasema:

6. Meona wengi warembo, mbeleni walokingia
Walikipigana kumbo, kujipara kiwania
Lakini tabia kombo, zao halizichukia
Ndipo kawachilia, walokuja wakenda

8. Lakini 'itaomba mungu, aloiumba dunia
Nami anelee wangu, nitkejivuni
Wangu atokuwa wangu, siyo wangu wa udhia
Mtuvu wa kusikia, kati wajao na kwenda.

Mwandishi anasema kwamba wanawake ni wengi dunia lakini tabia za wale wengi ni 'kombo' au hasi na kwamba haziwezi kuitwa za mke mwema kama aliyetoka kwa Mungu.

Mada na msatiati wa shairi hili ndiyo yamechangia katika kufumba ujumbe wa mshairi na hivyo, kumfanya mfasiri kupata maana kadha kando na maana muhimu inayofungamana na muktadha wa unyumba au ndoa.

### 4.6 Leo homa!

Hatua ya kwanza ya kufasili shairi hili ni kujua maana ya mada. Homa ni ugonjwa wa ghafla unaompata mtu kwa sababu ya baridi au magonjwa mengine kama vile malaria. Homa ni ugonjwa hatari. Katika shairi hili mwandishi anaashiria kwamba yaliyompata ni ya ghafla na kwamba ni kama homa. Homa humkosesha mtu raha, hivyo mada ya shairi hili imetupa taswira ya mhusika mgonjwa na asiye na raha.

Msamiati unaotumika na mwandishi vile vile si wa kawaida na hivyo, unafumba ujumbe wa mwandishi jambo linalomlazimu mfasiri kuwa mwangalifu na kumlazimu kulisoma shairi lote ili kupata ujumbe wa mwandishi. Kwa mfano:

1. Kunigeuka ghafla, mwana menitia homa
   Kinyume cha Jamala, kunidhania si vyema
   Leo nashindwa na kula, kisa moyo waniuma.
   (*Malenga wa Vumba*)

Maneno 'kinyume cha "jamala" yanatoa maana ya kinyume cha tabia yako. 'Moyo waniuma' ni mbinu ya tashihisi iliyo na maana ya kufadhaika au kukosa utulivu moyoni. Msamiati wa kikale uliotumiwa katika ubeti wa mwisho pia unachangia kufumba ujumbe kwa wasomaji. Kwa mfano:

7. Nakusihi ishe kondo, mikono naweka
   Mwana liondowe fundo, na moyo kutakasika
   Uekewe penys pendo, shida kukosa dhihaka
   (*Malenga wa Vumba*)

Neno "kondo" lina maana ya vita. Neno "fundo" nalo linamaanisha hasira zilizofichwa moyoni. Mwandishi katika ubeti huu anaomba msamaha kwa mpenzi

wake na kuomba kwamba warundiane na wawe na upendo kama ilivyokuwa zamani.

Mwandishi alikuwa na dhamira mbili: Kwanza, anaweza kuwa anawaonyesha waliooa kuwa familia hazikosi matatizo na kwamba waja wanapaswa kuwa na unyenyekevu na kukuza uelewano.

Pili, shairi hili linaweza kuwa la kuwasuta wapenzi ambao huwageuka wenzao ghafla na kutatiza mshikamano wa kijamaa.

Maana zote mbili zinakubalika kwa mujibu wa mhimili wa udenguzi unaodai kwamba mfasiri wa kifasihi anaweza kupata maana mbili za matini moja zisizolingana.

## 4.7 Maudhui yanayohusu matumizi ya lugha

Iwapo mwandishi anaifahamu fika lugha aitumiayo anaweza kucheza nayo ili imtumikie kama apendavyo. Mwandishi hutumia mbinu za lugha kisanaa ili kuficha au kufumba maudhui mazito. Utafiti huu umechanganua mashairi yafuatayo:

"Mkufuu na mwanafuu" (uk 65) na "Kisichoimbwa na M'ngu" (uk 59) katika diwani ya *Malenga wa Mvita*; pamoja na "Dunia jukwaa" (uk 35) na "Alfaqru fakhri" (uk 20) katika diwani ya *Malenga wa Vumba.*

Hata hivyo, mashairi kadha ya *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba* yamehusiana na usanii na usarifu wa lugha kwa njia mbalimbali. Pia, Kuna yale yanayoonyesha desturi ya washairi ya kujigamba na kujitutumua kishairi ili kuonyesha upeo wa ustadi wao katika kuisanii na kuisarifu lugha. Vile vile, kuna mashairi yanayoonyesha ufundi wa kutumia neno lile lile katika kila mstari au

karibu kila mstari kwa maelezo mbalimbali. Aidha, kuna mashairi yaliyotungwa ili kuoonyesha ufundi wa kuuliza na kufumba ujumbe au maana ya mwandishi.

### 4.8 Mkufuu na mwanafuu

Shairi hili lenye beti ishirini na saba ni la bahari ya ngonjera. Kila ubeti una mishororo mitatu na hivyo, ni la aina ya tathlitha. Shairi hili linalitiririsha ujumbe kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho. Hata hivyo, fumbo lenyewe limefumbuliwa au kupewa jawabu katika ubeti wa mwisho. Hivyo, ni shairi linakinzana na maoni ya K. Amri Abedi (1954) yanayodai kwamba ubeti mmoja unajitosheleza kimaana.

Hili ni shairi lililofuata mpango wa 'kufunga nyama'. Ahmadi Nassir ameichanganya kazi ya malenga wawili na kuwaita "mkufuu" (mkufunzi) na "mwanafuu" (mwanafunzi).

Kwa mujibu wa Chiraghdin (1971:17), mkufuu na mwanafuu ni maneno yaliyotokana na fumbo la kale la Kimvita lililosema:

> Cha mkufuu, mwanafuu ha, na akila hu
> Cha mwanafuu, mkufuu hu, na akila ha.

Yaani cha mkufunzi, mwanafunzi hali, na akila hufa; cha mwanafunzi mkufunzi hula na akila hafi.

Kwa hivyo, mada yenyewe inaashiria fumbo. Mwandishi ameufumba ujumbe wake kwa matumizi ya mada ambayo ni fumbo. Msamiati wa kikale, pamoja na msamiati uliokiuka matumizi ya kawaida ya lugha (idhini ya mtunzi kama vile ya kitabdila), pamoja na taswira na picha. Maneno kama "akhana" (ndugu yetu) "tamkini" (hakika), "taratamba" (tupa tupa; hangaika) na "huisi" (hujui),

yanawza kuufumba ujumbe au kumwogofya msomaji na hivyo, kumtenganisha na ujumbe wa mwandishi.

Nahau kama "ninakupa mji" ina maana ya kukubali kushindwa au kutoweza kukifumbua kitendawili. Msemo wa "meta na kuvuka" una maana ya kufanya juhudi zote.

Wahusika wawili wa shairi hili wanadhihirisha jinsi ya kufumbua fumbo. Wanaonyesha kuwa lazima udadisi wa kindani ufanywe. Kwa mfano mkufuu anatega fumbo ifuatavyo:

1. Kitandawili natowa, mwanafunzi taireni
Ameumbwa hana mbawa, umuonapo matoni
Iwapo wamtambuwa, nambia ni ndege gani?

Mwanafuu anaposhindwa kukitegua kitendawili anaanza udadisi wa ndani kwa ndani.

6. Kukuuliza sitindi, suala hazinisha
Na kwamba nawe u fundi, najuwa sitokuchosha
Yuwenda au henendi? Tafadhali nigilisha

Udadisi huu unaakisi mhimili wa kwanza wa nadharia ya udenguzi unaodai kwamba msomaji anapaswa kuchanganua matini na kuitazama kwa jicho la ndani ili kufasiri maana ya matini hiyo. Anapoendelea kudadisi kitendawili alichopewa kwa kina zaidi, mwanafuu anauliza:

24. Jambo jengine akhana, nitakalo kwako wewe
Ni hili sikiza sana, na jawabu nitowe
Yuna ngozi au hana? Hela nambiya nijuwe

Kama yalivyokuwa mashairi ya kufunga nyama aliyeshindwa anatua mji na hivyo, kupewa jawabu la kitendawili au fumbo hilo.

27. Tamati safari yangu, nimekwenda nisharudi

Sasa nafungua pingu, nikweleze uburudi
Ndege wenyewe ndu yangu, ni YAI tuza fuadi

### 4.9 Kisichoumbwa na M'ngu

Hili ni shairi la beti ishirini na nne. Aina ya shairi hili ni tarbia kwa sababu kila ubeti una mishororo minne. Shairi hili lina kibwagizo. Hata hivyo, kibwagizo katika beti kadha ukiwemo ubeti wa kwanza, ubeti wa nne na ubeti wa ishirini nne zimetofautiana na beti nyingine.

Msamiati usio wa kawaida kama vile "thakili" (zito; gumu); "upotole" (upotovu); "asilani" (kabisa); "muthmini" (yenye thamani); "wangwani kuna udindi" (uwanjani kuna ngoma); na "sahibu –li- midani" (mwenye uwanja) yametumika kufumba ujumbe wa mshairi. Hivyo inambidi mfasiri kuuchanganua kwa njia sahihi na kipata maana iliyokubalika na kulingana na muktadha wa utunzi.

Fumbo hili limetiririshwa katika beti zote lakini mtunzi akamwachia mfasiri ya kufumbua mwenyewe.hivyo, ubeti mmoja hauwezi kufumbua kitendawili hiki bali ni shairi zima.

Katika fumbo huwa kuna jambo ambalo limefumbwa ambalo limefumbwa ambalo msikilizaji anahitajika kufumbua labda kwa kujibu swali au kutoa ufumbuzi unaotakiwa (wamitila 2003:104). Shairi hili lina mada inayodhihirishwa kuwa fumbo:

1. Shairi natawakali, wasikizi pulikani
Aishaje mushkili, hatosheka kwa yakini
'Tamnoza mwanamwali, tosa iliyo mtini
Na sasa nisikizani, munijibu hili langu

2 N'a suala thakili, ngumu kwa asobini
Ambayo nawasaili, nisai na ikhiwani
Mwenye fahamu kamili, nanieleze n' nini
Kitu gani duniyani, kisichoumbwa na M'ngu?

Mtunzi amefumbata maana yake kwa lugha nzito, msamiati wa kikale na wa kilahaja pamoja na idhini ya kishairi. Hivyo, itambidi mfasiri anayechanganua shairi hili awe mwangalifu na mvumilivu ili aweze kudondoa maana au ujumbe wa mtunzi. Maneno kama mushkili, pulikani na thakili, yaliyo na maana ya tatizo, sikizeni na gumu mtawalia yanafumbata zaidi ujumbe na huenda yakamwogofya msomaji au mfasiri wa shairi hili.

Mshororo ambaonikitu gani duniyani, kisichoumbwa na M'ngu una sauti nyingine ya ndani inayoweza kutujulisha kuwa kuna kitu fulani kisichoumbwa na mungu. Lakini mwandishi anataja vitu kadha wa kadha vikiwemo vinavyoonekana na visivyoonekana. Kwa mfano:

5. Kitu wenyewe si gari, wala chombo cha angani
Hakitokani na pori, wa chombo baharini
Matoni kiko dhahiri, muonapo kioneni
Kitu gani duniyani, kisichoumbwa na m'ngu?

Mwandishi alimaliza shairi lake bila kututolea jawabu. Hivyo, msomaji ana nafasi kubwa ya kudadisi shairi hili na kulipa maana mbalimbali kulingana na muktadha alimotungia mtunzi pamoja maana nyingine zinazoweza kupatikana katika mazingira ya sasa.

Ujumbe amao unaonekana kuwa wazi ni sauti ya ndani ya shairi inayokusudiwa kutujulisha kuwa kila kitu kimeumbwa na mungu.

### 4.10 Dunia jukwaa

Katika tungo za mbinu za lugha, mshairi hujaribu kudhihirisha ustadi wake katika kuitawala na kuisanii lugha vilivyo. Hivyo, hukitumia chombo hiki cha ushairi ili papo hapo ajisifu ategee wenzake mafumbo au akieleze kitu, jambo au mandhari

Fulani kisanaa hadi picha ya mawazo anayoyasawiri bongoni mwake yajifichue waziwazi.

Mada ya shairi 'Dunia Jukwa' ni fumbo lenyewe kwa sababu neno jukwa ni sitiari kwa sababu jukwaa halisi ni pahali pa kuchezea michezo ya kuigiza. Kulingana na Mnyachama (2004: 127) ulinganisho wa kisitiari hufanya kitu kimoja kisemwe kuwa ni kingine. Hivyo, ni ulinganisho usiokuwa wazi.

Aidha, ulinganishaji wa dunia na jukwaa unaweza kuitwa wa kijazanda. Jazada ni aina ya fumbo ambamo ndani mwake maana ya kitu imefichwa. Jazada na sitiari zinaleta maana sawa ya kitu kilichositiriwa.

Katika shairi hili kama inavyokuwa katika jazada kuna uhamishaji wa sifa za jukwaa kwenda kwa dunia. Jazada ina uhusiano mkubwa na utamaduni pamoja na muktadha wa matumizi jambo ambalo linafungamanisha utafiti huu na uhistoria mpya.

Maneno ya kilahaja pamoja na ya kikale kama vile nduze (ndugu zake); chezato (cheza vizuri); abaa (baba); waoli (watazamaji); na mvina (mchezaji) ni msamiati unaofumba ujumbe wa mwandishi. Kwa hivyo, inamlazimu mfasiri kujua maana ya msamiati usio wa kawaida ili kupata maana iliyofichamwa kwenye lugha iliyotumika.

Maneno kama "mekomaa" (amekomaa); "kwakowe" (kwako wewe); na "tabu" (taabu) ni maneno yaliyotumia idhini ya mshairi ya inkisari kuwatenganisha zaidi wasomaji na ujumbe wa mtunzi.

Mchezo wa lugha umetumiwa kwa namna inayofana zaidi kama ifuatavyo:

6. Ulimwengu karakana, menaa kila vifaa
Tafuta yako supan, uwashe na mshumaa
Ufanye jambo la mana, wapisha mno wasaa
Hii dunia jukwaa, chezato uache jina



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Mwandishi anamaanisha kwamba dunia ina kila aina ua ala au vifaa ambavyo iwapo vitatumika vyema binadamu ataishi vyema duniani.

Kibwagizo hii dunia jukwaa, chezato uache jina kina maana ya kuwa mtu akiwa duniani ajilinganishe na mchezaji wa kuigiza. Mwigizaji hufanya kila awezalo akiwa jukwaani ili aweze kutangazwa mshindi. Maana ni kwamba kila mja afanye yale mazuri na kuacha yali mabaya.

Mshairi anawahimiza watu waishi maisha mema pamoja na kuwasaidia wengine pamoja na wazazi, majirani pamoja na wale wadogo au watu wasiojiweza.

Mshairi pia anaweza kuwa na maana ya kuwa maisha ya duniani ni mafupi kama ilivyo michezo ya kuigiza na kwamba tujale yale tunayofanya katika maisha ya kila siku.

Maana nyingine ni kwamba dunia ni mahali pa kufanya kila aina ya mchezo au mambo (fujo) na kwamba kila mja afurahie kufanya yanayomfurahisha katika maisha yake mafupi.

**4.11 Alfaqru fakhri**

Shairi hili limepewa mada 'Alfaqru Fakhri' maneno yanayotokana na lugha ya Kiarabu yanayomaanisha umaskini ndiyo fahari yangu. Maneno haya ni msemo wenye umbuji na falsafa kubwa. Ni fumbo ambalo likifumbuliwa linapata maana ya kuwa anayeutumia ameridhika na kile apatacho na wala hana haja kamwe ya kujishughulisha au katamanitamani mali ya watu. Mada hii inamtatanisha msomaji kwa sababu imeandikwa kwa Kiarabu, maneno yanayofumba ujumbe wa mtunzi.

Msamiati wa Kiarabu kama vile "Alfaqru fakhri" (umaskini ndiyo fahari yangu); "Qahari" (Mungu) pamoja na msamiati wa kilahaja kama vile "ghubari" (majivuno); "natashakari" (nashukuru) yanachangia katika ufumbaji wa maana ya mwandishi.

Boukheit anatiririsha ujumbe wake kutoka ubeti wa kwanza akieleza sababu za kutosheka na alicho nacho:

1. Kuwa nayo nyingi mali, na wana nyumba chakari
Majumba kila mahali, mema mema ya fakhari
Yote hayo bure ghali, uwapo si masururi
Alfaqru fakhri, 'kiwa ndiyo yangu hali

Mwandishi anasema kwamba hata mtu akiwa ndiye tajiri kuliko wote, au awe na mali nyingi na hata majumba mengi, yote hayo ni bure iwapo mtu huyo hatosheki rohoni mwake.

Katika beti zinazofuata anasuta wale wenye majivuno na wanaojidai kwamba ni matajiri huku wakila vyakula vya kitajiri na kujiwekea ulinzi wa hali ya juu wa kujilindia usalama wao na wa mali yao.

6. Uonapo shambani, mkulima siajiri
Mlinzi najiamini, wa manyani na hinziri
Bunduki siiamini, nyuta zungu ni hatari
Alfaqru fakhri, ndipo nikenda shambani.

Boukheit anaendeleza shutuma zake kwa watu ambao wanapenda pesa sana hata wakafikia kiwango cha kusahau imani yao na kufanya pesa mungu wao. Kwa mfano:

8. Watu wameghafilika, kwa kuabudu dinari
Imani zimewatoks, wendapo huwaza shari
Hawajui kuridhika, tamthili ya kafiri
Alfaqru fakhri, nipatacho hutosheka

Boukheit amekamilisha shairi lake kwa kumwomba Mungu ambariki yeye katika hali hiyo yake na pia kushukuru kuwa Mungu alimuumba akiwa huru.

Aidha, anatoa wito kwa watu wote waishi maisha ya kutosheka, ya uvumilivu na unyenyekevu. Anatoa wito kwa matajiri wawe na moyo wa kutosheka. Shairi hili linaweza kutumiwa kuwaangazia na kuwasuta watu wa kisasa ambao hata wawe matajiri kiasi gani, wanaendeleza tamaa zao kwa kuwadhulumu wale wengine na hata kuiba mali zaidi ili kuwa matajiri zaidi.

## 4.12 Maudhui ya masaibu, majonzi na maliwazo

Utafiti huu umekamilishwa kwa kuchanganya mashairi ambayo kama anwani inavyoeleza yanaeleza mwisho wa mwanadamu kwa lugha inavyostahiki kina cha majonzi na msiba na, kwa jinsi itiavyo ukiwa; lugha yenyewe ina utukufu ulinganao na lugha nyengine yoyote. Sehemu hii imechanganua mashairi wawili: "Kullu nafsiri Dhaaiquatul Mawt" (uk 167) kutoka *Malenga wa Mvita* pamoja na "Inna Lillahi" (uk 109) kutoka *Malenga wa Vumba.*

## 4.13 Kullu nafsin dhaaiqatul mawt

Hili ni shairi lililopewa mada ya maneno yanayotokana na lugha ya Kiarabu. Mada pekee inatosha kufumba ujumbe au maana ya mwandishi kwani si watu wengi wanaoielewa lugha ya Kiarabu.

'Kullu Nafsin Dhaaiqatul Mawt' ni aya ya Kurani tukufu (Sura 21:34) inayoeleza kuwa kila roho itaonja mauti. Shairi lenyewe ni la mpango wa 'takhmis' ambao ndio utumikao kwa mambo ya namna hii.

Ahmadi Nassir ametumia msamiati wa kikale na wa lahaja ya kimvita kufumba ujumbe wake anapoutiririsha kutoka ubeti wa kwanza hadi ule wa saba. Uchanganyika na ule wa Kiarabu unamwacha msomaji katika nafasi ya kuchanganyikiwa. Inabidi mfasiri awe makini sana na pia awe mjuzi lugha zote zilizotumika au apate mwongozo kutoka kwa wajuzi wa lugha hizo ili kupata kufahamu maana ya mwandishi.

Msamiati usio wa kawaida ni kama "fahama na allama" (wenye fahamu na elimu); "tama" (mwisho); "Al-marhumu" (marehemu); "swahilihina" (watu wema); "kadhwa" (amri); "ikabu" (adhabu); na "mahashari" (siku ya kufufuliwa). Mfasiri analazimika kuufahamu msamiati wote au ajaribu kuulinganisha na muktadha iwapo atataka kuufumbua ujumbe wa mwandishi.

Katika mtiririko wa ujumbe wake mwandishi ametumia lugha nzito kujitambulisha kama ifuatavyo:

1. Nduza akhiyari, fahama na allama
Ataimba shairi, hilisha nitiye tama
Lulu na johari, pande moja limezama
Naye ni nasiri. Marehemu bin Juma
Mengiya shubiri, kwa sanda uturi mwema

Ahmadi anaonekana kujiliwaza wakati wa kufikiwa na msiba wa kuondokewa na babaake, marehemu Nasiri wa Jumaa. Anaendeleza maombolezo yake katika beti zote huku akimwombea dua marehemu mwenda zake apate nafasi pale walipo watu wema kama asemavyo:

Rabi mkirirmu, karama zako janna
3. Umpe makamu, nanafasike kusona
Awe muniimu, ja hali ya swahilina
Akitanaamu, suhuba ya swidikina
Rabi mrehemu, kwa nguvu zako Rabana

Mwandishi ametamatisha shairi lake kwa kuwakumbusha watu wote kwamba, siku yao ya kufa ikifika hakuna atakayeweza kuomba muda zaidi. Anasema:

7. Nduli hasairi, siku ya siku 'kifika
Huja kana shari, mikono 'kakuandika
Kwa mbinu za bari, ruhu yako ikatoka
Mwisho ni shubiri, na ubao kufinika
Hadi mahashari, ndipo mja kufufuka.

Ahmadi Nassir amefanikiwa sana kupitisha ujumbe wake kwa lugha ya kidini na ya kumfikirisha msomaji kuhusiana na maisha anayoishi duniani. Shairi hili linaweza kuwa pia mahubiri ya dini ya Kiislamu. Ahmadi amewataja Mitume wengi kama vile Adamu na Hawaa pamoja na Swahaba na ali zake.

Aidha, ametumia msamiati wa Kiarabu unaotumika kwa kiasi kikubwa katika dini ya Kiislamu. Vili vile, ametumia mada "Kullu Nafsin Dhaaiqatul Mawt" ambayo ni sura 21:34 ya kurani tukufu.

### 4.14 Inna lillahi

Hili ni shairi lilitungwa na Boukheit akiomboleza kifo cha mwandishi mashuhuri aliyeitwa Shihabuddin Chiraghdin. Kwa kiasi kikubwa shairi hili linafumba ujumbe wa mwandishi kwa msamiati uliotumika ukiwemo ule wa Kiarabu pamoja na wa lahaja ya Kivumba. Vile vile, lugha yake imeegemea zaidi katika dini ya Kiislamu, swala ambalo huenda likawatenga wasomaji wenye imani tofauti na dini ya Kiislamu. Mada iliyopewa shairi hili ni ya maneno ya Kiarabu kujifunza msamiati wa Kiarabu. Yote haya yanamlazimu mfasiri kusoma kwa makini shairi zima ili kupata maana ya mwandishi. Boukheit anasema:

5. Lau yote nakutubu, kitabu hukamilika
Hayano yalotuswibu, ya kifo kilichotuka
Kifo cha bwana Shihabu, mwalimu alosifika
Si khiyari 'metutoka, mwalimu wetu Shihabu

Ubeti huu wa kwanza ndio unatudokezea ujumbe wa mwandishi huyu kwamba anamwomboleza Shihabuddin wala si mada. Msamiati wa Kivumba pamoja na wa kikale uliotumika ni kama "tumerufaika" (tumeshituka); "muwele" (mgonjwa); "zimetuduru" (zimetuzunguka); "rajiuna" (warudi kwako); "sairaka" (adhabu yako); na "ameihami" (ameikinga) unaleta utata wa kujua maana ya mwandishi moja kwa moja. Msamiati kwa kisai kikubwa hutumiwa na washairi kufumba ujumbe wao. Lazima mfasiri wa shairi awe na ujuzi mpana wa lugha ya Kiswahili pamoja na lahaja zake ili kupata maana ya mashairi mbalimbali.

Boukheit ameutiririsha ujumbe wake kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho kwa kueleza sababu za majonzi yake.

Katika ubeti wa pili anasema kwamba watu wakiwemo wadogo kwa wakubwa wameshitushwa na kifo cha Shihabuddin.

Katika ubeti wa tatu anasema kwamba wote walimlilia lakini machozi hayakumkinga na kifo.

Ubeti wa nne, anasema jina la mwalimu huyu lilijulikana sana na kwamba wengi wataomboleza wakipata habari za kifo chake.

Ubeti wa tano, anamlinganisha shihabuddin na mwanga au nuru iliyowamulikia; yaani mafunzo aliyowapa.

Katika beti zote Boukheit ameonyesha jinsi mwalimu huyu alivyowafaidi wengi wakiwemo wanafunzi na wasomaji wa vitabu vyake.

Boukheit anamaliza shairi lake kwa kumwombea dua ili apewe nafasi nzuri huko 'Janna', yaani peponi au mbinguni kwa Mungu.

Kupitia shairi hili Boukheit amedhihilisha vile alivyomthamini Shihabuddin

na vile vile maandishi yake.

Pili, kupitia shairi lake Boukheit anawafunza waliomwengu kwamba maisha ya duniani ni kama safari na kwamba watende yaliyo mema ili wapate nafasi kwa mungu (Janna).

**4.15 kiishilio**

Kwa mukhtasari, sura hii imechanganua mashairi ya kimafumbo katika diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*. Mashairi hayo yamefumba ujumbe au maana ya waandishi kupitia misamiati ya kikale, ya kikahaja, ya kigeni pamoja na maneno yaliyotumika kwa idhini ya kishairi kama vile yaliyotumia tabdili, mazida na inkisari.

Aidha, watunzi wa *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba* wametumia tamathali mbalimbali za usemi kama vile tashbihi, sitiari na jazada pamoja na mafumbo ya Waswahili na Waarabu ikiwemo ya misemo na misamiati ya kidini.

Ufasiri wa mashairi haya ya kimafumbo umefanywa kwa kuzingatia muktadha wa kitamaduni wa mashairi hayo. Aidha, ufasiri umezingatia mihimili ya nadharia ya udenguzi iliyodai kwamba: lazima matini ipasuliwe katika vipengele vyake mbalimbali ili kuweka wazi maana au ujumbe uliofumbwa. Vile vile, maana kadha

za mashairi teule hupatikana na ambazo haziwezi kuitwa za mwisho. Utafiti huu ulitimiza malengo yake kwa kuzingatia mihimili ya nadharia changamano iliyoteuliwa.

Sura inayofuata imehitimisha kazi hii kwa kujadili eneo la kazi kwa jumla, matatizo na mafanikio ya utafiti pamoja na mapendekezo ya utafiti zaidi utakaohusiana na mada ya utafiti huu.

# SURA YA TANO

## Hitimisho

### 5.0 Utangulizi

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchanganua mashairi ya kimafumbo katika diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba* na kuweka wazi maana za watunzi. Ili kulifikia lengo hili lugha iliyotumika na watunzi wa diwani hizi ilichanganuliwa ili kubainisha mbinu za lugha zilizotumika katika ufumbaji wa maana au ujumbe. Aidha, uchunguzi huu ulikusudia kubainisha au kutoa mwelekeo wa jinsi au namna ya kufasiri maana zilizofumbwa na waandishi. Tumetamatisha kwa kutoa mapendekezo ya tafiti zingine ambazo zinaweza kufanywa kuhusu uwanja huu tulioshughulikia. Utafiti wetu ulifanywa kwa kuzingatia nadharia changamano ambayo ni mseto wa nadharia mbili: nadharia ya udenguzi na nadharia ya uhistoria mpya.

### 5.1 Eneo la kazi kwa jumla

Utafiti huu umejihusisha na uchanganuzi wa mashairi ya kimafumbo katika diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba.* Tumeshughulikia mashairi kumi kwa kuzingatia na mada zifuatazo:

(a) Unyumba: 'Owa' na 'Nenda na bahati yangu' (*Malenga wa Mvita*); 'Mpende akupendae' na 'Leo Homa' (*Malenga wa Vumba*).

(b) Lugha: 'Mkufuu na Mwanafuu' na 'Kisichoumbwa na M'ngu' (*Malenga wa Mvita*) na 'Dunia Jukwaa' na 'Alfaqru Fakhri' (*Malenga wa Vumba*).

(c) Maliwazo/makiwa/majonzi: 'Kullu Nafsin Dhaaiqatul Mawt' (*Malenga wa Mvita*); 'Inna Lillahi' (*Malenga wa Vumba*).

Sura ya kwanza ya kazi hii imeshughulikia mada ambayo tumefanyia utafiti wetu. Katika kushughulikia swala hili, tumeanza kwa kujadili swala la utafiti na kuendelezea kusudi letu la kufanya utafiti huu. Pia, tumeelezea sababu za kuteua swala letu, sababu zilizopelekea washairi kufumba mashairi yao, jinsi ya kufumbua mashairi na upeo wa kazi yetu.

Sura ya pili ya utafiti huu ilichunguza habari zilizowahusu waandishi wa *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba;* historia na utamaduni; shughuli za kuchumi, kijamii na kisiasa; pamoja na matumizi ya lugha katika jamii ya Waswahili.

Kwanza, ilibainishwa kwamba muktadha wa utunzi (historia na utamaduni) huchangia katika ufumbaji wa mashairi.

Pili, Ilibainishwa kuwa utamaduni wa Waswahili ulichangia katika matumizi ya lugha ya kimafumbo katika diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*.

Tatu, elimu na malezi waliyopata Ahmadi na Boukheit kutoka kwa wazazi na jamaa zao, yaliathiri maisha yao. Malezi hayo yaliwapa watunzi hawa wawili msingi wa kutaka kuwapa wanajamii maadili.

Umuhimu wa kuangalia sehemu hizi mbili ni kutoa mwangaza wa kazi iliyokuwa inatafitiwa. Hii ni kwa sababu ufumbuaji wa mashairi haujashugulikiwa sana na watafiti wengi jambo ambalo lilifaa sana na kudokezea historia kwa wasomaji na watafiti wa baadaye.

Katika utafiti huu, imefahamika kuwa mashairi ya *Malenga wa Mvita* yamesheheni fikira nzito, maelezo, maonyo na mafunzo kuhusu matatizo ya kilimwengu yanayomhusu mwanajamii pamoja na maisha yake ya kila siku. Aidha, utu, busara na tabia njema ndiyo falsafa ya *Malenga wa Vumba*. Maelezo haya yanaafiki vyema kipengele cha nadharia ya uhistoria mpya kwamba fasihi haiwezi kutengwa na historia, siasa na jamii ambamo inaibuka. Vile vile, hali zote zinazohusu utamaduni ambamo fasihi hiyo imeibuka hutiliwa maanani.

Sura ya tatu ilichunguza matumizi ya lugha ya kimafumbo katika kazi za mashairi, sababu za ufumbaji, na jinsi mashairi ya *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba* yalivyofumbwa. Aidha, arudhi ya mashairi na migogoro ya utunzi yalishughulikiwa

Sura ya nne ilishughulikia ufumbuaji wa mashairi ya *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*. Sura hii vile vile, ilichanganua njia za ufumbuaji wa mashairi na namna ya kupata fasiri mbalimbali za mashairi hayo.

**5.2 Matokeo, matatizo na mafanikio ya utafiti**

Katika kazi yetu ya utafiti, tulikusudia kuchanganua mashairi ya kimafumbo katika diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*. Haja yetu ya utafiti ilikuwa kuchunguza kama lugha ya kimafumbo inaweza kuchanganuliwa na kuweka dhahiri ujumbe wa mwandishi. Baada ya kufanya hivyo, tumeweza

kufanikiwa na kutambua kuwa lugha ya kimafumbo inaweza kuchanganuliwa na wasomaji wakafaidika kwa kuelewa ujumbe wa mshairi.

Pili, utafiti huu ulibainisha kwamba kuna sababu kadha zinazochangia matumizi ya lugha ya kimafumbo katika utunzi wa mashairi. Utafiti hasa ulilenga mashairi ya diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*. Sababu hizo ni pamoja na tajriba za watunzi; shughuli za kiuchumi, kijamii na kisiasa; historia ya jamii pamoja na utamaduni.

Lengo la pili lilikuwa ni kuchunguza vipengele vya lugha vilivyochangia katika ufumbaji wa maana ya mtunzi. Lengo hili lilitekelezwa katika sura ya tatu ilipochanganua mbinu za ufumbaji pamoja na sababu za ufumbaji.

Utafiti huu uligundua kwamba Ahmadi na Boukheit walitunga mashairi ya aina mbili: mashairi ya kawaida na mashairi ya kimafumbo au mashairi mazito. Aidha, utafiti ulibainisha kwamba Ahmadi Nassir na Boukheit Amana walitunga mashairi ya kimafumbo na kwamba walifumba mashairi yao kwa matumizi ya lugha ya kitamathali, hususan tashbihi, sitiari, jazada na tashira.

Pili, waliweza kutumia methali, misemo na nahau pamoja na msamiati uliokiuka matumizi ya kawaida. Msamiati uliotumika ni wa kikale, wa kilahaja pamoja na ule uliotumia idhini ya mshairi.

Sura ya nne ilifanikiwa kutekeleza lengo la tatu lililokuwa kudhihirisha fasiri za maana za mashairi ya kimafumbo. Aidha, sura hii ilitekeleza lengo la nne lililotaka kudhihiridha kwamba mashairi ya limafumbo yanaweza kupata maana tofauti tofauti kutegemea hali tofauti za kueleza maana.

Matokeo haya yaliafiki kipengele cha nadharia ya udenguzi kwamba ufasiri wa matini hauwezi kufika mwisho na kuwatosheleza wanajamii wote. Wakati wowote matini isomwapo maana hupatikana. Aidha, maana hiyo haiwezi kuitwa ya mwisho.

Utafiti huu ulibainisha kwamba waandishi wa *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba* waliathiriwa na utamaduni, shughuli za kiuchumi, kijamii na kisiasa na mazingira yao kwa jumla.

Kutokana na maelezo ya utafiti huu imedhihirika kwamba, Ahmadi Nassir na Boukheit Amana ni waandishi waliobobea katika matumizi ya lugha kwa sababu walitumia mbinu mbalimbali za kimafumbo zilizopatikana katika jamii zao.

Utafiti huu vile vile umedhihirisha kuwa kuna uhusiano kati ya kazi za kisanaa na jamii ya msanii.

Aidha, uhusiano huo hauwezi kupuuzwa. Hii ni kwa sababu mtunzi ni zao la jamii na kwamba sanaa ni njia muhimu sana ya kuunganisha mwanajamii na wanajamii wengine.

Kazi za mwanafasihi huathiri wanajamii kwa kuwafunza, kuwaonya, kuwaeleza na kuwapa maadili. Kwa muhtasari, utafiti huu umebainisha kwamba Ahmadi

Nassir na Boukheit Amana walitumia mashairi ya kimafumbo katika kuwasilisha maudhui ya *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba.*

Kwa upande mwingine, tuliweza kutatizika katika utafiti wetu kutokana na kutokuwepo kwa maandishi mengi kuhusu mafumbo ya Kiswahili.

Aidha, hatukupata vitabu na tafiti nyingi zilizohusu uchanganuzi wa mashairi ya kimafumbo.

Vile vile, mashairi mengi ya *Malenga wa Mvita* yametungwa kwa lugha nzito. Hivyo, ingebidi kuyachanganua yote jambo ambalo halikufanikishwa na utafiti huu.

## 5.3 Mapendekezo

Utafiti huu umeshughulikia ufumbuaji wa mashairi katika diwani za *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*. Tuliangalia jinsi msamiati, tamathali za usemi pamoja na matumizi mengine ya lugha kama vile methali na misemo yalivyochangia katika ufumbaji wa mashairi. Matumizi ya idhini ya mshairi vile vile yalichanganuliwa kama njia mojawapo iliyotumika katika ufumbaji wa ujumbe wa mshairi.

Kwa hivyo, hatukuingilia maudhui ya diwani hizo kwa undani kwa sababu haja yetu katika utafiti huu ilikuwa ni kuonyesha jinsi ujumbe ulivyofumbwa na jinsi ya kuufumbua. Kwa hivyo, ndiyo sababu tumeingilia kwa undani utamaduni wa mwandishi pamoja na matumizi ya lugha katika diwani hizi.

Ni wazi kwamba kuna mambo mengi ambayo hatukushughulikia na ambayo yeyote aliye na hamu ya kufanya utafiti zaidi kuhusu mashairi ya kimafumbo anaweza kuchunguza.

Hivyo, ni mapendekezo yetu tafiti zingine zifanywe katika nyanja zifuatazo:

Utafiti zaidi unaweza kufanywa ili kushughulikia ulinganishi na ulinganuzi wa lugha kama ilivyotumika katika *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*.

Vile vile, maudhui yaliyoshughulikiwa na malenga wa diwani hizi mbili yanaweza kulinganishwa.

Aidha, utafiti zaidi unaweza kufanywa kubainisha iwapo riwaya, tamthilia au hadithi zinaweza kuwa mafumbo kama ilivyodhihirishwa katika mashairi ya kimafumbo.

Utafiti zaidi katika nyanja hizo utachangia kueleweka kwa lugha ya kimafumbo na hivyo, kurahisisha ufasiri wa matini.

**Marejeleo**

Abdalla, A. (1972) *Sauti ya Dhiki.* Nairobi: Oxford University Press.

------------- (1975) Utangulizi wa mhariri katika *Diwani ya Nyamaume.* Nairobi: Shungwaya Publishers.

------------ (1993) *Ushairi wa Kiswahili Na Uhusishwe Usiuliwe.* Dar es Salaam:Zinduko.

Abdulaziz, M. H. (1979) *Muyaka:19th Century popular Swahili poetry.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Abedi, K. A. (1954) *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri:* East African Literature Bureau, Nairobi.

Amana, B. (1982) *Malenga wa Vumba. Nairobi:* Dar es Salaam: Oxford University Press.

Bloom, H. (1988) *The Anxiety of influence: A Theory of Poetry.* New York: Oxford University Press.

Chacha, M. C. (1987) 'The meaning and interpretation of Swahili poetry'.Ph.D Thesis. Yale University.

Chiraghdin, S. (1971) Utangulizi wa *Malenga wa Mvita.* Nairobi: Oxford University Press.

--------------- (1973) Utangulizi wa *Sauti ya Dhiki.* Nairobi: Oxford University press.

--------------- (1987) *Utangulizi wa Malenga wa Karne Moja,* Nairobi: Longman Kenya limited.

Chiraghdin, S. na S. Nabhany (1975) 'Tarehe ya ushairi wa Kiswahili katika TUKI MULIKA' No.7.: Chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Chiraghdin, S. na M. Mnyampala (1977) *Historia ya Kiswahili.* Nairobi: Longman.

Daiches, D. (1956) *Critical Approaches to Literature.* London: Longman.

Davis R. Na R. Schleifer (1986) *Contemporary Criticism: Literary & Culatural Studies*: Longman London.

Derrida, J. (1976) *Gramatology*. Baltimore, M. d. (Tafsiri kutoka De la grammatologie, Paris: 1967)

Farouk, T. (1969) Utangulizi wa *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili.* Nairobi: Oxford University press.

Greenblatt, S. (1980) "Renaissance Self fashioning". Chicago: University of Chicago press.

Greenblatt, S. na Gallagher, C. (2000) *Practicing New Historicism.* Chicago: University of Chicago.

Gibbe, A.G. (1990) 'Ufumbaji na Ufumbuaji wa Mashairi':Jarida la Kiswahili. Dar es Salaam: Education Service Centre L.t.d.

--------------- (1978) *Ushairi wa Shabaan Robert.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Goring, P. na wenzake (2001) *Studying Literature: The Essential Companion.* London: Anold.

Johnson, F. (1935) *Kamusi ya Kiswahili.* London: Oxford University Press.

Kandoro, S.A. (1972) *Mashairi ya Saadani.* Dar es Salaam: Shirika la Magazeti ya Chama Ltd.

---------- (1977) *Mashairi ya Saadan.*Dar es Salaam: Mwananchi Publishing.

---------- (1978) *Ushahidi wa mashairi ya Kiswahili.* Nairobi: Longman.

-------------(2003).'Hatua mbalimbali za kubuni na kutunga shairi la Kiswahili':Makala za semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III.Dar es Salaam: TUKI.

Kamau, I. (1986) 'The Teaching and Study of literature in secondary schools: where and why we fail'. Tasnifu ya P.G.D.E Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kezilahabi, E (1974) *Kichomi*. Nairobi: Heinemann Education Books.

----------- (1982) *Ushairi wa Shaaban Robert*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

------------ (1973) 'The development of Swahili Poetry : 18th and 20th century' katika Kiswahili.Juzuu 42/2 na 41/1. Uk. 62-67.

Kibao, S.A. (2003) 'Namna ya kujifunza, kuliandika na kulifumbua shairi la Kiswahili': Makala za semina ya kimataifa ya waandishi wa Kiswahili. Dar es Salaam : TUKI.

King'ei K. (2000). *Miale ya Uzalendo*. Nairobi: Phoenix Publishers.

King'ei, K. na A. Kemoli (2001). *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.

------------- (2003) Mwongozo wa Kitumbua kimeingia mchanga: Sasa sema publications.

Knappert, J. (1979) Four centuries of Swahili verse . Nairobi:Heinemann.

Massamba D.P.B. (2003) 'Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili' : Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III .Dar es Salaam:TUKI.

Masinde, E.W. (1992) 'Mashairi Huru: Uchambuzi wa Dhamira na Mtindo'. Tasnifu ya M.A. Nairobi: Chuo kikuu cha Kenyatta.

------------ (2003) 'Ushairi wa Kiswahili: Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui'. Phd. Nairobi: Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Mbaabu, I (1985) *Utamaduni wa Waswahili.* Nairobi : Publishing and Book Marketing.

McGann, J. (1985) *Historical Studies & Literary Criticism.* Madison: University of Wisconsin.

Mohamed, S. A. (1985) *Kina cha Maisha.* Nairobi: Longman Kenya.

------------------ (1977) 'Fani katika sauti ya Dhiki katika MULIKA Na.11. UK.24-32.

------------- (1978) *Asali Chungu* Nairobi : Longman Kenya Limited.

--------------(1980) *Sikate Tamaa.* Nairobi : Longman Kenya Ltd.

Momanyi, C. (1991). 'Matumizi ya Taswira kama kielelezo cha uhalisi katika *Utenzi wa Al- Inkishafi'.* Tasnifu ya M.A.Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

----------(1998). 'Usawiri wa mwananke mwislamu katika jamii ya Waswahili'. Tasnifu ya Ph.D. Nairobi: Chuo Kikuu Kenyatta.

Mnyampala, M. (1965) *Diwani ya Mnyampala.* Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

Msami (1982) Utangulizi wa *Malenga wa Vumba.* Nairobi, Dar es Salaam: Oxford University Press.

Msokile, M. (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: East African Education Publishers Ltd.

Murfin, R.C. (1991) *Case Studies in Contemporary Criticism*. New York: St. Martins Press.

Mwangi, W. J. (2005) 'Ufundishaji wa Ushairi katika Shule za Upili', Tasnifu ya M.A. Nairobi: Chuo kikuu cha Kenyatta.

Nassir, A. (1971) *Malenga wa Mvita: Diwani Ya Ustadh Bhalo*. Nairobi: Oxford University Press.

Ndungo, C.M. (1985). 'Wanawake na mabadiliko ya Kihistoria katika fasihi ya Kiswahili'. Tasnifu ya M.A. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Njogu na Chimera (1999). *Ufundishaji wa Fasihi; Nadharia Na Mbinu*: Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nyanchama, B.M. (2004).'Matumizi ya Taswira na Ishara katika *Sauti ya Dhiki*'. Tasnifu ya M.A. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Nyembembe, J. (1997) *Jinsia: Upeo wa Wanaume na Wanawake*. Nairobi: Paulines Publication.

Odaga, A.B. (1985) *Literature for Children and Young People in Kenya*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Ombuge, K na K. Adaka (1999) Uchambuzi wa Mashairi. Nairobi: Stantex Publishers.

Rice, P. na Wengine (1993). *Modern Literary Theory*. London: Endward Arnold.

Robert, S. (1968) *Kielelezo cha Insha*.London : Nelson.

------------ (1972) *Sanaa ya Ushairi*.Nairobi: Thomas,Nelson and sons.

Ruo, K. R. (1989). *Nguzo za Ushairi wa Kiswahili*: Nairobi: Macmillan.

Sanchez, V.A. (1973).*Art and Suciety*. London: Monthly Review Press.

Scheifer, R. (1994). *Historical Critique* in *Contemporary Literary Criticism, Literary and Cultural Studies*. London: Longman.

Senkoro, F.E.M.K. (1987) *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

--------- (1988) *Shairi: Nadharia na Tahakiki*: Dar es Salaam: University Press.

Syambo, B. na A. Mazrui (1992) *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Publishers.

Wallah, Wallah bin (1988). *Malenga wa Ziwa Kuu*. Nairobi: Heinemann Kenya.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Misingi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publications Limited.

Wekesa, A. (2008). 'Matumizi ya Taswira katika Ushairi huru wa Kiswahili'. Tasnifu ya M.A. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Wellek, R. na A. Warren (1949) *Theory of Literature*. Harmorndsworth: Penguin Books Limited.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY